**Nipashe**

Alhamisi Mei 30, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579931

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Mke, binti na hawara wadaiwa kumuua mume

UK.2







UKURASA 13

# Msako mkali machinga wasio vitambulisho

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**TANZANIA YAPATA SOKO LA MAHINDI ZIMBABWE**

RAIS John Magufuli amesema Tanzania itaiuzia Zimbabwe tani 700,000 za mahindi kutokana na nchi hiyo...

**UKURASA WA 4**

**MAPITIO YA HUKUMU BAGENI MWEZI UJAO**

MAHAKAMA ya Rufani ya Tanzania imepanga kusikiliza mapitio ya hukumu ya kunyongwa ya aliyekuwa Mkuu...

**UKURASA WA 8**

**KAMPUNI ZAPATIKANA MIFUKO YA PLASTIKI**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba, amesema zimepatikana...



Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Alvaro Rodriguez (kulia), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Idara ya Ulinzi wa Amani Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Brigedia Jenerali David Mallugu, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Walinda Amani, katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 26. **PICHA: JOHN BADI**

## Daktari matatani tuhuma kunajisi

UKURASA 3



## Simulizi mwanafunzi kupigwa hadi upofu

• **Aeleza** mkasa mzima ulivyokuwa, muuguzi, wazazi wafunguka, polisi wamng'ang'ania mhusika... *Endelea uk. 2*

**MICHEZO** **TFF YAKIRI KUVURUNDA SAKATA KAGERA SUGAR** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mke, hawara, mtoto wadaiwa kumuua mume

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BONIFACE Agustino (46) mkazi wa Chamwino Manispaa ya Morogoro, anadaiwa kuuawa na mke, mpenzi wake na mtoto wake kwa kupigwa na kitu kizito kichwani kwa kile kinachodaiwa kuwa wivu wa kimapenzi.

Majirani walioshuhudia tukio hilo, akiwamo Mariam Mohamed, walidai kuwa juzi majira ya saa 8:00 mchana, walisikia vishindo na kelele kutoka kwa mwanamume huyo akiomba msaada na kudai kuwa mke wake anataka kumuua huku wakiwa chumbani kwao.

Mohamed alisema, awali mwanamume huyo alikuwa na ugomvi na mke wake, jambo ambalo lilisababisha ndugu kulisuluhisha, lakini wanashangazwa kuona mwanamke huyo akishirikiana na mtoto wake, wamefikia hatua ya kufanya mauaji hayo.

Alidai kuwa mwanamke huyo, Neema Godfrey, alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamume aliyefahamika kwa jina moja la Salum ambaye alikuwa mpangaji wake katika nyumba waliyokuwa wakiishi na mume wake, huku pia mwanamume huyo akiwa na uhusiano wa kimapenzi na binti yake, Alphonsina Boniface. Pia Nipashe ilizungumza na ndugu wa marehemu, Revina Makundi, ambaye alisema kaka yake huyo na mkewe walikuwa na ugomvi kila mara ambao yeye alikuwa akiusuluhisha kuhusu Boniface kumbaka binti yake wakati akiwa mdogo kwa imani za kishirikina.

Aidha, Makundi alisema wanandoa hao walikuwa na ugomvi wa kimapenzi baada ya mpangaji wao kutembea na Godfrey na binti yake, hatua iliyosababisha mpangaji huyo kufukuzwa, lakini baadaye alirudi.

Mtendaji wa Kata ya Chamwino, Bright Sospeter, alisema majira ya 10:00 jioni alisikia watu wakieleza tukio hilo huku wakiwa na hisia za kutokea mauaji ndipo walijumuika na viongozi wengine.

Alisema walipofika eneo la tukio walimhoji mwanamke ambaye ni mke wa marehemu na kusema mumewe alirukwa na akili mchana na ndiyo maana alisema anauawa na muda huo wakati anaulizwa hakuwapo.

Sospeter alisema walipoingia ndani, walimkuta na kumkuta binti na kumuuliza ndipo akasema baba yake alienda kwa Ustaadhi kuombewa, hivyo hayupo jambo lililowafanya walazimike kupekua nyumba nzima na ndipo walipokuta akiwa tayari amefariki dunia akiwa chooni, huku pembeni yake kukiwa na mchi na damu sakafuni. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kusema wanawashikilia watu watatu kwa mahojiano zaidi.

Aliwataja watu hao kuwa ni Neema Godfrey (41) mkazi wa Chamwino, Alponcina Boniface (19) na mtu mwingine ambaye hakumtaja kwa sababu za kiuchunguzi. Mutafungwa alisema inadaiwa kuwa mpangaji aliyekuwa amehamishwa alihusika baada ya kuingia ndani akiwa amevaa vazi aina ya dela hadi usoni na baadaye kutoroka. Aliwataka wananchi wa mkoa wa Morogoro hususan wakazi wa Chamwino, kushirikiana na polisi kufanikisha mtuhumiwa mwingine wa mauaji kupatikana.

# Msako vitambulisho machinga Jumatatu

**Na Mary Geofrey**

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu kama 'machinga' ambao wanafanya shughuli zao bila kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali vilivyotolewa na Rais John Magufuli, wametangaziwa msako mkali kuanzia Jumatatu.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amepiga marufuku wamachinga ambao hawana vitambulisho na kuendelea kufanya biashara katika jiji hilo wataanza kusakwa Jumatatu. Makonda alipiga marufuku hiyo pamoja na msako huo, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, na kusema kuwa Rais Magufuli, aliwakabidhi vitambulisho 175,000.

Alisema kati ya vitambulisho hivyo walivyopewa, amepita katika mitaa zaidi ya tisa na kukuta wafanyabiashara ambao hawajapata vitambulisho hivyo.

"Kuanzia Jumatatu tutaanza kusaka wale wote ambao wanafanyabiashara katika mkoa wetu bila kuwa na vitambulisho. Marufuku kufanyabiashara bila kuwa na kitambulisho," alisema Makonda.

Alisema wapo wafanyabiashara ambao hawana vitambulisho hivyo, na kuwataka ambao hawajapata wafike ofisi za wilaya na kata kwa ajili ya kuvipata.

Alisema kuanzia Jumatatu mfanyabiashara yeyote atakayekutwa hana kitambulisho hicho, atachukuliwa hatua kali za kisheria. Desemba 10, mwaka jana, Rais Magufuli alitoa vitambulisho 670,000 kwa lengo la kuwatambua wafanyabiashara wadogo nchini na kuhakikisha wanafanya shughuli zao bila kusumbuliwa.

Rais Magufuli alitoa vitambulisho hivyo katika mkutano wake na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wakuu wa mikoa yote nchini kujadili namna ya kuboresha mazingira ya ukusanyaji mapato.

Alisema kwa muda mrefu amekuwa akiiagiza TRA na halmashauri kutowatoza kodi wajasiriamali wadogo, ambao mitaji yao haizidi Sh. milioni 4, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Kila mkoa ulipewa vitambulisho 25,000 na kila mjasiriamali mdogo anapaswa kulipia Sh. 20,000 na fedha hizo kupelekwa TRA.

Kwa malipo hayo, kila Mkuu wa Mkoa atakusanya Sh. milioni 500 na ikilazimu aagize vitambulisho vingine kwa ajili ya watakaovihitaji.



Rais Dk. John Magufuli akiwa mbele ya mnara wa Kumbukumbu ya Makaburi ya Mashujaa wa Taifa la Zimbabwe kabla ya kuweka shada la maua nje kidogo ya Jiji la Harare, nchini Zimbabwe jana. **PICHA: IKULU**

# Apata upofu kwa kuchapwa kisa kuchelewa kwenda shule

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MWANAFUNZI Nicholaus Kwimba (17) wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Kate, Nkasi mkoani Rukwa amepata tatizo la uoni kutokana na kupigwa fimbo na mwalimu wake kwenye macho na kumsababishia kushindwa kuona. Kutokana na kitendo hicho, Jeshi la Polisi mkoani Rukwa linamshikilia mwalimu Peter Silamba wa shule hiyo kwa tuhuma za kumpiga na kumsababishia tatizo hilo mwanafunzi huyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Mathias Nyange, alisema tukio hilo lilitokea Mei 21 majira ya saa 2:30 asubuhi shuleni hapo wakati akiwaadhibu wanafunzi waliochelewa kufika shuleni.

Akisimulia tukio hilo mwanafunzi huyo ambaye amelazwa wodi namba tatu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Rukwa mjini hapa, mwanafunzi huyo alisema mwalimu huyo alikuwa akiwaadhibu wanafunzi waliochelewa kufika shuleni na yeye alikuwa mmoja wao.

"Alipomchapa mwanafunzi mwenzangu ambaye alikuwa wa kwanza kuchapwa, mimi nililala chini kisha mwalimu alinichapa viboko viwili wakati akitaka kunichapa cha tatu niligeuza uso na kumwangalia na kisha alinichapa kwenye macho na ghafla nikaacha kuona na mpaka sasa nipo wodini licha ya matibabu ninayopata lakini bado sijaanza kuona," alisema.

Kwimba alisema baada ya mwalimu huyo kumchapa fimbo machoni alimwambia ainuke na kuondoka, lakini alishindwa kutembea kwa kuwa alikuwa haoni.

Mama wa mwanafunzi huyo, Grace Sumuni, alisema baada ya kupata taarifa za mtoto wake kupata upofu baada ya kuchapwa na mwalimu, alikwenda shuleni hapo akiwa ameongozana na baba yake mzazi kisha kumchukua kwa ajili ya matibabu.

"Kwa kuwa huduma za macho zinapatikana Sumbawanga mjini, tuliamua kumkimbiza hospitali ya mkoa ambako alipokewa na kupewa kitanda hatimaye alianza kupatiwa matibabu," alisema.

Mama huyo alisema familia haitaki kesi bali wanachohitaji ni kushirikiana na mwalimu huyo katika matibabu ya mtoto wao, ili aponea haraka na kuendelea na masomo.

Pia aliwashauri walimu kuangalia maeneo ya kuwachapa wanafunzi ambayo hayatawaletea madhara makubwa.

Mhudumu wa wodi aliyolazwa mwanafunzi huyo, Marietha Mwanakatwe, alisema hali ya mgonjwa inaendelea vizuri tofauti na alipofikishwa kwa kuwa amepatiwa matibabu na ametolewa bandeji iliyokuwa imefungwa usoni.

Kamanda Nyange alisema kuwa mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa ili kujibu tuhuma zitakazomkabili.

HABARI KITAIFA

## Tanzania kuiuzia Zimbabwe mahindi tani 700,000

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amesema Tanzania itaiuzia Zimbabwe tani 700,000 za mahindi kutokana na nchi hiyo kukabiliwa na upungufu wa chakula.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu, Rais Magufuli alitoa ahadi hiyo jana muda mfupi baada ya kufanya mazungumzo na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, Ikulu jijini Harare.

Alisema katika msimu uliopita Tanzania ilipata ziada ya chakula ya tani milioni 3.3 baada ya kuvuna tani milioni 16.8, ambapo kati yake mahitaji ya nchi ni tani milioni 13.5.

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli ameikaribisha Zimbabwe kujifunza jinsi Tanzania inavyotoa mafunzo ya kujenga Taifa kwa vijana kupitia Jeshi la Kujenga Taifa

INAENDELEA UK. 8

# Daktari matatani tuhuma kunajisi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limemkamata daktari wa hospitali ya wagonjwa wa akili, Ame Juma Ame (50), kwa tuhuma za kumlawiti kijana mmoja mwenye umri wa miaka 21 (jina linahifadhiwa).

Daktari huyo anatuhumiwa kumwekea dawa za kupoteza fahamu katika juisi kisha kumfanyia unyama huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Thobias Sedeyoka, alisema daktari huyo alimlawiti kijana huyo nyumbani kwake Fuoni Mkoa wa Mjini Magharib Unguja alipomwalika kupata futari.

Alisema Jeshi la Polisi limeshakamilisha uchunguzi na wanatarajia kulipeleka jalada la kesi hiyo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya hatua nyingine za kisheria, ikiwamo mtuhumiwa kufikishwa mahakamani.

Alisema mtuhumiwa huyo yuko nje kwa dhamana kutokana na Jeshi la Polisi kutokuwa na mamlaka ya kumweka mtuhumiwa ndani kwa zaidi ya saa 24.

Kamanda huyo alieleza kuwa mwathirika wa tukio hilo aliahidiwa kulipiwa ada ya chuo na mtuhumiwa huyo, na ndipo alipokwenda kuchukua fedha nyumbani kwake na kumfanyia kitendo hicho.

## TPA, TRA zarushiana mpira foleni bandarini

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), zimetupiana mpira kuhusu msongamano mkubwa wa malori wakati wa ukaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam.

Kwa muda sasa, kumekuwa na malalamiko ya madereva wa malori na wadau wa bandari hiyo kuhusu foleni kubwa inayotokana na ukaguzi na mizani bandarini hapo.

Meneja wa Bandari ya Dar es Salaam, Fred Liundi, aliiambia Nipashe jana kuwa suala la kuchelewa kwa malori hayo wanapaswa kuulizwa TRA kwa kuwa mifumo ya uhakaki ndani ya bandari hiyo inayolalamikiwa na madereva wa malori kuwa chanzo cha foleni ni ya mamlaka hiyo.

Liundi alisema mifumo inayotumika kuhakiki mizigo inayoingia na kutoka bandarini hapo, imewekwa na TRA.

"Suala la mifumo kuleta shida labda uwaulize TRA kwa sababu kama mfumo wa 'clearance' utoaji mizigo uko chini hiyo kasi ya wafanyakazi wanaipata wapi? Mimi labda uniulize ikiwa ile mitambo ya kunyanyua mizigo imeharibika au wafanyakazi wameshindwa kubeba mizigo," alisema Liundi.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, aliruka kimanga na kusema hapajakuwapo na tatizo hilo wiki hii na kumtaka mwandishi kumtajia siku kamili ambapo tatizo hilo lilitokea

"Sina taarifa za mifumo kuleta shida wiki hii labda uniambie muda maalum kwamba ni wakati gani imetokea shida hiyo kwa wiki hii," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
28 - 05 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe 03-06-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dsm Ports kuelekea Kinyerezi Power Plant**, gari hizo zenye namba za usajili:
**T 639 DFE / T 974 CPS / T 406 DFE / T 387 DHQ / T 416 DFE T416 AYQ / T 135 CCP / T 969 CPS / T 628 DFA / T 310 DDH**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.65** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.10** |

3. Njia itakayotumika: **Dsm Ports hadi Kinyerezi** Kupitia Tabata, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115253702



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
28 - 05 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe 03-06-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dsm Ports kuelekea Kinyerezi Power Plant**, gari hizo zenye namba za usajili:
**T 277 AZB / T 380 DHQ / T 528 BKC / T 830 DJB / T 911 BTE T 605 AUE / T 633 DFE / T245 BYM / T 559 BKC / T 890 DJB**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.65** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.10** |

3. Njia itakayotumika: **Dsm Ports hadi Kinyerezi** Kupitia Tabata, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115253702



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
28 - 05 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe 03-06-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dsm Ports kuelekea Kinyerezi Power Plant**, gari hizo zenye namba za usajili:
**T 624 DFA / T 485 AGZ / T 411 DFE / T 256 DYM / T 156 BTE T 139 CHN / T 261 BXH / T 892 DJB / T 798 AUX / T 251 BYM**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.65** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.10** |

3. Njia itakayotumika: **Dsm Ports hadi Kinyerezi** Kupitia Tabata, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115253702



**MAJEMBE AUCTION MART LTD**
**(VIJANA WA KAZI)**

**MNADA WA HADHARA**

Kwa niaba ya Shirika La Nyumba la Taifa (NHC), Tutauza mali za wadaiwa wote Wa shirika la Nyumba zilizochukuliwa wakati wanaondolewa kwenye majengo ya Shirika la nyumba baada ya kushindwa kulipa kodi ya pango.

**MNADA UTAFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI 01/06/2019 KUANZIA SAA 5;00 ASUBUHI,KWENYE YARD YETU ILIYOPO MBEZI BEACH KARIBU NA RAINBOW HOTEL.**

| | |
|---|---|
| **MAJINA YA WADAIWA** | MAKATU KAKURU,NDIBALEMA HENRY,ISC CO LTD,TRANSPORT RESOURCES,RYOBA LEAH, MOHAMED NIYAMAT, SABIRA RATTANSI,MWIMANZI PROSPER, MUKESHI GLOBAL ESTATE,CARGO WORX, MARYS EXECUTIVE LODGE. |
| **MALI ZITAKAZOUZWA** | SIMU ZA MKONONI,MEZA,VITI,TV,DECK, PLAYER,CAMERA,PAD,COMPUTER,SCREEN,KABATI, ALLUMINIUM,FILE CABINET,PRINTER,JOKOFU, GENERATOR,GAS,KIOO,STABILIZER,SOFA SET, CRATE ZA SODA,MITUNGI YA MOTO (MALI NI NYINGI SANA) |

**MASHARTI YA MNADA:**
a). Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili kutoka.
b). Mnunuzi atakayeshinda, atalipa 100%.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA.**
**0712 964561,0715735655,0754301930,0715868000**

115252802

# Mamia wafurika kupima saratani

**Na Elisante John,** SINGIDA

WAKAZI wa Mkoa wa Singida, wamefurika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa kupima saratani kutoka kwa madaktari bingwa wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) ya Dar es Salaam, ili kubaini kama wana viashiria vya maradhi hayo.

Hatua hiyo ni mpango wa serikali katika kuhakikisha inadhibiti magonjwa ya saratani nchini, hivyo kuiwezesha jamii kushiriki vyema kwenye shughuli za kiuchumi. Timu ya madaktari bingwa wa magonjwa ya saratani, pathologia na wataalamu wa tiba shufaa kutoka ORCI, wanaendesha upimaji huo kwa siku saba kuanzia jana, mjini hapa katika hospitali hiyo.

Meneja wa Kitengo cha Saratani kutoka ORCI, Dk. Magula Stephano, alisema katika muda huo wa siku saba, wanawake na wanaume watafanyiwa uchunguzi wa awali juu ya saratani za mlango wa kizazi, matiti, tezi dume na ngozi kwa watu wenye ualbino bila ya gharama yoyote.

"Naona jamii hivi sasa imeanza kuelewa umuhimu wa kufanyiwa uchunguzi huu. Katika siku ya kwanza, tayari tuna wanawake watatu na wanaume wawili waliopima afya zao, ambao wameonekana kuwa na viashiria vya saratani. Huu ni mwanzo mzuri," alisema Dk. Stephano. Alisema licha ya taasisi yake kuhusika na upimaji, pia itatoa mafunzo ya magonjwa ya saratani kwa madaktari na wauguzi wa halmashauri za wilaya za mkoa wa Singida na wagonjwa wa saratani watakaobainika, watapatiwa huduma ya tiba shufaa.

Akifungua huduma hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Angelina Lutambi, aliwataka wakazi wa Singida kuchangamkia fursa hiyo ili kunufaika na tiba zinazotolewa na madaktari bingwa, hali ambayo pia itaokoa gharama za kusafiri hadi jijini Dar es Salaam, kusaka matibabu.



Wahitimu wa Shahada ya Umahiri katika Uongozi wa Biashara (MBA), Mhasibu wa Kampuni ya The Guardian Ltd, Jackson Paulo (kulia), Angela Costantino (katikati) na Davis Matola, wakifurahia jambo katika mahafali ya 49 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, yaliyofanyika katika ukumbi wa Nkrumah chuoni hapo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mapitio ya hukumu ya SP Bageni Juni 16

**Na Hellen Mwango**

HATIMAYE Mahakama ya Rufani ya Tanzania imepanga kusikiliza mapitio ya hukumu ya kunyongwa ya aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Kinondoni (kwa sasa mkoa wa kipolisi Kinondoni), Mrakibu wa Polisi (SP) Christopher Bageni Juni 16, mwaka huu.


Maombi hayo ya mapitio yamefunguliwa mahakamani hapo na mshtakiwa yakiwa na sababu mbalimbali ikiwamo kupinga hukumu iliyotolewa Septemba 16, 2016.

Mapitio hayo yamepangwa kusikilizwa mbele ya jopo la majaji watatu wakiongozwa na Jaji Stella Mugasha, akisaidiana na Ferdinand Wambari na Rehema Kerefu.

Pamoja na mambo mengine, katika maombi yake, SP Bageni anapinga hukumu iliyotolewa katika mahakama hiyo chini ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Bernard Luanda akisaidiana na Sauda Mjasiri na Sen-istocles Kaijage kwamba lilifanya makosa ya dhahiri.

Pia anadai kuwa jopo hilo lilifanya makosa katika mwonekano na kusababisha haki

INAENDELEA UK.8



# Ofisa Tanroads, mkandarasi kortini tuhuma za rushwa, kutakatisha fedha

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kigoma, imewafikisha watu wawili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma kwa tuhuma 11, kati ya hizo 10 ni za ukiukwaji wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Nyingine ni utakatishaji fedha Sh. milioni 24.6.

Washtakiwa hao ni Mhandisi Ofisi ya Wakala wa Barabara (TANROAD) Mkoa wa Kigoma, Geofrey Mutakubwa (44) na Mkurugenzi wa Kampuni ya KAGECO Civil Works and Building Contractors ya Kigoma, Theonest Bagasingire (52).

Watu hao walipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Flora Mtarania na waliposomewa mashtaka yao, walikana kuhusika na wako mahabusu katika Gereza la Bangwe kwa sababu shtaka la utakatishaji fedha halina dhamana kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Mwendesha Mashtaka kutoka Takukuru Mkoa wa Kigoma, Boniface Kamwesigile, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo ya uhujumu uchumi Na. 3/2019 haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Mtarania alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Juni 10, mwaka huu.

Akisoma hati ya mashtaka, Kamwesigile alidai kuwa kati ya Februari, 2017 na Januari 2018 maeneo ya Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa wa kwanza, Mutakubwa, alitenda makosa sita kwa kutumia mamlaka vibaya, kujipatia manufaa yasiyo halali, kujihusisha na vitendo vya rushwa katika ununuzi na kujihusisha na vitendo vya rushwa katika mikataba, huku Bagasingire akikabiliwa na makosa manne ya kujihusisha na rushwa katika ununuzi na mikataba.

Kamwesigile aliendelea kudai kuwa washtakiwa wote kwa pamoja walitenda kosa la utakatishaji fedha Sh. 24,600,000 kupitia akaunti za benki ya CRDB Tawi la Kigoma, Urambo Tabora na Ubungo, Dar es Salaam, huku wakijua kuwa fedha hizo zilikuwa mazao ya rushwa.

TANGAZO


www.tigo.co.tz
SAIZI YAKO
Saizi Yako
Furahia SAIZI YAKO!
Ofa maalum kwa ajili yako
*147*00# au *148*00#
tigo
Ofa inapatikana kwenye *147*00#, *148*00# na Tigo Pesa App
215253302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vijengwe viwanda vya kurejeleza plastiki

**WATANZANIA** bila shaka wanafahamu kuwa siku imefika kwa taifa kuingia kwenye zama za mwisho za kutumia mifuko ya plastiki.

Hapa nchini mifuko hiyo ni bidhaa ambazo zimetumiwa kwa miongo kadhaa.

Mifuko ambayo kuanzia sasa haitatumiwa ni kuanzia ile laini yenye viwango duni kiasi kwamba hata ukiweka bidhaa zinaweza kudondoka wakati wote kwa vile kifungashio hicho hakina kiwango wala sifa za kuhimili uzito.

Mifuko hiyo ikiwamo mingine mikubwa inayoitwa Rambo ina sifa mbaya ya kuchafua mazingira kuanzia viwanja vya nyumbani, shule, sehemu za wazi, vyanzo vya maji pamoja na baharini.

Kwa ujumla huharibu mazingira ya juu na chini ya ardhi kwa kasi ya kutisha na isiyo na dawa wala ufumbuzi wa haraka kwa kuwa pamoja na kuua viumbe wa baharini na nchi kavu, taka hizi haziozi zikielezewa kuwa zinaishi kwa miaka zaidi ya 500 hata 1,000.

Kwa hali kama hiyo ni lazima plastiki iondoke na kwa kuanza ni kuchukua hatua kama hizo, ndiyo maana serikali imepiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo ambayo kuanzia Juni mosi haitatumiwa popote, badala yake mifuko yenye viwango vinavyokubalika ambavyo vimeshaidhinishwa na wataalamu wa mazingira, afya, ubora na usalama wa bayoanuai vitachukua nafasi yake.

Tunaunga mkono juhudi za serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko duni ya plastiki ambayo ni kitisho kwa maisha, lakini tunapenda kuishauri kuwa ni lazima kuwa na vifungashio bora na mbadala wa plastiki.

Tunasisitiza kwa uzito wa kipekee kujenga maeneo maalumu ya kukusanya bidhaa zote za plastiki ili zitumike kama malighafi za viwanda vya kurejeleza.

Ni wazi kuwa mbali na mifuko ya plastiki kuna tani kadhaa za mabaki ya bidhaa hizo kama vyombo vya nyumbani, maua, matairi, vifaa vya ofisini, maturubai, makasha ya kufungashia bidhaa kama soda na bia na kwa ujumla, mbali na mifuko hiyo nchi ina mabilioni ya tani hizo za mipira ambazo haiozi.

Shime serikali na wadau, kupiga marufuku mifuko ya Rambo na jamii za plastiki kunakoanza kesho kutwa, kuwe mwanzo wa kuhimiza ujenzi wa viwanda vya kurejeleza na pia maeneo mengi yakiwamo mijini na vijijini yatakayotumika kukusanya taka zote za plastiki ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Bidhaa za plastiki hutumiwa popote kuanzia mijini hadi vijijini tena kila dakika hutumiwa kufungasha bidhaa, mizigo, shehena na zama hizi imeibuka kuwa miongoni mwa bidhaa zenye bei nafuu ikilinganishwa na chuma.

Kwa maneno mengine ni wazi kuwa matumizi ya plastiki yasiyo ya mifuko hayakwepeki. Cha kuangalia sasa ni ubunifu wa namna ya kufanya maandalizi mazuri ya kulinda watu na bayoanuai isiangamizwe na bidhaa hizo.

Kwa kuwa ufungashaji bidhaa nao ni jukumu la kudumu kutengeneza vifungashio mbadala ni kazi ya kila mmoja.

Tunashauri wanaozalisha bidhaa waone umuhimu wa kuwa na vifungashio visivyoharibu mazingira na kuachana na plastiki.


Pengine ni wakati wa kuandaa sera za kuhamasisha viwanda, kampuni maduka makubwa na wawekezaji kuzalisha vifungashio vinavyooza ili kuondoa plastiki.

Tunaishauri taasisi za kitafiti na mafunzo ya ufundi kubuni teknolojia rahisi za kutengeneza vifungashio ili ziwe fursa za ajira kwa vijana, lakini pia kuendeleza harakati za kuondokana na plastiki zinazoharibu mazingira.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kigoda cha Mwalimu Nyerere kitumike kukuza Kiswahili

Na Beatrice Moses

**TAMASHA** la Kigoda cha Mwalimu Nyerere, ni jukwaa la aina yake linalotumiwa na wasomi kutoa hoja na kujadili mada zinazohusu mambo ya Afrika na vikwazo vinavyoikabili.

Katika tamasha hilo la 11, pamoja na wasomi wengine kadhaa kuwasilisha mada zao, Profesa Patrick Lumumba kutoka nchini Kenya, alikuwa ni miongoni mwa wawasilishaji mada.

Anasema, kuna yanayoonekana kuwavutia wengi, kutokana na uwezo wake wa kuchambua mada kwa ufasaha.

Profesa Lumumba, mbobezi wa taaluma ya sheria, anaeleza kuwa Afrika imekuwa dhaifu, hivyo inakwama kushindana na mataifa mengine, kwa sababu imegawanywa na wakoloni.

Anabainisha kuwa Wachina ndiyo wanaojenga viwanja vya michezo Afrika. Je, hapa Dar es Salaam imejengwa na nani? Wamejenga kule Nairobi, Kenya, hata Uganda na nchi nyingi za Afrika wanaendelea kujenga?

"Hakuna chakula cha bure, Wachina wameshajua udhaifu uliopo Afrika, ndiyo maana wanaona njia nyepesi ya kushika ufahamu wetu ni kuwekeza hata katika taasisi za elimu ya juu," anasema.

Profesa Lumumba anasema, hivi sasa China imeanza kupandikiza utamaduni wake, kwa kutumia lugha yake inayoweza kumeza utamaduni wa Afrika.

Anasema Kiswahili ni miongoni mwa zana zinazoweza kutumika katika mawasiliano ya Waafrika, katika masuala ya biashara na elimu, hivyo kuunganisha nguvu ya kuimarisha umoja kama ilivyo, kwa nchi za Ulaya zinavyotumia Kiingereza.

Ni vyema ifike wakati sasa, waandaaji wa Kigoda cha Mwalimu, wawe mfano wa kuendeleza nadharia za Mwalimu Nyerere kwa vitendo, kwa kuiwezesha lugha ya Kiswahili iwe ndiyo lugha kuu.

Nasema hivyo, kwa sababu lugha kuu inayotumiwa kwenye tamasha hilo ambalo mwaka huu limedhaminiwa na Uongozi Institute, taasisi ya Haki Elimu na Benki ya CRDB inatawaliwa katika lugha ya Kingereza.

Wazungumzaji wengine katika tamasha hilo, ni pamoja na mfanyabiashara mahiri, Ali Mufuruki, aliyezungumzia kuhusu mustakabali wa soko huria na dola.

Profesa Georges Ntalaja, raia wa Kongo anayeishi Marekani, alizungumzia dhana ya utawala bora na siasa, huku Profesa Paul Zeleza kutoka Malawi, Dk. Suzan Kavuma Uganda aliwasilisha mada kuhusu hali ya Uganda katika kuendeleza viwanda.

Watoa mada wote walitumia lugha ya Kiingereza kuwasilisha mada zao na kwa nadra miongoni mwao, ndio walidokeza Kiswahili.

Profesa Lumumba anataja methali ya Kiswahili kuwa ni "Vita vya panzi furaha ya kunguru." Alitumia methali hiyo kuonyesha jinsi mgawanyo au migogoro kwa mataifa ya Waafrika, inavyoutumiwa vyema na mataifa ya kigeni kujinufaisha na rasilimali za Afrika.

Inatimu miaka 20 sasa, tangu kufariki Mwalimu Julius Nyerere, Oktoba 14, 1999. Miongoni mwa maono yake, ni kuona Afrika inakuwa na maendeleo na kumudu kujitegemea kiuchumi na kukuza lugha ya Kiswahili aliyoiamini inaweza kutumiwa vyema kuliunganisha bara la Afrika.

Hivi karibuni, vyombo vya habari kadhaa na mitandao ya kijamii, imebainisha kuwa Afrika Kusini iliidhinisha lugha ya Kiswahili kufundishwa katika shule za nchi hiyo Septemba 2018, utekelezaji wake utaanza mwaka 2020.

Hatua hiyo ni fursa kwa walimu wa lugha ya Kiswahili kutoka Afrika Mashariki, hasa nchi za Tanzania na Kenya ambako lugha hiyo ni rasmi.

Ni wazi kuna wataalamu wa kutosha na wana sifa inayojitosheleza kwenda katika nchi hiyo kufundisha lugha hiyo maridhawa.

Kwa hiyo naamini, Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu, Profesa Rwekaza Mukandala, aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na wakati fulani, Mkuu wa Idara ya Sayansi ya Siasa na Uhusiano wa Umma, ataona umuhimu wa kutumia jukwaa hilo kukuza Kiswahili barani Afrika, iwe lugha kuu zaidi.

Natambua kwamba ni jukwaa linalokusanya wasomi kutoka mataifa mbalimbali, wakiwamo wasiojua lugha ya Kiswahili. Ni vyema wakawekewa watafsiri wa lugha, ili nao waanze kuona umuhimu wa kujifunza Kiswahili.

## HABARI KITAIFA

# Mikataba gesi asilia yaanza kufumuliwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema iko katika mchakato wa kuirekebisha mikataba yote ya gesi asilia ili ilinufaishe taifa kama ilivyopendekezwa na kamati maalum iliyoundwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai kuchunguza maendeleo ya sekta hiyo.

Novemba 2017, Spika Ndugai, kwa mamlaka aliyonayo kisheria, aliunda kamati maalum mbili kuchunguza na kuishauri serikali kuhusu mwenendo wa sekta ndogo ya gesi asilia na uvuvi wa bahari kuu.

Kamati hizo mbili zilikabidhi ripoti zake kwa Spika Ndugai mwaka jana na baadaye kiongozi huyo wa Bunge kuzikabidhi kwa serikali ili zifanyiwe kazi.

Katika mapendekezo yake, pamoja na mambo mengine, kamati iliyochunguza sekta ndogo ya gesi asilia, iliitaka serikali kuifanyia marekebisho mikataba yote ya gesi iliyoingia na wawekezaji ili kulinufaisha taifa na iende sambamba na sheria mpya zinazohusu rasilimali za taifa zilizotungwa na Bunge hivi karibuni.

Akichangia bungeni jijini Dodoma jana mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Adelardus Kilangi, alisema kuwa baada ya kupitia mikataba ya uchimbaji na utafutaji gesi, ofisi yake imebaini upungufu katika mikataba hiyo.

Alisema serikali inachambua na kuangalia muundo upi wa kifedha na kiuchumi utakaotumika ili Tanzania kupata faida kutokana na mikataba hiyo.

Alisema hatua iliyofikiwa ni ya utekelezaji wa mapendekezo ya kamati iliyoundwa na Spika Ndugai kuchunguza namna taifa linavyoweza kunufaika kwenye sekta ndogo ya gesi. Dk. Kilangi alilazimika kulitolea ufanunuzi suala hilo kutokana na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhoji bungeni utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya kamati iliyoundwa na Spika huku Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia (CCM) akihoji pia sababu za serikali kutotoa leseni mpya za uchimbaji na utafutaji wa gesi.

Dk. Kilangi alijibu akisema: "Mheshimiwa Spika, moja ya mapendekezo ya kamati uliyounda kuchunguza sekta ndogo ya gesi na uvuvi, ni kurejea mikataba ya utafutaji na uchimbaji.

"Kazi hiyo ikapewa ofisi ya AG (Mwanasheria Mkuu wa Serikali). Tulianza kazi kuipitia mikataba yote, tukaunda timu kutoka wizara na sekta mbalimbali za serikali."

Dk. Kilangi alisema ofisi yake ililazimika kuijengea uwezo timu hiyo ya wataalamu na baadaye ilianza kupitia mkataba yote 11 ya utafiti na uchimbaji gesi.

Alibainisha kuwa timu hiyo aliangalia muundo gani wa kifedha na kiuchumi uliotumika na ikagundulika lazima kama nchi, kuangalia mfumo upi utumike na kazi hiyo itafanyika kunzia Juni 6-25, mwaka huu.

# Bil. 119/- zalipa wastaafu mapunjo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umetumia Sh. bilioni 119 kulipa wastaafu waliopunjwa mafao ambao awali walilipwa kwa kutumia kikokotoo kipya.

PSSSF pia imeeleza kwamba Sh. bilioni 880 zimetumika kulipa mafao kwa wastaafu 10,000, huku wengine 227 wakisubiri hatima yao kutokana na kuwekewa pingamizi na mwajiri.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu kukutana nao kila Jumatano ya mwisho wa mwezi, Meneja Kiongozi anayeshughulikia Uhusiano wa PSSSF, Eunice Chiume, alisema baada ya mifuko kuunganishwa ulipaji mafao kwa wastaafu wote wa mifuko minne ulikamilika Februari, mwaka huu.

Chiume alisema wakati ulipaji ukiendelea, Rais alitoa agizo la kutumika kwa kikokotoo cha zamani na kulazimika kuwalipa wastaafu waliopunjwa mafao yao.

"Tuliendelea kulipa mapunjo kutokana na kikokotoo kurudi kile cha zamani. Takribani Sh. bilioni 119 tumetumia kulipa na yenyewe wameshamalizika," alisema.

Aidha, alisema mafao ya wastaafu wote ambao walikuwa hawajalipwa kwa takribani miaka miwili ambao walirithiwa na PSSSF hadi Februari, mwaka huu, walikuwa wamelipwa wastaafu wote takribani 10,000.

"Tuliwalipa Sh. bilioni 880, lakini pia tukumbuke Desemba, mwaka jana, mwishoni, kulikuwa na maagizo ya Rais kuhusu kubadilika vikokotoo kwa hiyo pamoja na kwamba tulimaliza mwezi wa pili kulikuwa na malimbikizo ya kikokotoo," alisema.

Alisema hivi sasa wanalipa pensheni za kawaida za kila mwezi kwa wastaafu 124,000 pamoja na wategemezi wao.

Kuhusu wastaafu 227, meneja huyo alisema bado hawajalipwa ingawa mafao yao yametayarishwa kutokana na kuwekewa pingamizi na mwajiri kwa madai mbalimbali.

"Tunasubiri pingamizi ziondolewe maana wako ambao walisimamishwa kwa vyeti feki, masuala ya kinidhamu na kesi za kijinai. Hawa wakipata 'clearance' kutoka kwa mwajiri sisi tunawaingiza kwenye daftari letu," alisema.

Akizungumzia malalamiko ya baadhi ya wastaafu kutolipwa mafao yao, Chiume alisema watu wanaolalamika wengi ni wale ambao hawajalipwa kutokana na kuwekewa pingamizi la vyeti feki.

"Mtu hajalipwa, lakini ukifuatilia unakuta yule mmoja ambaye labda suala la vyeti feki na utaona kuna pingamizi lilishatolewa na mwajiri labda msimamisheni mtoeni kwenye daftari la wastaafu mpaka atakapomaliza suala lake, kuna wengine mpaka walishaandikiwa cheki ikaenda lakini tukaambiwa hao wana matatizo," alisema.

Alibainisha kuwa walikuwa wengi na lakini hadi sasa wamebaki 227 kutokana na kila barua inapotolewa na mwajiri ya kuruhusu kulipwa mafao wamekuwa wakilipa bila kuchelewa.

Alisema kila mwaka hufanyika uhakiki wao ikiwamo wa taarifa za benki, hivyo baadhi hulalamika kutolipwa wanakuwa hawajahakiki taarifa zao.

Kuhusu Jumatano ya PSSSF, meneja huyo alisema wameamua kuanzisha siku hiyo ili wawe wanaeleza kinachoendelea kwenye mfuko huo.

"Hadi sasa mfuko una wanachama 763,000 na wastaafu 124,000 ambao wanalipwa pensheni za kila mwezi," alisema.


**HALMASHAURI YA MJI KAHAMA**

**TANGAZO LA ZABUNI**

**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03**

1. Halmashauri ya Mji Kahama inakaribisha maombi ya Zabuni za huduma mbalimbali zisizokuwa za kitaalam,bidhaa na kazi mbalimbali kutoka kwa watu binafsi,vikundi au kampuni zenye kutoa huduma hizo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020
2. Hivyo basi Halmashauri ya Mji Kahama inakukaribisha kuleta maombi yako kwa ajili ya huduma zisizo za kitaalam, bidhaa na kazi kama zilivyoelezwa kwenye orodha hapa chini.

| | |
|---|---|
| **A.** | **ZABUNI ZA HUDUMA ZISIZO ZA KITAALAMU(Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/01)** |
| 1 | Uchapishaji wa nyaraka mbalimbali (printing services)<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/01** |
| 2 | Huduma za kunyonya maji taka<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/02** |
| 3 | Huduma ya matangazo ya sauti(public advertisement)<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/03** |
| 4 | Huduma ya ulinzi kwenye majengo na ofisi za Halmashauri<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/04** |
| 5 | Huduma ya usafi kwenye majengo na ofisi za Halmashauri<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/05** |
| 6 | Huduma za kukarabati vifaa tiba (preventive and mantainance)<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/06** |
| 7 | Huduma ya kukodisha viti ,meza,mapambo na mahema<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/07** |
| 8 | Huduma ya ukarabati vifaa vya ofisi (ambavyo ni scanners,photocopy machine computer,printer,ups)<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/08** |
| 9 | Huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/09** |
| 10 | Kupangisha vibanda 12 katika soko la Namanga –kodi TZS 60,000/= kwa mwezi<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/10** |
| 11 | Kupangisha meza sabini katika soko la Namanga –kodi TZS 10,000/= kwa mwezi<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/11** |
| 12 | Kuendesha choo cha soko la Majengo<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/12** |
| 13 | Huduma ya kukusanya na kusafirisha taka ngumu<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/13**<br>Zabuni hii itafanyika katika maeneo yaliyo gawanywa katika kanda mawili kama ifuatavyo:-<br>Kanda A:-Kuzoa taka ngumu kwenye vizimba vya kata za Nyasubi, Majengo, Kahama Mjini, Malunga, Mhungula, Nyihogo,Nyahanga na Busoka na kuzipeleka bampo kuu la Busoka<br>Kanda B:-Kukusanya ada, kuzoa taka ngumu na kuzisafirisha moja kwa moja kwenda dampo la Busoka katika kata za Kagongwa, Mwendakulima, Mhongolo na Zongomera |
| **14** | Kuendesha choo cha parking ya malori Majengo<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/14** |
| **15** | Kuendesha choo cha stendi kuu ya mabasi<br>**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/15** |
| **16** | Utangazaji stendi kuu ya mabasi ,stendi ndogo,stand ya CDT na stendi ya viwanda Dodoma. **Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/16** |
| **B.** | **ZABUNI ZA BIDHAA (Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/G/03)** |
| 1 | Huduma ya kuuza matofali. **Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/01.** Wazabuni waliomba na kupitishwa mwishoni mwa mwaka huu wa fedha wataendelea na mikataba yao. Wazabuni waliopitishwa mwezi wa Julai mwaka 2018 wanatakiwa kuomba upya pamoja na wengine wapya wanaohitaji kuingia kwenye uzabuni |
| 2 | Huduma ya kuuza mitunga ya Gesi. **Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/02** |
| 3 | Huduma ya kuuza mawe ,mchanga, kokoto na moramu. **Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/03.** Wazabuni waliomba na kupitishwa mwishoni mwa mwaka huu wa fedha wataendelea na mikataba yao. Wazabuni waliopitishwa mwezi wa Julai mwaka 2018 wanatakiwa kuomba upya pamoja na wengine wapya wanaohitaji kuingia kwenye uzabuni |
| 4 | Huduma ya kuuza mbao na mirunda. **Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/NC/03/04** |
| **C.** | **ZABUNI ZA KAZI ZA UJENZI (ZABUNI NA. LGA/155/2018/2019/W/03)** |
| 1 | Huduma ya ukandarasi(contractors pre-qualification) wa majengo,barabara,umeme,air condition na majokofu.(**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/W/03/01).** Wakandarasi waliomba na kupitishwa mwishoni mwa mwaka huu wa fedha wataendelea na mikataba yao. Wakandarasi waliopitishwa mwezi wa Julai mwaka 2018 wanatakiwa kuomba upya pamoja na wengine wapya wanaohitaji kuingia kwenye uzabuni |
| 2 | Mafundi ujenzi mbalimbali(local Fundi).<br>(**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/W/03/02).** Mafundi waliomba na kupitishwa mwishoni mwa mwaka huu wa fedha wataendelea na mikataba yao. Mafundi waliopitishwa mwezi wa Julai mwaka 2018 wanatakiwa kuomba upya pamoja na wengine wapya wanaohitaji kuingia kwenye uzabuni |
| 3 | Mafundi wa kuchomelea (Welding). (**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/W/03/03)** |
| 4 | Mafundi umeme ambao siyo wakandarasi, mafundi selemala. (**Zabuni Na. LGA/155/2018/2019/W/03/04)** |

**3. MASHARTI KWA WAOMBAJI**

1. Mwombaji awe na leseni hai kwa biashara husika, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi(TIN),usajili wa kampuni,usajil wa VAT kwa wale wanaokidhi matakwa ya kusajiliwa kwenye VAT,uhalali wa kisheria wa kusaini nyaraka (Power of attorney).
2. Mwombaji ataje kiasi cha asilimia (%) atakacholipwa na Halmashauri kutoka kwenye makusanyo.Makusanyo yote yanatakiwa kuingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri.Mwombaji atatakiwa kulipa dhamana ya mwezi mmoja kabla ya kusaaini mkataba.Afanye utafiti kabla ya chanzo kabla ya kuomba.Asiwe anadaiwa kodi ya aina yoyote na Halmashauri.
3. Kwa upande wa huduma tofauti na kukusanya mapato mwombaji ataje gharama/bei kwa huduma takayoitoa.
4. Maombi yatalipiwa ada ya uzabuni ya TZS 50,000/= ambzo hazitarejeshwa ,fedha hizi zilipwe ofisi ya mkurugenzi wa Mji,S.L.P 472 kahama,isipokuwa kwa zabuni ya kupangisha vibanda na meza zitalipwa TZS 10,000/= kwa kila zabuni.
5. Mwombaji wa kukusanya taka ngumu anatakiwa awe na magari/trekta yenye uwezo wa kubeba tani 8 au zaidi.

Wafanyakazi wote wawe waadilifu na wenye umri zaidi ya miaka 18 na wapewe vifaa vya kazi pamoja na nyenzo za kujikinga(viatu vigumu,kofia ngumu,ovaroli,miwani,gloves na mask) vyote vikiwa na nembo ya kampuni husika,awe na ofisi yake inayotambulika katika mji wa Kahama,awe tayari kufanya kazi katika mazingra yenye miundombinu hafifu mno;(barabara mbovu na njia zenye matope),awe na uwezo wakufanya kazi kabla kuanza kukusanya pesa angalau kwa mwezi mmoja,awe tayari kulipa ushuru wa dampo kiwango cha 15% ya makusanyo ya ushuru kila mwezi kwa mkurugenzi wa Mji wa Kahama,awasilishe bank statement ya miezi 6 ya nyuma,

Awasilishe kadi za umiliki wa magari na vifaa vingine alivyo navyo,awe na uwezo wa kuondoa taka mbili kwa wiki toka kila kaya au jengo.

6. Vitabu vya Zabuni vinapatikana kwenye Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Mji Kahama, S.L.P 472, Kahama kuanzia Saa 1.30 Asubuhi hadi Saa 9.30 Alasiri
7. Maombi yote yajazwe kwa umakini na yaambatane na nakala halisi Moja na nakala iliyorudufiwa (Copy) Moja) na yafungwe vizuri kwa lakiri na juu ya bahasha andika jina la zabuni unayoomba. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 13/06/2019 saa 5.00 asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo na waombaji mnakaribishwa kuhudhuria sherehe za ufunguzi.

**Maombi yote yatumwe kwa:**
**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA MJI,**
**S.L.P 472,**

8. Maombi yatakayochelewa au sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi ambayo hayakufunguliwa kwenye sherehe ya ufunguzi wa maombi , kwa hali yoyote ile hayatapokelewa na hayatakubaliwa kwa tathmini.

**Anderson D Msumba**
**KAIMU MKURUGENZI WA MJI**
**KAHAMA**

215252302

# Kampuni za kukusanya mifuko plastiki zatajwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba, amesema zimepatikana kampuni tatu ambazo zitakuwa zinakusanya taka za plastiki na kuzitengenezea mabomba na madawati.

Makamba alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana, wakati akizungumza katika semina ya wahariri na waandishi wa habari.

"Tumepata bahati katika siku mbili hizi zilizobaki, kumejitokeza kampuni tatu kubwa ziko mkoani Mwanza ambazo zitatumia mifuko hii inayokusanywa na kuirejeleza na kuitengenezea mabomba ya maji pamoja na madawati, kwa hiyo mifuko itakuwa ni malighafi kwa bidhaa tunazozihitaji nchini," alisema Makamba.

Aliongeza: "Kwa hiyo tunapenda kutoa wito kwa wale wenye shehena kubwa kabla ya Juni mosi unaweza kuzipeleka moja kwa moja kwenye hivyo viwanda ukafanya nao biashara badala ya kutuletea sisi serikali ambao hatutakulipa. Kwa hiyo hii mifuko inayokusanywa si uchafu tena bali ni malighafi."

Makamba alisisitiza kwamba wameanza kuondoa mifuko ya plastiki ya kubebea na kwamba mifuko mingine ya vifungashio wataendelea kuiondoa hatua kwa hatua.

"Safari ya kuondoa taka za plastiki hapa nchini ni hatua kwa hatua, hakuna nchi ambayo imeamua kuondoa mifuko yote ya plastiki. Kwamba mifuko, chupa, vifungashio na vipakti vya sukari vya chumvi vyote uondoe kwa wakati mmoja utakuwa hauna maarifa, kwa hiyo ushindi wa kwanza kwetu sisi ni wa plastiki na ushindi wa pili utakuwa ni uendelezaji wa chupa za plastiki," alisema Makamba.

Aliongeza: "Kwa hiyo kwa mara ya kwanza tumelazimisha wazalishaji wa bidhaa za mifuko ya plastiki kushiriki katika utaratibu wa urejelezaji wa bidhaa hiyo na baadaye tutaenda katika hatua ya bidhaa nyingine hasa zile ambazo zimesamehewa, huko mbele nazo tutatengeneza utaratibu wa kuwa ziwe zinaoza kwenye mazingira."




Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Runali, mjini Nachingwea. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango na Mwenyekiti wa Runali, Hassan Mpako. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mapitio ya hukumu ya SP Bageni Juni 16

**INATOKA UK. 4**

kutokuzingatiwa, hivyo kuomba mahakama itenguwe hukumu hiyo.

Septemba 16, 2016 mapema saa 3:45 asubuhi, msajili wa mahakama hiyo (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu) John Kahyoza alisoma hukumu hiyo baada ya kusikilizwa kwa rufani iliyokatwa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

DPP alipinga hukumu ya Mahakama Kuu iliyowaachia huru aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Dar es Salaam (RCO) Kamishna Msaidizi wa Polisi Abdallah Zombe na maofisa wenzake watatu akiwamo Bageni mwaka 2009.

Akisoma hukumu hiyo, Kahyoza aliwataja walalamikiwa kuwa ni ACP Zombe, SP Bageni, aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi wa Kituo cha Polisi Urafiki, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Ahmed Makelle na Rajabu Bakari.

Alisema Mahakama ya Rufani ilipitia ushahidi uliotolewa Mahakama Kuu na kuona kwamba ilishindwa kuwatia hatiani washtakiwa wa mauaji na kwa kosa la kusaidia mauaji kufanyika.

"Kosa la kuua na kosa la kusaidia kuua ni makosa mawili tofauti, si sahihi kwa mtu aliyeshtakiwa kwa mauaji kutiwa hatiani kwa kosa lingine ambalo tangu mwanzo mshtakiwa alitakiwa kulijua ili kujitetea," alisema na kuongeza kuwa:

"Washtakiwa wote katika utetezi wao walipinga kuhusika katika mauaji hayo, lakini mlalamikiwa wanne, Rajabu alisema ukweli katika ushahidi wake kwa kueleza tukio la mauaji lilivyofanyika katika Msitu wa Pande, lakini ushahidi wake ulitakiwa kupokewa kwa makini na unatakiwa kuwapo na ushahidi mwingine wa kuunga mkono."

Akifafanua zaidi, Kahozya alisema: "Mlalamikiwa wa kwanza, Zombe, mahakama haikuona kama kuna ushahidi wa kumtia hatiani kwa mauaji wala kwa kusaidia kuua japo kuna jambo kichwani mwake analolifahamu kuhusu mauaji hayo. Ushahidi mwingine unaonyesha wajibu rufani watatu walishuhudia mauaji, lakini hawakuua."

Jopo, kwa mujibu wa Kahozya, lilisema wamekubaliana kwamba watu wanne waliuawa kwa bunduki na mauaji yalikuwa ya kinyama katika Msitu wa Pande.

Mahakama hiyo ilijiuliza maswali kwamba je, wajibu rufani walikuwapo Pande? Jibu ni kwamba walalamikiwa wa pili, wa tatu na wa nne walikuwapo katika msitu huo na kwamba mlalamikiwa wa nne alisema ukweli mahakamani kuhusiana na tukio hilo.

Ilidaiwa kwamba mauaji hayo yalifanywa na askari Polisi Sadi, lakini mshtakiwa huyo hajawahi kushtakiwa. Mahakama inajiuliza waliouawa walipelekwa Pande kwa amri ya nani.

Kwa mujibu wa ushahidi, mahakama inajiuliza nini nia ya kuwapeleka watu hao Pande sehemu ambayo haina hata nyumba, mlalamikiwa wa pili, Bageni ndiye alitoa amri ya kuua, ushahidi unaonyesha washtakiwa waliwapeleka wakiwa hai Pande na waliwarejesha wakiwa marehemu.

"Marehemu walipelekwa huko ili tukio la mauaji lifanyike bila kipingamizi kwa kibali cha Bageni, ushahidi wa mlalamikiwa wa nne uliungwa mkono na tabia ya Bageni kwamba alikuwa akificha ukweli kuhusu mauaji hayo," alisema. Hata hivyo, ushahidi wa maofisa watatu wa Jeshi la Polisi, wote walidanganya kwamba mauaji yalitokea Sinza katika majibizano kati ya Polisi na marehemu wakati wengine wa Sinza walisema hawakusikia tukio la aina hiyo kutokea.

"Mahakama hii imeona walalamikiwa wa kwanza, wa tatu na wa nne, rufani dhidi yao inatupwa hakuna ushahidi wa kuwatia hatiani, mjibu rufani wa pili mahakama inatengua kuachiwa kwake kutiwa hatiani na Mahakama Kuu, inamuhukumu kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya watu wanne," alisema Msajili Kahyoza na kusababisha mahakama hiyo kulipuka kwa vilio.

Katika kesi ya msingi, Wafanyabiashara wa madini kutoka Mahenge, Morogoro waliouawa ni Sabinus Chigumbi, maarufu Jongo na ndugu yake, Ephrahim Chigumbi, Mathias Lunkombe na dereva teksi, mkazi wa Manzese Dar es Salaam, Juma Ndugu.

Walidaiwa kutenda makosa hayo Januari 14, mwaka 2006, katika Msitu wa Pande, uliopo wilayani Kinondoni baada ya kuwakamata wafanyabiashara hao Sinza, walipokuja Dar es Salaam kuuza madini.

## Tanzania kuiuzia Zimbabwe mahindi tani 700,000

**INATOKA UK. 3**

(JKT) na amebainisha kuwa JKT inasaidia vijana kuwa wazalendo wa kweli, kuwa na nidhamu na wakakamavu.

Rais Magufuli pia alielezea kutofurahishwa kwake na kutofanyika kwa Kamati ya Kudumu ya Pamoja tangu mwaka 1998, hali iliyosababisha kukosekana kwa msukumo wa kutosha wa kutekeleza maeneo muhimu ya uhusiano yenye kuimarisha uchumi wa pande zote na hivyo ametaka mawaziri na wataalamu kufanya kikao cha JPC ndani ya mwezi mmoja.

Aidha, Rais Magufuli alisisitiza kuwa Tanzania itaendelea kuwa rafiki wa kweli wa Zimbabwe na ameahidi kuwa tayari kuwaleta walimu watakaofundisha lugha ya Kiswahili katika shule na vyuo vya Zimbabwe.

Halikadhalika, Rais Magufuli ametoa wito kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania na Zimbabwe kuongeza biashara kati ya nchi hizo ikilinganishwa na hali ilivyo hivi sasa ambapo kiwango cha biashara katika nchi hizo ni Sh. bilioni 22.578 tu.

Kwa upande wake, Rais Mnangagwa alimshukuru Rais Magufuli kwa utayari wake wa kutoa mahindi kwa ajili ya kusaidia upungufu wa chakula nchini Zimbabwe na amesisitiza kuwa Wazimbabwe watafurahi kupata chakula kutoka kwa ndugu zao Watanzania.

Kuhusu maeneo mengine ya ushirikiano ambayo mawaziri walijadiliana kabla ya mazungumzo hayo, Rais Mnangagwa alisema Zimbabwe ipo tayari kuyatekeleza na kukamilisha maeneo mapya yatakayokubalika na kutiwa saini makubaliano yake.

Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na Zimbabwe kuitumia Bandari ya Mtwara katika kusafirisha mizigo yake, kushirikiana katika utalii na usafiri wa anga, kubadilishana utaalamu katika kilimo, mifugo na uvuvi. Baada ya mazungumzo hayo viongozi hao wamekutana na waandishi wa habari na kuweleza juu ya yaliyojiri wakati wa mazungumzo.

# Majaliwa awapa maelekezo watumishi ofisi yake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu waongeze kasi ili utendaji kazi serikalini uweze kufikia hatua nzuri.

"Ninawashukuru watumishi wote kwa ushirikiano mnaotupatia mimi pamoja na mawaziri wenzangu, makatibu wakuu wote watatu, wakurugenzi mbalimbali na wakuu wa vitengo. Tunatakiwa tuongeze kasi ili tufikie hatua nzuri ya utendaji kazi serikalini," alisema.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokutana na viongozi na watumishi wa ofisi yake na kufuturu nao pamoja kwenye makazi yake jijini Dodoma. Alisema utendaji kazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu ni mgumu kwa sababu unahusika na usimamizi wa shughuli za serikali nzima na watendaji wote wa serikali. "Sekta yetu ni ngumu kwa sababu sisi ni wasimamizi wa serikali na watendaji wote wa serikali. Tuna wajibu wa kuwaunganisha watendaji wa wizara zote serikalini," alisema.

"Sisi sote ni watumishi wa umma, kwa hiyo mchango wenu una maana kubwa na unachangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya serikali nzima. Ninawapongeza kwa utumishi mwema na wenye uadilifu," alisema Waziri Mkuu.

Mapema, akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na watumishi hao, Waziri wa Nchi (OWM-SBAU), Jenista Mhagama, alisema uamuzi wake wa kuwaalika watumishi na kufuturu nao ni dalili njema kuwa anathamini kazi zinazofanywa na watumishi walio chini yake.

"Ni viongozi wachache sana wanaowakumbuka watumishi walio chini yao. Tunakushukuru kwa kututhamini na tunaahidi kukupa ushirikiano wa dhati unaoenda sambamba na utendaji kazi uliotukuka," alisema.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Waziri Mkuu na Bunge, Maimuna Tarishi alitoa shukrani kwa niaba ya watumishi wote na kuahidi kufanya kazi kwa bidii.



Kamishna wa TIRA, Dk. Banhayo Saqware (kulia), akisalimiana na Mbunge wa Maswa Magharibi, Mashimba Ndaki. Pembeni ni Mkurugenzi wa Bodi ya AAR, Dk. Edmund Mndolwa (katikati) na Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajab Shaban, katika futari iliyoandaliwa na kampuni ya AAR jijini Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

# Uongozi wa soko watumbuliwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAFANYABIASHARA wa Soko Kuu la Manispaa ya Lindi wamewaondoa madarakani viongozi wao kwa kilichoelezwa umeshindwa kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa.

Uamuzi wa kuuondoa uongozi huo uliokuwa chini ya mwenyekiti, Ayubu Abdallah Mmakuwa, umefanywa na wafanyabiashara 91 kati ya 130.

Mkutano wa kuwaondoa viongozi hao na kuwaweka wengine uliongozwa na mwenyekiti wa muda, Kiba Abdallah, huku wafanyabiashara hao ukimrejesha kiongozi mmoja, Juma Rashidi Judifa aliyekuwa katibu.

Wakati uchaguzi huo ukiondolewa madarakani mwenyekiti, Ayubu Abdallah Mmaku ambaye hakuhudhuria.

Wafanyabiashara walimchagua Juma Judifa kuwa mwenyekiti mpya akisaidiwa na Mohamedi Matiko, wakati nafasi ya katibu na mtunza hazina zilichukuliwa na Yusufu Mgomba na Anafi Issa.

Baada ya uchaguzi huo, wafanyabiashara hao waliutaka uongozi mpya utekeleza majukumu yao ikiwamo kuwasomea mapato na matumizi yanayotokana na soko hilo pamoja na kuandaa katiba itakayowaongoza na taratibu zote zikiwamo ukomo wa kuwapo kwao madarakani.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Judifa aliwaahidi ushirikiano.

# TIRA aipongeza AAR kwa huduma bora za bima

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kusimamia Shughuli za Bima Tanzania (TIRA), imeipongeza Kampuni ya Bima ya AAR kutokana na inavyojitolea kusaidia jamii na kutoa huduma bora.

Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alitoa pongezi hizo juzi kwenye Ifutari iliyoandaliwa na AAR jijini Dodoma ambayo ilihudhuriwa na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wa dini, Bodi ya Wakurugenzi wa AAR na wawakilishi wa watoa huduma za bima.

"Kwa dhati, niwapongeze AAR kwani wamekuwa mstari wa mbele kujitolea kufanya shughuli za kijamii kama kusaidia watoto yatima, wazee, walemavu na hata kusaidia kuhuisha ubora wa mazingira yetu. Na leo juhudi zao zimefanikisha uwapo wetu katika kushiriki Iftari itakayohamasisha ari na moyo wa kujitoa zaidi kwa jamii," alisema Dk. Saqware.

Aidha, Dk. Saqware alitoa wito kwa kampuni nyingine na watu binafsi kuiga mfano wa AAR na kujitolea kuhuisha ubora wa maisha ya jamii kadiri wawezavyo ikiwa ni kuakisi kipindi cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alizitaka taasisi zote zinazotoa huduma za bima kuzingatia matakwa ya sheria na kujikita katika kutoa huduma bora, na kushiriki katika kuzuia udanganyifu katika sekta ya bima.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa AAR, Violet Modichai, aliwashukuru wabunge kwa kuhudhuria tukio hilo na kueleza kuwa wameamua kutumia Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuwakutanisha wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi pamoja na wadau wa bima, ili kukumbushana kuhusu umuhimu wa kujitolea kwa jamii pamoja na kutii sheria na maelekezo ya vitabu vitakatifu.

"Tunaahidi kuendelea kutoa msaada zaidi kadiri tuwezavyo. Pia, tunahakikisha tunaendelea kutoa huduma bora zaidi kuojenga taifa lenye afya na lenye uhakika wa kulinda maendeleo ya kila mmoja kupitia bima," alisema Modichai.

Mbunge wa Maswa Magharibi ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Bunge, Mashimba Ndaki, aliishukuru AAR kwa kuandaa tukio hilo.

"Sisi kama wabunge na familia zetu tunafaidika na huduma za bima ya afya. Kwahiyo, niwapongeze watoa huduma kwa kuturahisishia maisha yetu. Badala ya kuhangaika kutafuta fedha wakati nimeugua, wao wananisaidia kwa kuwa nimeshalipa kabla," alisema.

Mbunge huyo ambaye alisema anaridhishwa na huduma ya bima za afya, alitoa ombi lake kwa kampuni za bima kuangalia uwezekano wa kupunguza zaidi gharama za bima za afya ili wananchi wengi zaidi waweze kujiunga.

Aliwaomba AAR kupeleka huduma ya bima ya afya vijijini ili kuwasaidia pia wananchi walioko katika maeneo hayo kufaidika na ubora wa huduma hizo.

"Kuna zahanati kule vijijini, ambazo nyingine tunajenga sisi wenyewe, ningependa pia ninyi kama mashirika ya bima za afya kama mkishiriki pamoja nasi kwenye shughuli hizo ili kutuwezesha sisi wananchi kuanzia ngazi ya chini kabisa kule vijijini tuweze kupata huduma za bima ya afya karibu na bora, ili mwisho wa siku Watanzania wote tuwe na afya bora," alisema.

Mwaka huu, AAR iliyokuwa inatoa huduma ya afya pekee, ilianzisha utoaji wa huduma za jumla (general insurance) kutokana na maombi ya wananchi waliohitaji huduma zao kwenye maeneo mengine pia.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kushoto), akisalimiana na Spika wa Bunge la Vijana 2018/2019, Zephania Sane, wakati uongozi wa Bunge hilo ulipomtembelea ofisini kwake,jijini Dodoma jana. Kushoto ni Naibu Spika wa Bunge hilo, Ashiruna Muhunzi na Katibu wa Bunge, Alphonsina Ambrosi. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Kuku wa kisasa wazua jambo bungeni

BUNGE limeelezwa kuwa hakuna utafiti wa kisayansi ambao unaonyesha kuku wa kisasa (broilers) wana madhara kwa afya za binadamu ikiwamo kusababisha vitambi.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alijibu swali la Mbunge wa Konde(CUF), Khatib Said Haji, kwa niaba ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mbunge huyo alisema watu wanaotaka kupunguza mwili au vitambi wanakatazwa kula baadhi ya aina ya nyama na kushauriwa kula samaki na kuku.

"Lakini katika nyama za kuku, kuna kuku kutoka nje ambao wanauzwa, wana mapaja kama watu hao. Je, hao kuku wa kizungu hawana uhusiano wa moja kwa moja kwenye kuongeza vitambi?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema ulaji wa kuku wa kisasa na ulaji wa kuku kwa ujumla unaongeza protini ambayo huwa inatokana na wanyama na mimea.

Alibainisha kuwa hakuna utafiti wa kisayansi uliothibitisha kuwa kuku hao wana madhara kwa binadamu.

"Ulaji wa kupitiliza ndiyo utakaoweza kusababisha hayo matatizo, lakini broilers hawana shida yoyote, kinachowafanya wakue ni homoni ambazo kisayansi ni vitamins. Kwa hiyo, sisi wana sayansi tunachokifanya, vyakula vya broilers tunaweka vitamins za kutosheleza kuhakikisha ukuaji wao unakua ni wa haraka kulinganisha na kuku wa kienyeji," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma, alihoji serikali inatoa ushauri gani kwa wasio na vitambi wale vyakula gani kwa kuwa pamoja na matumizi ya vyakula vya wanga, bado wapo kwenye maumbile hayo hayo. Akijibu swali hilo, Ulega alimshauri mbunge huyo kuwaona wataalamu wa lishe ili kumpangia vyakula vitakavyoweza kumsaidia kupata kitambi. Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Khadija Nassir Ali, alisema uzito mkubwa mwilini ni dalili za mwanzo za magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kupambana na magonjwa haya? Mbali na mazoezi, ni mbinu gani nyingine za kitaalamu za kupambana na kitambi?" Mbunge huyo alihoji.

Akimjibu mbunge huyo, Ulega alisema serikali inatengeneza mpango mkakati wa mwaka 2016-2020 wa kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Alisema kitambi ni dalili mojawapo ya uzito uliopita kiasi na si dalili njema na husababisha magonjwa hayo.

"Njia bora ya kupambana na kitambi ni kujikinga kutokukipata kwa kuhakikisha unazingatia ulaji wa vyakula unaofaa na ufanyaji wa mazoezi," Ulega alisema.

# Serikali yatangaza mkakati kupanga miji

SERIKALI imeanza utekelezaji wa mkakati wa kupanga miji yote ambayo imetangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa kuandaa mipango kabambe ya majiji, manispaa na miji.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alijibu swali la Mbunge wa Kasulu Mjini, Daniel Nsanzugwanko (CCM).

Mbunge huyo alihoji kwanini serikali isije na mkakati endelevu wa kupanga miji yote ambayo imetangazwa kwenye gazeti hilo.

"Kwanini serikali inatoa hoja nyepesi kwamba kazi ya kupima na kupanga miji ni ya halmashauri wakati inajua kwamba halmashauri nyingi nchini hazina nguvu ya kipesa kufanya kazi hiyo?" Mbunge huyo alihoji.

Akimjibu mbunge huyo, Waziri Lukuvi alisema pamoja na utekelezaji wa mkakati huo, serikali imeainisha upya maeneo yote ambayo yameiva kuendelezwa kimji kwa ajili ya kuyatangaza katika gazeti hilo kuwa maeneo ya mipango.

Alisema kwa mujibu wa vifungu namba 7(1) na (5) vya Sheria ya Mipango Mji Na. 8 ya Mwaka 2007, jukumu la kupanga na kupima miji ni la Mamlaka za Upangaji ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Mamlaka za Miji Midogo.

"Hata hivyo, serikali imeendelea kuzisaidia halmashauri kupanga na kupima miji yao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo," Lukuvi alisema.

Alitolea mfano kuwa katika mwaka huu wa fedha, serikali kupitia wizara yake, imetoa jumla ya Sh. bilioni 6.4 kwa halmashauri 29 kwa ajili ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

Alisema serikali pia inawezesha uandaaji wa mipango kabambe ya miji 18 kupitia Programu ya Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Miji chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Aliongeza kuwa mwaka 2008, serikali iliandaa Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Ardhi wa Mji wa Kasulu wa miaka 10 kuanzia mwaka 2008 hadi 2018 ambao ulikuwa unatumika kuongoza na kusimamia uendelezaji wa mji huo.

"Mpango huo uliisha muda wake mwaka 2018. Hivyo, ni jukumu la Halmashauri ya Mji wa Kasulu kuanza mchakato wa kuandaa mpango kabambe wa

# Taulo za kike bado ghali

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema licha ya serikali kuchukua hatua ya kuondoa kodi ya Ongezeko la Thamani(VAT) kwenye taulo za kike, hakuna mabadiliko ya bei kwa bidhaa hiyo sokoni.

Imesema hali hiyo inatokana na bei ya bidhaa hiyo katika soko kuamuliwa na nguvu ya soko na gharama nyingine za uzalishaji na uendeshaji.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Ashatu Kijaji, alitoa kauli hiyo jana bungeni alijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum(Chadema), Sophia Mwakagenda.

Mbunge huyo alisema katika bajeti ya mwaka 2017/18, serikali iliondoa kodi hiyo, lakini mpaka sasa ni mwaka mmoja bei ya taulo za kike haijashuka.

"Je, ni lini serikali itasimamia kwa ukamilifu suala hili ili bei za taulo za kike zishuke na kusaidia afya za wanawake, hususan wasichana," Mwakagenda alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Kijaji alisema gharama zinazochangia kutoshuka kwa bidhaa hizo ni pamoja na upatikanaji wa malighafi, mishahara, uwekezaji, mifumo ya uzalishaji, teknolojia, ushindani katika soko, umeme, maji na majitaka, usambazaji na ubora wa bidhaa.

"Kutokushuka kwa bei ya taulo za kike kunabainisha kwamba, kodi inachangia kwa sehemu ndogo sana katika kupanga bei ya bidhaa, kama ambavyo serikali imekuwa ikisisitiza na kutoa ufafanuzi mbele ya Bunge," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa, mfumo wa uchumi ni wa soko huria na bei ya bidhaa huamuliwa na nguvu ya soko, yaani ugavi na mahitaji ya soko.

"Fursa pekee iliyopo ni kuhamasisha uwekezaji mkubwa wa kutumia teknolojia yenye gharama nafuu katika kutengeneza taulo za kike, kupunguza gharama nyingine, sambamba na kuchochea ushindani wa bei katika soko na siyo kuondoa kodi na kupanga bei ya bidhaa," alisema.

Katika swali lake la nyongeza, Mwakagenda alihoji mkakati wa serikali kuweka bei elekezi kwenye taulo za kike.

Akimjibu mbunge huyo, Dk. Kijaji alisema hakuna ulazima wowote wa kuweka bei kwenye bidhaa hizo kwa kuwa wako kwenye soko huria na serikali haitaki kuingilia jambo hilo.

"Tunachohitaji ni kuja na mpango wa kibajeti wa kushughulika na jambo hili ili kusaidia watoto wetu wa kike," Dk. Kijaji alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA

# Mawakala forodha walalamikia vipimo

**Na Zanura Mollel ,** LONGIDO

CHAMA cha Mawakala wa Forodha wanaofanya kazi mpakani (Taffa), wa Namanga, mkoani Arusha, wamelalamikia hatua ya Wakala wa Vipimo (WMA) kubadilisha mfumo wa kulipia mizigo inayoingia nchini.

Akizungumzia hatua hiyo jana, mwenyekiti wa chama hicho Ismail Kilas, alisema kuwa mabadiliko ya ulipaji wa mizigo inayoingizwa nchini, yamefanywa ghafla hali itakayosababisha uchumi wa nchi na wafanyabiashara kuwa mgumu. Alisema hapo awali walikuwa wakilipia thamani ya mzigo kwa asilimia 0.2 kama mzigo upo chini ya Sh.100,000.

Pia walikuwa wakilipa kwa thamani ya mzigo ukiingia nchini, lakini kwa sasa WMA imewaletea mabadiliko ya kulipia kwa kila aina ya bidhaa, ikimaanisha kama gari moja limebeba bidhaa 30 wanalazimika kuzilipia zote kwa Sh.100, 000.

Alitaka kufahamishwa iwapo kuna kifungu cha sheria kinachowaongoza wakala huyo wa vipimo kutoza fedha kwa kila mzigo mmoja mmoja uliopo kwenye gari.

Alisisitiza kuwa sheria inasema kila gari ilipie asilimia 0.2 ya thamani ya mzigo uliobebwa.

Hata hivyo, alionya kuwa mabadiliko hayo yanaelekea kukwamisha shughuli za kibiashara katika mpaka wa Namanga, Sirarali na Mtukulu ambako sheria hiyo imeanza kutumika, japo katika mipaka mingine sheria hiyo haitumiki.

Alilalamikia kitendo cha serikali kupitisha sheria hizo bila kuwashirikisha wadau au watumiaji wa sheria ambao inaonekana kuwa ni kandamizi kwao.

Aidha, chama hicho kimeweka msimamo wa pamoja na kudai kuwa hawapo tayari kuendelea kufanya kazi na wakala huyo, huku wakidai fedha za mizigo ambayo haistahili kulipiwa walizolipia kwa muda mrefu walilipishwa kimakosa.

"Kuna mizigo ambayo haistahili kutozwa kodi mfano malighafi za viwanda vya kuzalisha bidhaa nyingine, hapa wapo mawakala wamelipia malighafi hizo, fedha hizo tunazitaka, tunaomba Waziri Mkuu aingilie kati jambo hili," alidai Kais.

Aliongezea kuwa magari yameegeshwa mpakani kwa zaidi ya siku tano kutokana na mabadiliko ya ulipiaji katika kitengo cha vipimo. Chanzo ni kutokana na mvutano uliokuwa ukiendelea baina yao na mawakala wa vipimo.

"Tumepokea barua inayotutaka kulipia kwa kila aina ya bidhaa, lakini sheria haizungumzii hivyo, ndiyo maana tumegoma kuvusha mizigo, japo kuna wasaliti waliovusha, lakini hao ni wale wenye aina moja hadi tatu ya bidhaa, lakini mtu mwenye bidhaa 80 ni vigumu, ukipiga mahesabu ya fedha tunayoilipa inazidi thamani ya manunuzi ya mizigo," alieleza Kais.

Mkurugenzi wa Ufundi Kitengo cha Vipimo WMA, Stella Kahwa, alipohojiwa alisema kuwa ameyapokea malalamiko hayo na anayafanyia kazi ili kubaini ukweli wa jambo hilo.

"Nimepokea malalamiko haya, lakini nimeelekeza itumike sheria ya awali ya malipo kwa mzigo kwa utaratibu uliokuwa unatumiwa," alisema Kahwa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Hudson Kamoga (kulia), akiwa na watumishi wenzake wakionyesha waandishi wa habari juzi, ramani ya jengo jipya la halmashauri hiyo, linalojengwa kwenye Kata ya Dongobesh. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wasaidizi wa sheria waagizwa kujisajili

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WASAIDIZI wa kisheria kutoka mashirika yanayotoa msaada na elimu ya kisheria (Paralegal Organizations), wamehimizwa kujisajili upya kabla ya kuanza kuwahudumia wananchi.

Wanatakiwa kujisajili kama watoa msaada wa kisheria chini ya sheria mpya iliyounda utaratibu huo.

Mratibu wa mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani Manyara (Macsnet), Nemence Iriya, aliyasema hayo jana mjini Babati, wakati akizungumza na wasaidizi wa kisheria wa halmashauri saba za wilaya za mkoa huo. Iriya alisema wasaidizi hao wa kisheria wanatakiwa wajisajili ili wapate cheti cha utambulisho kama taasisi ya watoa msaada wa kisheria chini ya Wizara ya Sheria na Katiba.

Alisema kutokana na hali hiyo wasaidizi hao wa kisheria wanapaswa kujisajili upya, ili vielelezo vyote vinavyowahusu wawe navyo wakati wakiwa wanafanya shughuli zao.

Mwanasheria wa Macsnet, Eliakim Paulo, alisema, kinachoendelea sasa ni kuwajengea uwezo zaidi wasaidizi hao wa kisheria wa mkoa huo.

Aliongeza kuwa kwa sasa wapo tayari kujisajili na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

"Wasaidizi hawa wa kisheria wametoka kwenye halmashauri zote saba za mkoa huu ikiwamo Babati Mji, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Mbulu Mji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Simanjiro, Hanang' na Kiteto," alisema Paulo.

Mmoja kati ya wasaidizi hao wa kisheria Pauline Longu kutoka Wilaya ya Hanang' alisema watahakikisha wanafanya usajili wao upya kama sheria mpya inavyowataka ili waweze kufanya kazi zao ipasavyo.

"Watu wengi wamejua na kupata haki zao kupitia Macsnet baada ya kutuwezesha wasaidizi wa kisheria, hivyo tunawashukuru sana na hatuna budi kujisajili ili jamii izidi kufaidika kupitia sisi," alisema Longu.

Msaidizi wa kisheria kutoka wilayani Simanjiro, John Sarakikiya, alieleza kuimarika zaidi baada ya mafunzo hayo ya Macsnet.

"Jamii hasa vijijini inatutegemea mno kwa kuwa wengi wao hawana uelewa juu ya masuala mbalimbali ya kisheria, ila kupitia sisi ambao tunaitwa 'bush lawyers' tunawasaidia mno," alisema Sarakikiya.

# DC akerwa maofisa maendeleo 'mangi meza'

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewataka maofisa maendeleo ya jamii, kuacha kujifungia ofisini badala yake watoke na kuwafuata wananchi ili kuwasaidia kupata maendeleo.

Aidha, aliwataka kuwafunza kuhusu kutumia rasilimali za kilimo na mifugo ili kujiletea maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye warsha iliyoandaliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na kuwashirikisha wadau kutoka vikundi vidogo na taasisi za fedha pamoja na maofisa wa maendeleo ya jamii kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Alisema maofisa hao wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha jamii inapata elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa rasilimali zao, na kuweza kujikwamua kiuchumi.

Murro alisema kuwa, kumekuwapo na changamoto kubwa wanazokabiliana nazo wananchi hususani katika masuala mbalimbali ya kukopa kutokana na wengi wao kutokuwa na elimu ya kutosha, hivyo ni wajibu wao kutoka maofisini na kwenda kupeleka elimu hiyo kwa wananchi.

"Nawaombeni sana mtoke maofisini sasa mkatembelee wananchi na kutoa elimu mbalimbali ili iwanufaishe na kuwawezesha kutumia rasilimali zilizopo, sambamba na kuwapa elimu juu ya matumizi sahihi ya mikopo, ili waweze kuitumia ipasavyo," alisema Murro.

Kwa upande wa Makamu Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dk. George Bakari, alisema lengo la warsha hiyo ni kuwakutanisha wadau wa maendeleo katika kuimarisha usimamizi bora wa vikundi vya vikoba kuanzia ngazi ya wilaya hadi mkoa.

Dk. Bakari alisema umefika wakati sasa wa maofisa hao kubadili mwenendo wa ufanyaji kazi wao, ili kuweza kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Aidha, aliwataka kuzunguka ndani ya jamii na kusikiliza kero zao na kutoa ufumbuzi wa changamoto hizo kwa wakati ili kuwezesha kupata maendeleo kwa haraka.



Mkuu wa Mkoa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emanuel Maganga, akizungumza katika hafla ya futari iliyoandaliwa na benki ya TPB, kwa ajili ya wateja wake na waumini wa dini ya kiislam, mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Marufuku kufunga nyama kwa magazeti

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amepiga marufuku wauza nyama mkoani humo kufunga kitoweo hicho kwenye magazeti.

Aidha, amewaonya kuwa magazeti yana athari kwa afya za walaji.

Agizo hilo ni kufuatia maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, alilolitoa Aprili 29, mwaka huu, kukataza mifuko ya plastiki kutumiwa nchini kutokana na madhara kwa binadamu na mazingira.

Alisema kuwa amepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa wauza nyama wanatumia magazeti kufungia nyama hali ambayo inaharatisha afya zao.

"Wananchi wamekuwa wakilalamika kuwa wanafungiwa nyama kwenye magazeti ambayo yana sumu, kwani wino unaotumiwa kuchapisha taarifa hizo haufai kuliwa." Aliongeza kuwa kama mkoa wameagiza wauza nyama waache mara moja na watumie mifuko au vifungashio rafiki wa mazingira.

Mkuu wa Mkoa, Dk. Mghwira, alisema watu wenye mzigo au bidhaa nyingi za mifuko yote ya plastiki iwasilishwe kwenye halmashauri na kuwekewa kumbukumbu ili kusubiri maelekezo ya wataalamu hasa kuitumia kwa matumizi mengine. "Wale wote wenye mifuko ya plastiki kwa kiwango kikubwa waiwasilishe kwenye halmashauri ili iweze kutumika kwa matumizi mengine kuepuka uchafuzi wa mazingira tutafuata maelekezo na ushauri wa wataalamu wetu."

Mbali na hilo alisema kuwa mifuko ya plastiki iliyotupwa katika majalala iwe imeokotwa yote na kuhifadhiwa sehemu maalumu na hairuhusiwi mwananchi kuendelea kuitupa mifuko hiyo na atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aliwataka Shirika la Viwango nchini (TBS) kutoa ufafanuzi sahihi kwa wananchi juu ya mifuko mbadala ambayo inakidhi vigezo na isiyo na madhara kwa wananchi na rafiki wa mazingira.

Alisema: "Kuna aina nyingi za mifuko mbadala ambayo imeleta mkanganyiko kwa wananchi. Alitaka ufafanuzi sahihi utolewe kwani mingine inaonekana kuwa ni mizuri lakini si rafiki wa mazingira," alisema.

Samwel Gideon, akitoa maoni yake aliiambia Nipashe kuwa, kufuatia agizo la Waziri Mkuu ni wakati wa watendaji hasa Idara ya Mazingira kuendelea kutoa elimu ya kina juu ya matumizi sahihi ya mifuko mbadala.

Aisha Mohamed mfanyabiashara wa soko la Mbuyuni, katika Manispaa ya Moshi alisema, ipo haja ya watendaji kufanya kazi kwa bidii kwani wapo wafanyabiashara ambao si waaminifu.

Alisema kuna uwezekano wa baadhi yao kuleta mifuko isiyo rafiki wa mazingira kutoka nchi jirani ili kudai fidia.

Akiwa katika Mkoa wa Kilimanjaro Waziri wa Biashara na Viwanda, Joseph Kakunda, alivitaka viwanda vikubwa na vidogo kuhakikisha vinaongeza uzalishaji wa mifuko mbadala kwani upo uhitaji mkubwa kwa sasa.

"Zipo tetesi kuwa baadhi ya wafanyabiashara ambao sio waaminifu wanatumia fursa hii kuingiza mifuko inayofanana na hii, lakini ndani yake kunachembechembe za plastiki hatutawavumilia na hatua kali za kisheria zitachukulia," alisema Waziri Kakunda.

## Wilaya Hai waongezewa muda kutibu watoto

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SERIKALI imeongeza mwezi mmoja wa kutekeleza kampeni ya kitaifa ya kutoa dawa za vitamini A na za minyoo tumbo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro.

Taarifa iliyothibitishwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, Valerian Juwal ilionyesha kuwa kampeni hiyo itaanza tena Juni Mosi hadi 31 mwaka huu.

"Ni kweli tumepokea maelekezo hayo, tutaanza tena kutoa vitamini 'A' na unyweshaji dawa za minyoo tumbo katika wilaya yetu," alisema.

Taarifa zaidi zilieleza kuwa kampeni hiyo inafanyika kwa lengo la kudhibiti magonjwa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, dawa hizo hutolewa kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi 59 katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyopo Wilaya ya Siha.

Hospitali ya Wilaya ya Siha peke yake kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Andrew Method, inahudumia wakazi wapatao 116,313 (kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012) kutoka vijiji 60 vilivyopo kwenye kata 17.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 2007 ikiwa kituo cha afya, baada ya vyama viwili vya ushirika wilayani humo kutoa ekari 40 za ardhi.

Lakini kwa sasa hospitali hiyo inahudumia kwa wananchi 1,500 hadi 2000.

# Waziri Kakunda sasa kuwasaka waigaji wa nembo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, amekitaka kiwanda cha kuunganisha magari cha Rajinder kuwasilisha malalamiko ya baadhi ya watu kuiga teknolojia yao kwa maandishi kwa Tume ya Ushindani nchini (FCC).

Alisema waigaji hao wanaodaiwa kughushi na kutumia nembo ya Rajender, taarifa zao zikifikishwa kwa maandishi watashughulikiwa kwa wakati.

Aliyasema hayo jana wakati alipotembelea kiwanda hicho na kuwataka waandike barua rasmi ili serikali iweze kushughulikia malalamiko hayo na hatua kali za kisheria zichukuliwe.

"Naiagiza tume ya usimamizi kuhakikisha inafika katika kiwanda cha Rajender na kushughulikia malalamiko hayo, ili kutokomeza na kudhibiti watu wasio waaminifu wanaotumia nembo ya Rajinder," alisema na kuongeza kuwa

"Hatutamvumilia mtu yeyote atakayemsababishia mwekezaji hasara ya kufunga kiwanda chake kwa ajili ya watu ambao si waaminifu wanaonakili na kukopi nembo ya mtu anayelipa staiki zote za serikali..."alisema.

Aliahidi kuwa serikali itamchukulia hatua kali za kisheria ili kutokomeza tabia hiyo.

Aidha, Waziri Kakunda alikitaka kiwanda hicho kusimamia usalama wa watu kazini ili kuepuka mamlaka zilizopo kuwapa adhabu.

"Pamoja na utendaji wenu mzuri unaofanyika naomba mzingatie zoezi la usalama kazini kwa wafanyakazi na utunzaji wa mazingira ikiwa ni hatua mojawapo ya ufanisi," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Manmohan Bhamva, alisema kinakabiliwa na changamoto kubwa ya watu kuigiza anachofanya huku akiiomba serikali kuangalia namna ya kutokomeza changamoto hiyo ili aweze kupanua kiwanda chake katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa sasa ametoa ajira kwa vijana waliomaliza mafunzo katika Vyuo vya Ufundi (Veta) zaidi ya 200, lakini ana uwezo wa kuajiri zaidi.

Alisema mafanikio yataonekana iwapo changamoto zake zitafanyiwa kazi kwa wakati.

"Leo ni kwa mara ya kwanza amekuja kiongozi mkuu katika kiwanda chetu. Sisi tunaona kama ni mafanikio makubwa na hii ni kutokana na ushirikiano mkubwa tunaoupata katika serikali kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa. Tutaendeleza kuzalisha kwa wingi na kulipa stahiki zote za serikali.

Kijana mkata vyuma, Samson Erick, akizungumzia mafanikio alisema mbali na kupata ajira amepata mafunzo maalumu ya namna ya kukata vyuma kwa kutumia kompyuta.

ama
ALHAMISI MEI 30, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 17

**Wanaosomea digrii wabu ni nyenzo kwa mgonjwa moyo bila daktari**



Ukurasa 14

Majeruhi wa mbwa kila kona




Ukurasa 14

**Msongo mawazo kwa madereva barabarani uko juu kuua abiria**



## 'DEBE' RUKSA YA BANGI

# Daktari aonya: Tusithubutu, madhara yanatisha hayalingani na tumbaku

Ukurasa 16

# Majeruhi wa mbwa kila kona

**London, Uingereza**

MADAKTARI wa Kiingereza wana hofu kubwa kutokana na kuwapo mlolongo wa matukio, watu kuumwa vibaya na mbwa wao, ikiwaacha wamechanika vibaya.

Anasema, kuna maelfu ya watu wako hatarini kwani ni wafugaji mbwa na hali hiyo isipoangaliwa haitaishia pazuri. Chama cha Tiba ya Mikono cha Uingereza, kinasema hivi sasa kuna taarifa za majeruhi 30, ambao wameumizwa vibaya na mbwa.

Majeruhi, Jillian Tisdale (65), anasimulia alivyoraruliwa na mbwa wake muda mfupi aliporejea nyumbani, akitoka kutembea na mbwa mwingine.

Jillian anayefananisha shambulizi hilo na mtu kukatwa na kisu kikali, anasema aliishia kauli maumivu makali kupindukia. Hivi sasa yuko katika hatua ya kupona akifanyia mazoezi kidole chake.

Daktari bingwa, Rebecca Dunlop, aliyemtibu Jillian anakiri ongezeko la matukio ya watu kujeruhiwa na mbwa na kushauri: "Ninawataka wote wanaowapenda mbwa wao kuwa makini na wachikue hatua za kawaida kuepuka athari kutoka kwa mbwa wao."



Kidole kilichojeruhiwa. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Msongo mawazo kwa madereva barabarani uko juu kuua abiria

• Malipo, kutokupumzika majanga • Hiace 'mchinjaji' wa kila mahali



Ajali ya lori, mkoani Mbeya.

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KILA ifikapo Mei 6 hadi 12 ya kila mwaka, Tanzania huungana na nchi zingine duniani kuadhimisha Wiki ya Kimataifa ya Usalama Barabarani.

Takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), vifo vitokanavyo na ajali za barabarani vinafikia milioni 1.35, huku kundi linaloonekana kuathirika ni kuanzia umri wa miaka mitano hadi 29.

Takwimu hizo zinaonyesha, vifo vinavyotokana na ajali za barabarani kwa upande wa watembea kwa miguu na waendesha baiskeli, vimefikia asilimia 26 na kwa waendesha pikipiki pamoja na abiria, vimefikia asilimia 28 ya ajali zote.

Hatari ya vifo vitonakavyo na ajali za barabarani, imeendelea kuwa juu zaidi katika nchi zenye kipato cha chini.

> Kutokuwapo kwa alama za barabarani katika eneo la ajali kama unatokea Lindi (ukomo wa mwendokasi na kuwapo kwa kona kali).

Takwimu zinaonyesha kuwa barani Afrika kuna ongezeko kubwa la ajali kwa asilimia 26.6, huku bara la Ulaya, likiwa chini kwa asilimia 9.3, kutoka wastani wa kundi la watu 100,000 katika jamii husika inayorejewa.

Nini sababu? Zipo nyingi za kitaalamu zinazotolewa, kwamba zinasababishwa na matukio au mazingira ya kuwapo mwendokasi, kutovaa kofia ngumu kwa waendesha pikipiki, ulevi, kutofunga mikanda na vizuizi vya watoto.

### WATAFITI WASEMA

Uchunguzi uliofanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), kabla ya kuwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), madereva wengi walipata ajali mwaka jana kutokana na matatizo yanayowazunguka, ikiwamo msongo wa mawazo.

Akitoa mada ya uchunguzi wa ajali za barabarani mjini hapa, katika mafunzo ya usalama barabarani yaliyoandaliwa na WHO jijini hapa, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Meneja, Usalama Barabarani na Mazingira kutoka LATRA, Geoffrey Silanda, anaainisha mengi.

Mosi, anataja ni baadhi ya ajali zilizofanyiwa uchunguzi zimeonyesha kuwapo tatizo la msongo wa mawazo, matatizo ya kifamilia na kipato duni kwa madereva.

Pia, anasema ajali zingine zinachangiwa na uchovu kwa madereva, kutokana na kuendesha magari bila ya kupumzika, ubovu wa magari na kuzidishiwa uwezo wa mizigo, pia hali mbaya ya miundombinu.

Kuna mikasa ya mifano inayohusiana na kutokea ajali barabarani katika maeneo tofauti ambayo ni marejeo hai ya mjadala huo wa kitaaluma, kuhusu ajali zinazoishia katika ama kupotea au uhai kuathiri uhai wa wengi katika namna tofauti.

### SIMULIZI ZA MIFANO

Katika mafunzo hayo kuna mifano kadhaa iliyorejewa kuoanisha hoja zilizotolewa. Ilielezwa ajali iliyotokea mkoani Morogoro, mnamo Machi 4, mwaka 2018, ilihusisha basi kubwa lililokuwa linaelekea Tunduma ambalo liligongana na basi dogo aina ya Toyota Hiace.

Wataalamu wanasema ilikuwa ajali inayoepukika, iwapo dereva wa basi aina Hiace, asingekuwa na kinachoelezwa kuwa msongo wa mawazo.

Silanda anasema, ni ajali iliyosababisha vifo vya watu watano na majeruhi tisa. Uchunguzi wa kamati illiyoundwa ulibaini chanzo ni uzembe wa dereva wa basi dogo aina ya Toyota Hiace, aliyejaribu kulipita lori lililokuwa mbele yake.

"Katika mchakato wa kulipita lori hilo, aligongana na basi lililokuwa likija mbele yake, likitokea Morogoro kuelekea Tunduma," anaeleza mwasilishaji huyo na kuongeza:

"Kamati ilibaini dereva wa basi hakufanya jitihada zozote za kulizuia basi lake kuepusha ajali, baada ya kuona hatari kubwa iliyokuwa mbele yake baada ya maamuzi ya dereva wa Toyota Hiace kuhama kutoka kwenye njia yake kwenda upande wa magari yanayoelekea Tunduma."

Silanda anadokeza kuwa wakati wa uchunguzi, kamati ilibaini dereva wa Toyota Hiace (marehemu) alikuwa na ugomvi na mke wake uliosababisha wawili hao kutengana.

Anaendeleza kwa kufafanua: "Hali hii ilitokana na ugomvi mkubwa baina ya mama wa marehemu na mke wa marehemu. Mama (mzazi) alilazwa hospitalini baada ya kupigwa na mke wa marehemu (dereva).

"Hali hii ilimfanya dereva kuwa katika katika msongo wa mawazo kwa muda wa siku tatu mfululizo. Ilikuwa siku ya Jumapili (siku ya ajali) alipoamua kwenda kuendesha gari, ili apate fedha za kumpa

AFYA

# Msongo mawazo kwa madereva barabarani uko juu kuua abiria

mmiliki wa gari na siku ya Jumapili huwa na wasafiri wengi wanaotoka na kuelekea katika Kijiji cha Mlali."

Anabainisha, katika kipindi chote alichokuwa akiendesha gari, dereva alikuwa katika msongo wa mawazo, hali iliyothibitishwa na kondakta na mama wa marehemu aliyehojiwa na kamati, pamoja na ndugu wa karibu.

**AJALI MKURANGA**

Aidha, Silanada anataja ajali nyingine (namba tunazo) ilitokea Machi 24 mwaka jana, iliyohusisha lori lenye tela iliyokuwa imepakia chumvi kutoka Kilwa likielekea Mwanza. Hiyo iligongana na basi dogo aina ya Toyota Hiace lililokuwa likitoka Mbagala Rangi Tatu, kuelekea Kimanzichana, Dar es Salaam.

Hiyo nayo ni ajali inayosimuliwa kusababisha vifo vya watu 26 na majeruhi wanane, chanzo anakieleza mtaalamu huyo wa usalama barabarani, kuwa ni dereva wa lori kushindwa kulimudu gari lake lililokuwa katika gia kubwa na mwendokasi kwenye kona kali mlimani.

"Kutokuwapo kwa alama za barabarani katika eneo la ajali kama unatokea Lindi (ukomo wa mwendokasi na kuwapo kwa kona kali)," anatoa kasoro, huku akiongeza lingine: "Excel' ya nyuma ya tela upande wa kulia, mfumo wake wa breki ulikuwa mbovu na haufanyi kazi kabisa."

Pia, Silanda anataja kasoro upande wa pili, basi dogo la Toyota Hiace, ilijaza abiria kuzidi uwezo wake unaostahili.

**AJALI IGUNGA**

Silanda anataja huo ni mkasa wa Aprili 4, mwaka jana, majira ya saa mbili usiku, lori (namba za usajili zinahifadhiwa) lililopakia viazi mviringo kutoka Njombe likielekea Mwanza, liligongana na basi aina ya Scania (City boy) lililokuwa linatoka Karagwe kuelekea Dar es Salaam.

Anasema, ni ajali iliyosababisha vifo vya watu 13 na majeruhi wanane. Chanzo chake kinatajwa kuwa ni lori iliyohama kutoka upande wake, kuelekea ambako basi lilikuwa linakuja, sababu ni kukwepa shimo la barabarani.

"Ajali ilitokea katika eneo la Makomero, katika Wilaya ya Igunga umbali wa kilomita 20 kutoka mji wa Igunga, kuelekea Singida. Na hapa, kamati ilibaini kuwa alama za barabarani zilikuwapo na zilikuwa zinaonekana vizuri, ingawa alama hizo hazikuwa kwenye kiwango kinachotakiwa," anasema.

Ni ajali iliyotokea wakati wa usiku na mvua zilikuwa zikinyesha, hivyo katika ufafanuzi huo, anatumia fursa ya uzoefu wa kuwapo mikasa ya aina hiyo, akiwataka madereva wote kuchukua tahad-




Ajali iliyohusisha basi la abiria, malori mawili ya mizigo na gari dogo aina ya Toyota Pick-up, asubuhi eneo la Igurusi, Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Desemba 2016.

> "Kamati imebaini kuwa, basi lilikuwa na madereva wawili wakati wa kuanza safari. Hata hivyo, dereva wa pili anayejulikana... hakuweza kuonekana baada ya ajali.



Ajali mojawapo iliyotokea saa tano usiku wa Januari mwaka jana eneo la Mubigera, Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera, gari aina ya Nissan Caravan, lilipogongana na malori mawili. Watu 11 walifariki papo hapo na watano kujeruhiwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

hari barabarani, wanapokutana na mazingira ya namna hiyo.

"Kamati imebaini kuwa, basi lilikuwa na madereva wawili wakati wa kuanza safari. Hata hivyo, dereva wa pili anayejulikana... hakuweza kuonekana baada ya ajali," anasema.

Meneja huyo anasema, dereva wa basi hakupunguza mwendo pamoja na kwamba ilikuwa usiku na mvua ilikuwa ikinyesha.

Alikuwa amewasha taa kubwa na kuna uwezekano alisababisha dereva wa lori kwa sababu ya kutoona vizuri.

**AJALI SINGIDA**

Silanda anaeleza mkasa mwingine uliofanyiwa uchunguzi, ni kwamba mnamo Novemba 23 mwaka juzi, majira ya saa mbili usiku, basi dogo aina ya Toyota Hiace lililotokea kijiji cha Mpipiti Singida Vijijini, kuelekea kijiji cha Mkiwa, lilipofika katika maeneo ya Ighuka liligongana na gari ndogo aina ya Toyata Noah, lililokuwa likitoka Manyoni kuelekea Mkalama.

Anasema, ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu 14 na majeruhi 20.

Kutokana na vyanzo vya ajali vilivyoainishwa na kamati iliyofanya uchunguzi, imependekeza kuimarishwa mafunzo kwa madereva na kutatua changamoto zinazohusiana na alama za barabarani.

Pia, maeneo mengine yanayotajwa, ni kudhibiti mwendokasi wa magari, kuwapo usimamizi sahihi unaokabili tatizo la uchovu wa madereva, kusimamia matengenezo sahihi ya magari na kuzuia upakiaji abiria au mizigo kuzidi uwezo wa gari husika.

AFYA


'DEBE' RUKSA YA BANGI

# Daktari aonya: Tusithubutu, madhara yanatisha hayalingani na tumbaku

• Wabunge watatu Kanda Ziwa wasimama kuitetea

Na Sabato Kasika

***"Bangi huharibu mapafu, kwani ina zaidi ya asilimia 50 hadi 70 ya kemikali aina ya 'carcinogenic hydrocarbons' kuliko mvutaji wa tumbaku na inachangia kuongeza mapigo ya moyo kutoka asilimia 20 hadi 100, muda mfupi tu wa saa tatu baada ya kuvuta."***




Uuzaji bangi katika nchi kunakoruhusiwa kisheria. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Mkurugenzi Mkuu wa Asasi ya Health Promotion Tanzania, Dk. Peter Bujari.



Mvuta bangi. Picha ndogo, mmea wa bangi.

KILIMO cha bangi kinazidi kupigiwa debe katika nchi mbalimbali duniani. Sasa nchini nacho kinaingia katika ulingo huo, tena kwa nguvu kubwa ya mamlaka mazito ya kisiasa yenye 'mkono' wa maamuzi.

'Wapiga debe' hao ushauri wao ni kwamba, serikali ihalalishe kilimo hicho kwa manaa ya kupata malighafi yanayozalisha dawa.

Wakati baadhi ya watu wakitaka ihalalishwe, kuna wataalamu wa afya hawako kinyume na hoja hiyo, wakitumia utetezi kwamba mmea wa bangi (cannabis plant), ni miongoni mwa dawa za kulevya, hatari kwa afya ya binadamu.

Ni hoja inayoambatana na uainisho wa aina za mimea ya bangi, orodha yake kufikia 400, katika mnyambuo unaotofautisha kila mmea na mwingine na madhara yake kiafya yanatofautiana.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Health Promotion Tanzania, Dk. Peter Bujari, anaendeleza uchambuzi wake huo wa awali kwamba kuna madhara ya muda mfupi na muda mrefu, anayoainisha:

"Madhara ya kutumia bangi yapo mengi kama vile kupoteza kumbukumbu, kujiamini kupita kiasi, magonjwa ya moyo, magonjwa ya mapafu na kupoteza hamu ya kula."

Anataja mengine ni kupungua uwezo kufanya maamuzi, kusisimka mwili au kupatwa na msongo wa mawazo, kichaa cha kudumu na kwa muda mfupi, ingawa kinaweza kuwa cha muda mrefu kwa watumiaji wa muda mrefu.

"Ingawa bangi inaonekana kuwa na viasili vya matibabu, viasili hivyo hutofautiana kutoka aina moja ya mmea kwenda nyingine.

"Hata hivyo, madhara yanaonekana kuwa makubwa kuliko faida yake. Ndio maana zao hilo linakatazwa nchi nyingi duniani," anasema Dk. Bujari.

Anafafanua upana wa magonjwa ya afya ya akili yanayoendelea kutesa watu, kwamba baadhi ya vyanzo vyake ni ulevi wa kupindukia, matumizi ya dawa za kulevya, ikiwamo bangi.

"Bangi huharibu mapafu, kwani ina zaidi ya asilimia 50 hadi 70 ya kemikali aina ya 'carcinogenic hydrocarbons' kuliko mvutaji wa tumbaku na inachangia kuongeza mapigo ya moyo kutoka asilimia 20 hadi 100, muda mfupi tu wa saa tatu baada ya kuvuta," anasema.

> **"Ingawa bangi inaonekana kuwa na viasili vya matibabu, viasili hivyo hutofautiana kutoka aina moja ya mmea kwenda nyingine.**



Operesheni kufyeka mmea wa bangi ikiendelea.

Anasema mvutaji bangi hupumua kwa tabu kuliko anayevuta tumbaku, ingawa wote wanaharibu mapafu, pamoja na kuwa na uwezekano mkubwa wa kukaribisha ugonjwa wa kansa.

Tanzania haijaruhusu kilimo cha zao hilo, ingawa katika baadhi ya mikoa kuna watu wanaendelea kuilima kinyemela na wahusika wamekuwa wakichukuliwa hatua kisheria.

Baadhi ya mikoa inayotajwa na serikali kuwa juu katika kilimo cha zao hilo haramu kisheria, ni Mara, Arusha, Njombe, Tanga, Simiyu, Rukwa, Geita na Morogoro kwa mujibu wa orodha iliyowahi kutolewa katika uwasilisho wa kiserikali bungeni.

Pia, kuna wakati polisi mkoani iliwahi kuchukua hatua ya kuvamia, ikikamata na kufyeka mashamba ya bangi katika baadhi ya maeneo, ikiwa milimani katika mkoa wa Kilimanjaro.

**WABUNGE WAONGEA**

Ni siku chache zilizopita, Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku (Msukuma), alishawahi kuibuka na hoja bungeni ya kuishauri serikali kuruhusu kisheria kilimo cha bangi na mirungi, ili kuiwezesha kujipatia fedha za kigeni kutokana na mauzo yake nje ya nchi.

Huo ulikuwa mwaka 2016, aliporejea mfano wa ruksa hiyo kutoka nchi jirani ya Kenya, ambao ndege mbili kubwa hutua nchini humo kuchukua mirungi na kupeleka sokoni katika nchi za Bara Ulaya.

Alichohimiza ni kwamba, zao hilo linalopatikana katika maeneo anayoyataja kuwa Geita na Bunda mkoani Mara yanaweza kuwanufaisha wananchi wengi.

Pia, mwaka juzi hoja hiyo ikachukua nafasi kwa mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, aliishauri serikali kufanya utafiti kuhusu bangi na tumbaku, iwapo kuna athari kubwa na akapendekeza iwe zao la biashara.

Alirejea kikao kingine, aliiomba serikali kutafiti au kuleta ushahidi kati ya bangi na tumbaku kupata usahihi wa kina kuhusu madhara linganishi kwa mazao hayo mawili.

Esther ana maoni kwamba, iwapo zao hilo litaruhusiwa na kuwekewa mipango ya namna ya kuilima na usafirishaji wake, ina nafasi ya kuliingizia taifa kipato, kuliko baadhi ya mazao yanayopewa kipaumbele.

Huku akieleza kwamba hapingani na serikali kuhusu mapambano yake dhidi ya dawa za kulevya nchini, anadai kuwapo mpango madhubuti wa kuliangalia zao la bangi.

Wiki hii nako ndani ya dimba hilo bungeni jijini Dodoma, Jumanne Kishimba, Mbunge wa Kahama, katika mjadala wa mawasilisho ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha, naye akahuisha hoja ya watanguliza wake, akitaka kuruhusiwa kilimo cha bangi.

Mtazamo wa Kishimba ni kwamba, zao hilo liruhusiwe kwa lengo la utengenezaji dawa za binadamu, akirejea kitaalamu kwamba asilimia 80 ya dawa za maumivu ya saratani zinatokana na mmea wa bangi.

Pia, Kishimba anatetea hoja yake kitaalamu, akiitaja nchi ya Uganda kwamba imesharuhusu ulimaji bangi, kwa ajili ya kutengenezea dawa za binadamu.

Kishimba, akiweka mustakabali wa hoja yake katika mustakabali wa kibiashara, eneo la ununuzi, anasema gunia moja la bangi nchini linanunuliwa kwa bei ya kati ya shilingi milioni nne mpaka milioni 4.5, wakati Lesotho na Zimbabwe, gunia hilo bei zake ni shilingi milioni 20.

> **"Hata hivyo, madhara yanaonekana kuwa makubwa kuliko faida yake. Ndio maana zao hilo linakatazwa nchi nyingi duniani.**

Hata hivyo, Kishimba, anaweka bayana kuwa anapinga vikali wote wanaotetea bangi ihalalishwe kwa ajili ya kuvuta.

**SERIKALI ILIKOSIMAMIA**

Katika ufafanuzi kwa Mbunge wa Geita Vijijini, aliyeishauri serikali kuruhusu bangi, aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakati huo, Dk. Khamis Kigwangala, alisimama kutoa msimamo wa serikali.

Dk. Kigwangala, ambaye kitaaluma ni daktari wa binadamu na kwa sasa ni Waziri wa Maliasili na Utalii, alieleza kuwa bangi na mirungi vina athari kubwa kiafya na hasa katika afya ya ubongo, hivyo serikali haitakubali kuruhusu dawa hizo.

Hadi sasa kuna nchi nne za Afrika zinazotajwa kuhalilisha kilimo cha zao hilo ambazo ni Lesotho, Zimbabwe, Afrika Kusini na Uganda.

## Aspirini tiba kiharusi cha damu kichwani

WAGONJWA wanaopatwa na kiharusi kutokana na tatizo la mshipa kupasuka kichwani na kuvuja damu, tiba imepatikana. Hiyo ni kupitia matumizi ya dawa aina ya aspirini, inayozuia uwezekano wa kuugua tena maradhi hayo au shinikizo la moyo.

Mabingwa waliotafiti, wanasema matumizi ya aspirini ni msaada mkubwa wa kuzuia uwezekano wa watu kupatwa tena na matatizo hayo kwa mara nyingine, lakini kigezo kikuu ni ushauri wa daktari kuwa jambo muhimu wakati wote.

Ni kazi mpya ya dawa hiyo, mbali na iliyozoeleka kuondoa maumivu na homa mwilini.

Sehemu kubwa ya kiharusi inachangiwa na damu kuganda katika mshipa, hivyo aspirini inasaidia kulainisha damu hiyo na inaondoa uwezekano wa kiharusi au shinikizo la damu na kiharusi.

Hata hivyo, pamoja na kushauriwa matumizi ya aspirini, kiafya imepigwa marufuku kwa yeyote mwenye umri chini ya miaka 16 kushirki matumizi hayo, isipokuwa kama mgonjwa atashauriwa na daktari.

Chama cha Kiharusi cha Uingereza kinasena, katika utafiti waliofanyiwa na kuhusisha watu 537 nchini Uingereza, ilibainika kwamba nusu ya waliojaribiwa kutumia dawa hiyo, walionyesha mafanikio.

Katika hilo, watafiti wanasema ina sifa kukabili shinikizo itokanayo na matatizo ya ubongo na



Kasha la dawa za aspirini na vidonge vyake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

wakati huo huo, ni salama kwa watumiaji.

Mtafiti kiongozi, Profesa Rutsam Salman, kutoka Chuo Kikuu cha Edinburgh, Uingereza anasema licha ya wengi kuhofu matumizi hayo, wataalamu hao watafiti, bado wanakiri kukubali uthabiti huo wanaouthibitisha.

Mtaalamu wa moyo, Profesa, Metin Avkiran, kutoka Mfuko wa Moyo wa Uingereza, ambao ndiyo wadhamini utafiti, ana maelezo kuhusu nafasi ya aspirini katika eneo lake la ujuzi wa tiba.

"Theluthi moja ya watu waliopata tatizo la kutokwa damu ambayo pia inajulikana kama kiharusi cha damu kichwani, walifanya hivyo kwa kutumia dawa ya kuzuia




kama vile aspirin, ili kupunguza hatari ya shinikizo la moyo.

"Sasa tuna ushahidi mkubwa kwamba hizi ni dawa zinazonusuru afya, baada ya ubongo kutoa damu, ikisaidia kuokoa pia hatari zingine, ambayo ni habari njema kwa wagonjwa na madaktari."

Hata hivyo, kuwapo taarifa hiyo, bado inasisitizwa mtu yeyote asichukue hatua ya kutumia dawa, pasipo ushauri wa daktari. **BBC.**

AFYA

# Wanaosomea digrii wabuni nyenzo kwa mgonjwa moyo bila daktari

• Roboti inayotekeleza kazi ya bingwa • Michakato tiba imepatiwa 'short cut'



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mt. Joseph, wakielezea mradi wao wa kutatua changamoto ya uhaba wa madaktari bingwa wa moyo nchini. Wa kwanza kushoto ni mhadhiri, Dk. Dk. Lawrence Kerefu. **PICHA: MARY GEOFREY.**

**Na Mary Geofrey**

WAKATI serikali inawekeza kupata madaktari bingwa wa kutibu magonjwa ya moyo nchini, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, Kitengo cha Uhandisi wa Umeme na Mawasiliano, jijini Dar es Salaam, kimebuni teknolojia mpya ya kukabiliana na uhaba huo wa matabibu bingwa.

Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), inasema tangu kuanza kutoa huduma ya matibabu ya moyo mwaka 2015, imeshaona wagonjwa zaidi ya 200,000, huku idadi ya madaktari bingwa walioko hawazidi 50.

Wanafunzi wa Chuo cha Mt. Joseph, Kitengo cha Uhandisi Umeme na Mawasiliano, kimeanzisha teknolojia hiyo ya matibabu, ikilenga kukabiliana na changamoto ya uhaba wa bingwa hao.

Mukrim Omary, ni kati ya wanafunzi wanne waliobuni teknolojia tajwa, anayetaja sababu ya kufikia uamuzi huo, kwanza walipobaini kuwapo changamoto hiyo. Anaifafanua katika lugha ya tahadhari kwamba iwapo haitatafutiwa ufumbuzi, itaongeza idadi ya vifo nchini vitokanavyo na magonjwa ya moyo.

Omary anasema ameona vyema kutafuta mbadala wa kutoa huduma ya matibabu, ili kuharakisha maamuzi ya kibunifu, mbadala ya kutegemea pekee kwa madaktari wanaotumia miaka minane kusomea ubingwa wa kutibu magonjwa hayo.

Kwa mujibu wa mtaala wa mafunzo hayo, inawachukua miaka mitano darasani na mmoja wa mafunzo kwa vitendo kutihimu shahada ya kwanza, kisha miaka miwili ya shahada nyingine ya ubobezi katika eneo tajwa; moyo.

> **Tulijiuliza kama madaktari bingwa waliopo nchini wapo 20 na wagonjwa wanaougua magonjwa hayo ni zaidi ya 60,000 kwa mwaka, ina maana ni tatizo ambalo linahitaji ufumbuzi wa haraka.**



Profesa Mohammed Janabi; Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. **PICHA: MAKTABA**

Anataja sababu nyingine waliyoiona ni kuwapo ongezeko la wagonjwa wanaotokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, yanayosababisha kuibuka magonjwa mengi ya moyo.

"Tulijiuliza kama madaktari bingwa waliopo nchini wapo 20 na wagonjwa wanaougua magonjwa hayo ni zaidi ya 60,000 kwa mwaka, ina maana ni tatizo ambalo linahitaji ufumbuzi wa haraka. Tukaamua kubuni teknolojia ya kutibu ugonjwa huo kwa njia ya roboti," anasema Omar.

Anasema kwamba, waliona vyema kutengeneza mfumo usio wa kibinadamu, kwa ajili ya kuchukua vipimo vya wagonjwa, kuupima ugonjwa na kutoa tiba kwa wanaoumwa moyo.

Omary anaeleza kuwa, kuna roboti waliowatengeneza wenye hisia au kitaalamu 'sensor' zitakazoupima moyo, kiwango cha damu na msukumo wa damu, mapigo ya moyo na joto la mwili.

Anasema, vipimo hivyo vinawezesha kubaini kama moyo una tatizo na kueleza tiba za ugonjwa ulipo katika moyo, hivyo kuanza matibabu haraka.

Mwanafunzi huyo anasema, pia wametengeneza mfumo wa moyo kwenye kompyuta, ambao utachukua taarifa zote za mgonjwa, kama vile jina, umri na taarifa nyingine muhimu kwa matibabu.

Omary anasema, urahisi wa mfumo huo ni kutoa huduma katika maeneo ambako wananchi hawafikiwi na huduma, mfano hao ni vijijini.

Anataja faida zake ni kuokoa muda, gharama za kusafiri umbali mrefu kufuata huduma, kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini, foleni za wagonjwa wanaosubiri huduma kwa muda mrefu.

**UTAKAVYOFANYA KAZI**

Mwanaidi Lulanga, anasema roboti huyo atafungwa katika ofisi za wilaya na mikoa, wakati mfumo huo utakuwa katika kila halmashauri katika hospitali zote za serikali.

Anasema, wakati mgonjwa huyo anapimwa na sensa hiyo inayowekwa mwilini na kuchukua dakika saba kutoa majibu, itaunganishwa moja kwa moja na roboti iliyopo ofisi ya wilaya au mkoa kutoa majibu ya mgonjwa huyo na maelezo ya tiba yake.

Mwanaidi anasema, mtoa huduma za afya atachukua taarifa za mgonjwa na vifaa hivyo, kisha kuvifunga katika mwili wa mgonjwa na wakati vinafungwa, mfumo utakuwa unachukua taarifa za mwili.

"Mfumo huu unachukua taarifa ndani ya dakika saba na kutoa majibu kulingana na ugonjwa uliogundulika na kueleza nini tiba halisi," anasema Mwanaidi.

Pia, anasema kifaa hicho kinaweza kumilikiwa na mtu yeyote aliye na upeo wa kielimu na uzoefu wa kupata huduma hiyo.

Anafafanua kwamba, namna ya kuunganisha mfumo huo ni kutumia simu ya mkononi aina ya 'smartphone.' Anasema gharama ya mfumo mzima, kuutengeneza hadi akatoa huduma ni Dola za Marekani 5,000 sawa na Sh. milioni 11.5.

Mwanaidi anasema, makisio ya gharama ya kumtibu mgonjwa, yanaweza kupungua kulingana na kifaa kitakapofungwa kwenye vituo vya afya vya serikali inaweza kuwa bure, kama itamiliki mifumo yake.

Anasema watu binafsi wanaweza kuchangia gharama kidogo, kulingana na matakwa ya mtoa huduma, lakini haziwezi kulingana na zile ambazo mgonjwa angetumia kufuata huduma hiyo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.

**MTAALUMA AFAFANUA**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha St. Joseph, Dk. Lawrence Kerefu, ameiambia Nipashe kuwa wa-

INAENDELEA UK.20

AFYA

KINAMAMA HATARINI

# Wakazi Magu wanavyotoa mimba kuchanganya vidonge, mitishamba

• Wahusika waganga magwiji watunzao siri • TFDA yahemea kitendawili cha dawa yake • Watoaji, matabibu asili wafunguka siri

**Na Mwandishi Wetu,** MAGU

HALI na matendo hayavutiii kuanzia afya na haki za binadamu. Inatajwa vifo vingi vya wanawake vinavyohusiana na uzazi nchini vinatajwa kufikia 556 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mujibu wa Takwimu za Utafiti wa Makazi na Afya (DHS) ya mwaka 2015/16.

Sababu inayotajwa ni ukosefu wa huduma, utokaji damu uliokithiri kujifungua nyumbani na utoaji mimba usio salama.

Japo utoaji mimba usio salama hauzungumzwi sana hadharani nchini kwa sababu sheria inatamka ni jinai, lakini ukweli ni mkondo wa kuchangia vifo vya wazazi kwa kiwango kikubwa.

Huwa ni tendo la siri, kulinda njia hatari zinazotumiwa, zikijumuisha dawa na vifaa vinavyoongeza hatari, badala ya usalama kwa wahusika.

Utafiti uliofanywa na mwandishi wa makala hii wilayani Magu, mkoa wa Mwanza mwezi uliopita, ulibaini wanawake wengi vijijini wanapata mimba wasizozitarajia.

Kutokana na sababu kama kipato kidogo walicho nacho, pia kukwepa mkono wa sheria kwa wasichana wanaokimbilia kwa waganga wa kienyeji.

Inadaiwa, waganga hao wanatumia dawa za kienyeji zinazochanganywa na vidonge vinavyotumiwa kufungua njia ya uzazi kutoa mimba.

Baadhi ya wanawake (majina tunayo) wanaeleza kuwa dawa hizo huchanganywa na chai, uji, supu au kwa njia nyingine atakazopanga mganga na kupewa mjamzito, ili aharibu mimba.

Wakazi wa Magu wanadai, kuna waganga wanaotumia dawa za asili kama majani yenye uchungu mfano mwarobaini, alovera na dawa za kung'arisha nguo nyeupe.



Mkunga wa jadi akiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

### MGANGA WA JADI

Mganga wa jadi, Makeremo Makeremo, katika ufafanuzi wake, anakiri kuwapo matendo hayo yanayochangia vifo vya wanawake.

Makeremo, mkazi wa Kitongoji cha Nyalukungu A mjini Magu, anasema utoaji mimba huo hufanywa na anaowaita 'waganga wasio waadilifu' na wakati hufikia mikasa ya vifo.

"Wengi hawafahamu vipimo wanakadiria na kubahatisha, matokeo yake ni vifo. Wanafanya hivyo kwa sababu ya pesa. Kumbuka, kuna watu wanapewa pesa ili kumuua mtu na wanafanya hivyo.

"Vivyo hivyo na mganga naye hawezi kukataa fedha hata kama hajui dawa, anachanganya kujaribu bahati yake apate chochote," anasema Makeremo.

Anawataja baadhi ya waganga wanaodaiwa kuhusika na utoaji mimba, baadhi wakiwa ni wakaaji

> **Wewe ukikataa wenzako wanakubali. Ninawafahamu 'wakunga feki' wanaofanya hayo mitaani.**

vijiweni (eneo la tiba) wanakowakusanya wanawake, mabinti na watoto wanaowatunza kwa muda mrefu.

### MKUNGA JADI

Leonida Anatoli, ni mkunga wa jadi aliyehudumia wajawazito kwa miaka 40 sasa mjini Magu. Anaeleza kuwa wakunga nao wanahusika kuwashawishi wanawake kutoa mimba kwa kuwapa dawa za asili au hata kuzichanganya na za hospitali.

Anasema, kuna mgawanyiko kila jamii ina dawa zake, huku akitaja dawa kuu za mjini Magu ni pamoja na zinazowekwa katika sehemu za siri, kunywa juisi ya mwarobaini, alovera na majivu.

Mkunga huyo mwenye umri wa miaka 74, anasisitiza kwamba hajawahi kumtoa mtu mimba, lakini wengi humfuata kumuomba katika anachokiita 'kuavia' (kuharibu) mimba.

"Wewe ukikataa wenzako wanakubali. Ninawafahamu 'wakunga feki' wanaofanya hayo mitaani," anasema huku akiwataja wahusika.

Anaendelea: "Wakiona wanapoteza damu nyingi au wameanza kupata matatizo makubwa wanakimbilia kwa waganga au wakunga. Mganga naye anajaribu bahati yake kwa kumpa dawa, wengine hufa."

Anasema, hayo hutokea zaidi vijijini ambako sehemu nyingi hakuna huduma nyingi za ama zahanati au vituo vya afya jirani, hasa kwa wanaoishi mashambani.

Mkunga anasimulia ushuhuda wa kuletewa mwanafamilia pasipo kutarajia:"Mwanamama alinijia na mimba ya miezi minne, akataka niitoe. Nilikataa nikamwambia zaa mtoto. Akakubali na akirudi kujifungulia hapa akanitupia mtoto. Nimemtunza na sasa ni mtu mzima."

### WASEMAVYO WENYEWE

Diwani wa Kata ya Magu Mjini, Mashaka Thomas, anasema pamoja na waganga wa jadi kusaidia kuharibu mimba, kuna anaowaita 'magwiji wa kienyeji' wa kutoa mimba kwa njia zisizo salama, ambao wanawake na mabinti wanawafahamu na huwapendelea, kwa vile ni wafi cha siri.

Mashaka anasema, kuna baadhi ya watoa mimba kwa kutumia tiba ya asili wanafahamika vijijini, lakini hawachukuliwi hatua kwa sababu jamii hazijahamasika kuhusu athari zake.Mhusika Zaina Magesa (si jina halisi), aliyetolewa mimba kwa njia zisizo salama, anatoa uzoefu wake akisema alichukua hatua hiyo mimba ilipokuwa na miezi mitatu na sababu ya kukimbilia waganga ni hoja ya kujifichiwa siri.

"Kwa mganga kuna siri, si rahisi kufahamika, labda kama mwanamke atapata matatizo hasa ikitoka, imefahamika kwa vyombo vya dola. Sheria inakataza utoaji mimba, watu wanafanya kwa siri wakiogopa kufikishwa mahakamani," anaeleza.

Huku akitamka asingependa kukumbushwa mkasa huo wa mimba, anataja kulichomsukuma kufanya hivyo ni umaskini.

Pia, kuna sababu anayoifanya kwa kauli: "Aliyenipa ujauzito nilipomwambia kuwa nina mimba alinitusi sana. Akanifukuza na kukata mawasiliano."

Mwanamke huyo ambaye hivi sasa anauza chakula kwa wajasiriamali sokoni mjini Magu, anasema wastani wa faida yake kwa siku ni Sh. 2,000 akiwa anategemewa na familia yake.

Anasema alitoa ujauzito mtaani kwa gharama ndogo baada ya waganga wataalamu wa hospitali kumdai Sh. 100,000. Hata hivyo hakufafanua utaalamu uliotumika.

"Unaweza kwenda kwa waganga wa mitaani wakiwamo wa tiba asili kwa Sh. 20,000, lakini ni hatari maana hawana ujuzi," anasema mama huyo anayedai, alifanya utafiti kabla ya kufikia maamuzi.

Roman Kiwango, ni mhudumu wa wagonjwa wa nyumbani wa kata ya Magu Mjini, anayehudumia wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), wenye kisukari na saratani, anaungana na watangulizi katika kutaja sababu ni kutafuta usiri.

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Wanaosomea digrii wabuni nyenzo kwa mgonjwa moyo bila daktari

INATOKA UK.18

nafunzi wa Kitengo cha Ubunifu na Ujasiriamali Teknolojia, walioamua kuibua wazo hilo wanalolifanyia kazi ni sehemu ya mradi wao na kujiajiri.

Anasema, chuo kilianzisha kitengo cha kuwawezesha wanafunzi kujiandaa, kwa ajili ya kujiajiri na kuendelea kukuza uchumi wa Taifa, ili wanaohitimu masomo wajiajiri na kuwaajiri vijana wengine.

"Tuliona mbali na chuo kutoa elimu bora inayomfanya mhitimu kuwa mfanyakazi bora katika idara zote. Ni vyema, pia kuangalia namna ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa kuwawezesha wanafunzi kujijengea msingi wa kuajiri wanapohitimu masomo," anasema Dk. Kerefu.

Anasema, badala ya mwanafunzi kutoka chuo asubiri kupata ajira, anapaswa atoke akiwa na mtazamo wa kujiajiri na kufungua kampuni yake.

Dk. Kerefu anasema, wanafunzi wanapaswa kuangalia jamii, matatizo yanayowagusa jamii, ili iwe fursa ya kibiashara kwa kuyatatua matatizo yao, badala ya kuwa sehemu ya matatizo, ilhali wamepata elimu.

Mhadhiri huyo anasema, wanawapa mafunzo ya ubunifu na ujasiriamali, hali inayowapatia ufahamu wa kuanzisha kampuni zao wenyewe.

Anasema, kupitia mradi walioanzisha, wanategemea kupitia vituo vya afya na hospitali zote nchini, madaktari na watoa huduma za afya watakaopewa mafunzo ya kutumia teknolojia hiyo, inayoenda kukabiliana na uhaba wa watoa huduma za afya.



Wanafunzi wakionyesha ubunifu wao. **PICHA: MARY GEOFREY.**

**UTEKELEZAJI WAKE**

Dk. Kerefu, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Ubunifu na Ujasiriamali Teknolojia, anasema moja ya jukumu la chuo kilichomwajiri ni kuwasimamia wanafunzi hao kuhakikisha wanatimiza lengo hilo, wanapohitimu masomo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

> "Tunawaambia kabisa kujiajiri ni kuendeleza ndoto zao, lakini kwenda kuajiriwa ni kuendeleza ndoto za watu wengine.

Katika hilo, anasema watahakikisha wanawawezesha kwa fedha za kujikimu, ili waendelee kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Anafafanua hatua hizo ni kuwafuatilia kwa hatua, kuhakikisha wanasajili kampuni yao, biashara na kupata wafadhili, kabla ya kuwaruhusu kuendelea kusimamia mradi huo.

Anasema, pia wanaingia nao mkataba wa kuendelea kufanya kazi katika kipindi hicho cha miezi sita hadi mwaka watakaokuwa nje ya chuo, wakiendelea na shughuli za mradi huo.

Mkurugenzi anaahidi endapo watakamilisha mradi huo, watakomba kampuni tarajiwa ikilipe chuo asilimia moja ya faida wanayopata, ili kuwezesha miradi mingine kwa wanafunzi wa baadaye.

Dk. Kerefu, anazidi kueleza: "Tunawaambia kabisa kujiajiri ni kuendeleza ndoto zao, lakini kwenda kuajiriwa ni kuendeleza ndoto za watu wengine. Hivyo, wanapaswa kujitahidi kuendeleza ndoto zao, ndio maana tumeamua pia kuwasimamia wakati ambao watakuwa wamemaliza chuo."

Mtaaluma huyo anasema, katika mradi huo wameshaishirikisha Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), ambayo wameahidi kushirikiana nayo.

Aidha, anasema katika ukuzaji vipaji vya wanafunzi wanaosoma chuoni hapo na kusukuma ajenda ya kufikiaTanzania ya Uchumi wa Kati wa Viwanda ifikapo 2025, chuo kimejikita kuelimisha nadharia kwa wanafunzi wake, ili kuwapa ujuzi wa kutosha.

**KULIVYO NCHINI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Profesa Mohammed Janabi, anasema kwa siku wanawaona wagonjwa 300 hadi 400 na madaktari wanaowahudumia wanaohitajika ni 50, ingawa katika uhalisia wako chini ya 20.

Pia, anasema, kuna viashiria vya ongezeko la idadi ya wagonjwa wa moyo kila mwaka, takwimu zikionyesha idadi ya wagonjwa kuongezeka kila mwaka.

Kwa mujibu wa takwimu za asasi hiyo, mwaka 2015 walipoanza rasmi kutoa huduma, waliwaona wagonjwa wa nje 23,000; mwaka 2016, wagonjwa 53,000; mwaka 2017, wagonjwa 60,000; na mwaka jana wagonjwa 76,00.

"Ukijumlisha hii miaka mitatu tumeshahudumia wagonjwa wa nje zaidi ya 200,000, tumelaza wagonjwa zaidi ya 11,000, tumefanya upasuaji wa kufungua kifua kwa kusimamisha moyo wagonjwa 800," anasema.

"Tumeshawafanyia upasuaji kwa tundu dogo wagonjwa 2,056. Kiujumla tumehudumia wagonjwa zaidi ya 250,000." anasema Prof. Janabi katika taarifa zake na vyombo vya habari.

**WHO**

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema kuwa jumla ya watu milioni 18 kila mwaka wanaopoteza maisha, kutokana na ugonjwa wa moyo sawa na asilimia 31 ya wagonjwa wote.

Pia, WHO inasema, asilimia 75 ya vifo vinavyotokana na magonjwa ya moyo, vinatokea barani Afrika. Kwingineko ambako hali si nzuri ni Latin Amerika na barani Asia.

## Wakazi Magu wanavyotoa mimba kuchanganya vidonge, mitishamba

INATOKA UK.19

"Wanawake hufuata dawa za kuzuia mimba kwa waganga wa jadi na inapotokea wanapata ujauzito huwarudia ili wawasaidie kuzitoa," anasema Kiwango.

Anataja wenye VVU hawazitaki mimba na kunasababisha utoaji mimba kwa njia zisizo salama na baadhi hata kupoteza maisha wanapokuwa kwa waganga wa kienyeji, wakikwepa hospitalini simulizi za ushauri ambazo hawazikubali.

**VIFO VYA UZAZI**

Mkoa wa Mwanza unatajwa kuwa wa pili, ukitanguliwa na Dar es Salaam kwa vifo hivyo, kwa mujibu wa takwimu za vifo vya wazazi zilizokusanywa kutoka katika hospitali za Tanzania na Waratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Tanzania Bara, mwaka 2018.

Dk. Anna Temba, mbobezi wa tiba ya afya ya uzazi, ana maelezo kuhusu utafiti uliofanywa na Chama cha Madaktari Bingwa wa Wanawake na Afya ya Uzazi Tanzania (AGOTA) pamoja na Shirika la Amref Health Africa, mwaka 2016.

Anasema, kila mwaka nchini kuna wastani wa mimba 405,000 zinazoharibiwa, hivyo anashauri elimu zaidi itolewe katika maamuzi sahihi yanayohusu tendo la ndoa, kubeba ujauzito na kupata huduma bora za uzazi.

Meneja wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Gaudensia Simwanza, anasema tatizo la kutumia dawa za hospitali anayoitaja 'mesoprostal' kutoa mimba kienyeji, linafahamika na kuna wakati TFDA ilishauriwa na serikali kuidhibiti dawa hiyo.

Anasema, ni dawa iliyosajiliwa na inatumika kufungua njia ya uzazi na kuwasaidia kinamama kujifungua, pia kupunguza damu nyingi kutoka baada ya kujifungua.

Gaudensia anaeleza, baada ya kutafiti ikabainika ni dawa muhimu kwenye vituo vya afya, hivyo kuidhibiti kunaweza kuwa na athari kubwa kwa kinamama wanaostahili kuokoa.

**NINI KIFANYIKE?**

Ofisa wa HBC Kata ya Magu, Roman Kiwango, anaeleza tatizo la kuharibu mimba, hata kuchangia vifo vya wazazi litapunguzwa, iwapo serikali na wadau wote kuanzia jamii, waganga na wakunga wa jadi, wataalamu wa afya watalizungumza suala hilo hadharani.

Ushauri wake ni kwamba, umma usiendelee kukaa kimya katika utoaji elimu ya kuwasaidia wanawake wanaotaka kutoa mimba, bali iwekwe miongozo jinsi ya kuwahudumia na kuwafikisha hospitalini na utoaji wa taarifa kwa waganga wakuu wa vituo vya afya, hata wilaya ili kuwaokoa kinamama wanaopoteza maisha.

Mganga wa jadi, Makeremo Makeremo, anashauri waganga wanaokusanya wagonjwa wengi hasa wanawake na mabinti wakaguliwe na kufuatiliwa kila mara, ili wadhibitiwe.

Mkunga wa jadi, Leonida Antony, anashauri utoaji mimba usio salama utamkwe ni 'Janga la Taifa' na kuzungumziwa kwa kuwakuhusisha viongozi mbalimbali kama vile wabunge, wanaosimamia dini na mawaziri.

Anahitimisha kwa kufafanisha namna kampeni inavyopaswa, ifanane na vita dhidi ya maradhi ya Ukimwi, majukwaa ya kitaifa yakitumika kwa kazi hiyo, ili ujumbe wa udhibiti umfikie kila mmoja.





# Mil. 480/- kufanikisha Nanenane 2019 Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHILINGI milioni 480 zinatarajiwa kukusanywa na halmashauri zote za mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwa ajili ya maandalizi ya Maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima, maarufu kama Nanenane, ambayo kikanda yatafanyika jijini Mbeya.

Akizungumza juzi kwenye Kikao cha Tathmini ya Maonyesho ya Nanenane mwaka huu, kilichofanyika katika Ukumbi wa JKT jijini Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alizitaka halmashauri zote za mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutoa michango yao ili kufanikisha maonyesho hayo ambayo yanatarajiwa kuanza Agosti Mosi, mwaka huu.

Aidha, alizitaka halmashauri zote zinazodaiwa kulipa malimbikizo ya madeni yote ya nyuma kabla ya maonyesho ya mwaka huu kuanza.

"Maonyesho haya ya wakulima yamekuwa na tija kwa kuwa wametangaza na kuuza mazao yao na kubwa zaidi wanajifunza elimu ya kuongeza thamani mazao wanayozalisha na kujiongezea kipato. Ili tuendelee kunufaika na maonyesho hayo lazima tuweke mazingira rafiki kupitia michango ya halmashauri," alisema Chalamila.

Aliwataka wakulima wote wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kujitokeza kwa wingi kwenye maonyesho hayo ili kukutanishwa na wadau wa masoko kwa ajili ya kuuza mazao na bidhaa zao.

Mwenyekiti wa kikao hicho ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka, alizitaka halmashauri zote kuandaa bidhaa bora ambazo zitaingia kwenye soko la ushindani.

Alisema anatamani maonyesho ya mwaka huu yawe tofauti na miaka iliyopita kwa kuhakikisha kila mshiriki anaandaa bidhaa bora na zenye ubunifu.

# Jafo ataka vijana kupatiwa ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, amewataka wakuu wa wilaya nchini kutenga ardhi ambayo itatumiwa na vijana kwa ajili ya ujasiriamali ikiwamo kilimo.

Jafo alisema hayo jana jijini hapa wakati wa kukabidhi Sh. bilioni 1.7 kwa taasisi tisa ambazo zinasaidia utengenezaji wa ujira, ujasiriamali, uongozi na maisha bora kwa vijana kupitia Mradi wa Inua Vijana, wa 'Feed The Future' unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (Usaid).

Mradi huo ambao unawanufaisha vijana mbalimbali kutoka mikoa ya Mbeya kwa wilaya za Rungwe na Kyela, Iringa na Zanzibar, una lengo la kuhakikisha wanajiajiri na kutengeneza fursa mbalimbali za kiuchumi kupitia kilimo kwa kuongea thamani ya mazao.

Jafo alisema ili vijana watimize malengo yao kupitia fursa wanazopata, serikali haina budi kuwaunga mkono kwa kutenga ardhi ambayo wataitumia kwa ajili ya kilimo na ujasiriamali.

Alisema mashirika ambayo yanawasaidia vijana, yanajikita zaidi kuwapatia maarifa na ujuzi wa namna ya kutengeneza bidhaa na kuwatafutia masoko pamoja na elimu ya kilimo chenye tija na kwamba jukumu la serikali ni kuunga mkono kwa kuwatengea maeneo ya uwekezaji.

"Wakuu wote wa wilaya hasa ambao vijana wao wamenufaika na mradi huu wa 'Feed The Future', nawaomba mkaangalie maeneo ambayo hayatumiki muwape vijana ili wayatumie kwa ajili ya kilimo, lakini pia kuwekeza kupitia viwanda vidogo vidogo walivyovianzisha," alisema.

Waziri Jafo aliupongeza mradi wa 'Feed The Future' kwa kuwafundisha vijana stadi mbalimbali za maisha zikiwamo ujasiriamali, uongozi na kwamba jamii haina budi kuunga mkono jitihada hizo kwa kupenda kununua bidhaa wanazozalisha vijana hao.

Mkurugenzi Mkazi wa Usaid, Andrew Karas, katika hotuba yake, aliipongeza serikali ya Tanzania kwa juhudi zake za kuwainua wananchi kiuchumi hususani vijana kwa kutoa fursa mbalimbali.

Alisema mradi huo unahamasisha vijana kuanzia umri wa miaka 15 hadi 35 hususani wa vijijini kushiriki katika kilimo.

Alisema hadi sasa vijana 7,000 tayari wamenufaika na mradi wa Inua Vijana kwa kupewa elimu ya ujasiriamali, stadi za maisha na uongozi na kwamba imewawezesha kufungua viwanda vidogo, lakini pia kulima kilimo bora.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mradi huo umeleta tija kwa vijana hasa wanaotoka kwenye familia maskini na ambao walihitimu vyuo vikuu na kukosa ajira.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, aliiomba Usaid kuzisaidia halmashauri za wilaya wanazofanya nazo kazi kuwaachia vitendea kazi yakiwamo magari na vifaa vingine pindi wanapokamilisha miradi yao ili vitumike kuendeleza na kufuatilia shughuli walizozianzisha.



Mwendesha guta akiwa amesheheni mzigo wa vipande vya magodoro, katika eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana na kumfanya ashindwe kuona nyuma, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ubakaji, ulawiti, mimba utotoni vyapungua Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi kupitia Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, limesema vitendo vya ubakaji na ulawiti vimepungua kutoka 108 hadi 91, huku mimba za utotoni pia zikipungua kutoka 59 hadi 30 katika kipindi cha mwaka 2018/19.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, Janeth Masangano, alisema hayo jana wakati wa mahojiano na Nipashe kuhusu vitendo hivyo mkoani hapa.

Alisema matukio hayo yamepungua kwa sababu ya elimu ya masuala ya jinsia inayotolewa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau.

Masangano alisema miaka ya nyuma vitendo vya ubakaji na ulawiti vilikuwa vinafanyika sana kwa sababu ya kutokuwa na elimu, lakini pia jamii haikutambua faida ya kuripoti matukio hayo pindi yanapotokea.

"Tunawapongeza wananchi na Jeshi la Polisi kwa jitihada wanazofanya kukabiliana na vitendo vya ukatili na ulawiti pamoja na mimba kwa watoto wetu. Jamii sasa imeelimika na inakemea na kuwachukulia hatua wanaohusika," alisema.


Katika Mkoa wa Mbeya, alisema wilaya inayoongoza kwa matukio ya ubakaji na ulawiti ni Chunya huku Rungwe ikiongoza kwa mimba za utotoni kwa kila wiki zaidi ya kesi tano zikiripotiwa.

Alisema sababu zinazochangia Chunya kuripotiwa matukio ya ubakaji na ulawiti ni imani za kishirikina kwa wachimbaji wa dhahabu ambao baadhi huamini ni njia ya kujipatia madini mengi au utajiri.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, alisema changamoto ya elimu kwa jamii ni miongoni mwa sababu zinazochochea vitendo hivyo na kwamba Jeshi la Polisi limeweka mikakati ya kutoa elimu ili kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi isiyokuwa ya Kiserikali ya Sauti ya Mama Afrika (Samofa), Thabitha Bughali, alisema changamoto ya kuwapo kwa matukio hayo ni wazazi kuwa chanzo kikubwa kwa kushindwa kulea na kuwatunza watoto kimaadili.

Alisema tamaa ya kipato ni changamoto kubwa, hivyo kuiomba serikali kutunga sheria kali ya kuwabana wazazi ambao wanashindwa kuwasimamia watoto na kutangulia maslahi ya fedha mbele.





# Unesco yavipa kazi vyombo vya habari

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VYOMBO vya habari vimetakiwa kuendelea kuandaa na kuandika habari za kuelimisha jamii, ili kuondoa dhana ya unyanyasaji wa kijinsia.

Hayo yalielezwa jana na Mwakilishi wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), Tirso Dos Santos, wakati alipokuwa akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tano kwa waandaji wa vipindi vya redio nchini.

Santos alisema vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuendelea kuelimisha jamii kupitia redio au magazeti ili kuondoa unyanyasaji wa kijinsia.

"Kila siku jamii inapata habari kupitia vyombo vyenu, hivyo mkiandaa vipindi vyenye kuelimisha jamii itasaidia kuondoa unyanyasaji wa kijinsi kwa makundi mengi," alisema.

Alisema wanaweza kuandaa vipindi vyenye kuelimisha kuhusu afya ya jamii, Ukimwi, na uzazi salama kwa makundi ya kinamama na vijana.

Alisema mimba za utotoni zimekuwa changamoto kutokana na vijana kuanzia umri wa mika 14 mpaka 19 kujiingiza kwenye mahusiano yaliyosababisha mimba hizo.

# Pinda: Elimu yetu inahitajika kufanyiwa marekebisho

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema umefika wakati mfumo wa elimu nchini ukafanyiwa marekebisho na kuingiza masomo ya elimu ya ujasiriamali katika mitaala ya masomo ya vyuo vikuu, ili kupunguza malalamiko ya ukosefu wa ajira kwa wahitimu.

Pinda aliyasema hayo jijini hapa wakati akizungumza na vijana wa Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) tawi la Ndaki ya Elimu, Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) wanaomaliza mwaka wa tatu wa masomo.

Alisema elimu inayotolewa nchini hivi imekuwa na changamoto nyingi ambazo zinatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuwasaidia vijana kuwa na uwezo wa kujiajiri.

"Nadhani kuna sehemu hatukufikiri vizuri, wakati tunajenga hizi taasisi zetu za elimu ilitakiwa tuone kwanza hawa vijana tunaowaanda lazima tujue wakitoka hapa watakwenda kufanya nini na wapi," alisema Pinda. Aidha, alisema kuwa kama serikali itaweza kuingiza masuala ya ujasiriamali katika mitaala ya elimu ya vyuo vikuu na vile vingine wahitimu watakuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe. "Leo hii mtu anayesoma sheria au udaktari akimaliza masomo yake hapa Udom kisha akaenda huko mtaani akakosa kazi hiyo aliyoisomea anasema yeye hana kazi na kuanza kulalamika kumbe upo uwezekano wa kutazama fursa zilizopo na kuanzisha kitu kikubwa na kuajiri wengine," alisema.

Alisema katika kuelekeza uchumi wa viwanda wizara ya elimu sasa inatakiwa kujipanga ili kuona kama inaweza kuweka masuala ya ujasiriamali katika mitaala yake ili kuwajengea uwezo vijana wa kuthubutu kufanya vitu kwa kutumia fursa zilizopo.

"Mimi ni Waziri Mkuu mstaafu, lakini ukija kwangu pale ninazao heka 70 ambazo heka 20 nimepanda miti ya miembe ya kisasa, heka 10 nimelima zabibu za mvinyo pamoja na zile za mezani, lakini pia nafuga nyuki pamoja na mabwawa saba ya samaki, nilifurahi sana niliposikia kuwa serikali inahamia hapa nikajua fursa ya soko ipo sasa," alisema.

Kwa upande wao wahadhiri wa chuo hicho, Dk. Ombeni Msuya na Dk. Abdallah Seni walisema wanaunga mkono kauli ya Pinda, kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia vijana wengi kuondokana na malalamiko ya kukosa ajira.

Hata hivyo, walisema vijana wanatakiwa kubadili fikra zao na siyo kuendelea kuangalia zaidi katika kile walichokisomea bali wafanye mambo kulingana na fursa zilizopo.

"Mimi huwa nawaambia wanafunzi wangu kuwa wasilalamike kuwa hakuna kazi bali wao ndiyo wameshindwa kuona fursa zilizopo na kuzifanya kuwa ajira, hivyo basi kupitia wazo la mheshimiwa Pinda, ujasiriamali ndio utakuwa mkombozi wao," alisema Dk. Seni.

Alisema hivi sasa wahitimu wa vyuo vikuu hawawezi kuona fursa zilizopo kutokana na kutojengewa uwezo katika masomo yao ili kuweza kuzitambua.



Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Udunga (wa pili kulia), akiangalia bidhaa zilizozalishwa na wajasiriamali kwenye maonyesho ya E-dodoma Empowerment 2019, yaliyofanyika katika Uwanja wa Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Sera mpya ya afya sasa kuzingatia hedhi salama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema serikali itahakikisha katika mchakato wa kuundwa kwa sera mpya ya afya suala la hedhi salama linapatiwa kipaumbele.

Waziri Mwalimu aliyasema hayo wakati akizungumza na wadau wa masuala ya hedhi salama katika Maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani jijini Dodoma. Alisema jamii bado ina mitizamo hasi juu ya masuala ya hedhi salama, hali ambayo inahitaji kutolewa elimu ya kutosha katika maeneo mbalimbali nchini. Alisema katika mchakato ambao unaendelea hivi sasa wa kuunda sera mpya ya afya lazima atahakikisha kuwa suala la hedhi salama linatiliwa mkazo ili jamii iweze kushiriki kikamilifu.


Aidha, alisema serikali kuanzia mwakani itashiriki kikamilifu katika maadhimisho hayo na kuziagiza halmashauri zote nchini kufanya maandalizi ya siku hiyo.

"Lakini pia serikali itaendelea kufanyia kazi changamoto zote zilizopo ikiwamo upatikaji wa maji, vyoo, vyumba vya kujihifadhia kwa watoto wa shule pamoja na upatikaji wa vifaa vya kujihifadhia na vile vya kuteketeza," alisema Mwalimu.

Pia alisema pamoja jitihada za serikali katika kuondoa kodi katika taulo laini za kujifadhia, lakini bei zilizopo hivi sasa hazijakidhi matarajio ya watu wengi.

"Sijui ni kwani bei bado zipo juu pamoja na serikali kuondoa VAT...napanga kumwandikia barua Waziri wa Viwanda ili kuona nini shida, lakini pia kwa mzalishaji wa pedi kuanzia mwaka ujao lazima kila paketi ziwe siyo chini ya 10 na siyo vinginevyo," alisema.

Vilevile, alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakikumbana na adha ya kukosa masomo kwa siku tatu hadi tano kila mwezi kutokana na kukosa vifaa vya kujihifadhia wanapokuwa katika hedhi. Suzan Lyimo, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake, alisema umefika wakati masuala ya hedhi yawekwe wazi ili kuijengea jamii uelewa wa mambo hayo kwa sababu si ugonjwa bali ni mabadiliko ya maumbile.





Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, Ahmada Yahya Abdulwakil (kushoto), akibadilishana mawazo na Mwakilishi wa Paje, Jaku Hassan Ayoub, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Vitambulisho Mzanzibari Mkazi vyaanza kuboreshwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi (ZID) vipo katika maboresho makubwa, ili viendane na mifumo wa mitandao mengine inayotumia au kuhitaji utambulisho wa teknolojia ya kielektroniki.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud Mohamed, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi waliolalamika kwa nini vitambulisho vya ZID havitumiki katika kufanya usajili wa simu.

Alieleza kuwa vitambulisho hivyo haviwezi kusomeka katika mitandao mengine kutokana na kutengenezwa tofauti na teknolojia nyingine.

Alisema hivi sasa zinafanyika juhudi ili kitambulisho cha ZID kiweze kuingiliana na kusomeka na vitambulisho vyingine vikiwamo vya taifa.

Alisema matarajio ya serikali ni kwamba vitambulisho vipya vitakavyotolewa hivi karibuni vitakuwa na sifa na ubora na kuingiliana na mitandao mingine na kusomeka vizuri.

Alisema hatua hiyo kwa kiasi kikubwa itasaidia na kutoa urahisi wa kupatikana kwa huduma mbalimbali bila ya usumbufu.

"Serikali inalifanyia kazi suala la kuboresha vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi na kuzingatia mambo muhimu kama usalama," alisema.

# Hakuna kuuza meli MV Maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZANZIBARI wamehakikishiwa kuwa meli ya MV. Maendeleo haitauzwa kwa sababu bado inahitajika kuwahudumia abiria na mizigo katika ukanda wa Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mohamed Ahmada, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani Pemba, Mussa Ali Mussa, aliyetaka kujua lini meli hiyo itafanyiwa matengenezo baada ya kushindwa kufanya kazi kwa muda mrefu sasa.

Ahmada alisema jumla ya dola za Kimarekani milioni 1.3 zinahitajika kwa ajili ya kuifanyia matengenezo meli hiyo ikiwamo kuisafirisha na kuipeleka kwenye (karakana ya kukarabati meli) chelezo.

Alisema hadi sasa jumla ya Dola 500,000 zimepatikana kwa ajili ya kuifanyia matengenezo meli hiyo na kwamba haiwezi kufanyiwa matengenezo yake Zanzibar, kwa hivyo lazima ipelekwe Mombasa.

"Mwenyekiti, MV. Maendeleo inahitaji dola za Kimarekani milioni 1.3 kwa ajili ya matengenezo makubwa na kuipeleka chelezoni, ili iweze kufanya kazi zake za kutoa huduma za usafirishaji abiria na mizigo katika ukanda wa Unguja na Pemba," alisema

# Wadau waunda mtandao kukomesha udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUANZISHWA kwa jumuiya ya mtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika Wilaya ya Kaskazini A kunaelezwa kuwa kutasaidia kuondosha vitendo hivyo katika wilaya hiyo baada ya kuonekana kuwa vimeshamiri kupindukia.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Ame Haji Ame, alieleza kuwa hali si ya kuridhisha katika wilaya hiyo kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo vinavyofanywa dhidi ya watoto na wanawake.

Alieleza kuwa bado jamii haitoi ushirikiano wa karibu kwa mwathirika wa matukio hayo, jambo ambalo linawapa mwanya wadhalilishaji wa kijinsia.

Alisema kuwa mtandao huo utafanya kazi ya kutoa elimu ya udhalilishaji kwa jamii ili kuwa tayari kutoa taarifa za matukio ya udhalilishaji wa kijinsia na kuzifikisha katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

"Hatuwezi kufanikiwa kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia kama jamii yetu haitabadilika na kuwa tayari kutoa taarifa za matukio hayo katika ngazi za kisheria ikiwamo polisi," alisema.

Katibu wa mtandao huo, Mwanajuma Kassim Makame ambaye ni Ofisa wa Wanawake Wilaya ya Kaskazini A Unguja, alisema matukio ya utelekezaji wa wanawake unaofanywa na wanaume yakiwamo wavuvi wakati wanapopiga kambi nje ya Zanzibar yanaongoza wilayani humo.

Alieleza kuwa kwa mwaka 2018-2019 jumla ya matukio 30 ya vitendo vya utelekezaji wa watoto na wanawake yameripotiwa katika wilaya hiyo.

Alisema matukio mengi ya utelekezaji wa familia hufanywa na wanaume wanaojishughulisha na uvuvi wakati wanapokwenda nje ya Zanzibar kwa ajili ya shughuli za uvuvi, ambapo hukaa huko zaidi ya mwezi mmoja sehemu hizo zinazoitwa (dago).

"kipindi cha miaka miwili kuanzia 2018- 2019 yapo matukio 30 ya vitendo vya utelekezaji wa wanawake dhidi ya wake zao zaidi wakati wanapokuwa nje ya nchi kwa shughuli za uvuvi," alisema.

Kwa upande wake Meneja Utetezi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Hawra Shamte, alisema lengo la kuanzishwa kwa mitandao ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia ni kukusanya taarifa na kuweka kumbukumbu ya takwimu za matukio yote yanayohusu ukatili wa kijinsia.

Aidha, alisema kazi za wajumbe wa mitandao ni kufuatilia taarifa zote zinazohusu ukatili wa kijinsia katika maeneo yao na kuripoti katika taasisi husika ikiwamo vyombo vya sheria.

# Wanafunzi 17 wapata ujauzito

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI 17 wa shule za Unguja na Pemba wamepata ujauzito kuanzia mwaka 2018-2019, huku wengine watatu wakiendelea na masomo ya sekondari licha ya kuwa wajawazito kwa kutumia sheria Namba.4 ya mwaka 2005 inayotoa nafasi kwa wanafunzi wa aina hiyo kuendelea na kusoma wakipenda.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema hayo wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019-2020.

Alisema kesi za kuwapa wanafunzi uja uzito zimeripotiwa kwa makamanda wa polisi wa mkoa kwa ajili ya hatua nyingine za kiuchunguzi ikiwamo vipimo vya kuchunguza vinasaba.

Waziri Pembe alisema Zanzibar inaendelea kutumia sheria inayowaruhusu wanafunzi waliopata ujauzito kuendelea na masomo yao wakipenda.

Alisema sheria hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa na kutoa nafasi kwa wanafunzi wa kike kuendelea na masomo yao ambao wengi wanaopata matatizo ya ujauzito ni wale waliopo elimu ya sekondari.

"Mheshimiwa Sheria Namba.4 ya mwaka 2005 ya wali (wanawake wasioolewa) na wajane, wanawake walioachika katika ndoa inatoa nafasi kwa mwanafunzi anayepata ujauzito kuendelea na masomo akipenda. Sheria hii bado ipo na wanafunzi wanaitumia vizuri," alisema.

Aidha, Pembe alisema jumla ya kesi nane za udhalilishaji wa kijinsia kwa wanafunzi kuolewa zimeripotiwa Unguja na Pemba, ambapo kwa mujibu wa sheria NO.6 ya elimu ya mwaka 1986 wanafunzi hao walipoteza sifa na kufukuzwa.

"Sheria ya Wizara ya Elimu NO.6 ya mwaka 1986 hairuhusu mwanafunzi aliyeolewa kuendelea na masomo kwa hivyo wanafunzi hao walifukuzwa shule," alisema.

Pembe alisema wizara ipo katika mikakati ya kuirekebisha ili iendane na wakati na marekebisho ya mambo mbalimbali yakiwamo kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia hayapewi nafasi, huku akiwataka walimu kufuata maadili na kujiepusha na matukio hayo yanayoweza kusababisha kupoteza ajira.

# Ukarabati MV Victoria, MV Butiama waanza

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

MATUMAINI yamerejea kwa wananchi wanaotumia usafiri wa majini katika Ziwa Victoria baada ya ujenzi na ukarabati wa MV Victoria, MV Butiama, chelezo na ujenzi wa meli mpya kuanza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya huduma za meli nchini, Eric Hamissi, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuwa ujenzi wa miradi hiyo unaotekelezwa na kampuni kutoka Korea Kusini, utaigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni 150 na miradi yote imeanza, huku tayari serikali ikilipa malipo ya awali ya asilimia 35 kwa ujenzi wa meli mpya.

Hamissi alisema hatua ya usanifu wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo na gari 20, imekamilika na tayari malipo ya awamu pili yamefanyika, hatua inayofuata ni ya ujenzi unaofanywa na mkandarasi Gas Entec kutoka Korea Kusini.

"Hatua iliyopo sasa hivi Korea Kusini ni ukataji vyuma 'still cutting stage' hivyo vyuma ndiyo vitakavyosafirishwa kuja Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa meli, tunategemea hivyo vyuma vyote vitaingia Tanzania mwezi Septemba mwaka 2019, mzigo wa vyuma vyote hivyo utakuwa takribani kontena 300 za futi 40, kwa hiyo ujenzi hasa utaanza kuonekana mwezi wa kumi (Oktoba) kwa sababu sasa hivi upo kwenye hatua ya makaratasi," alisema Hamissi. Aidha, Hamissi alisema wataalamu wa kuhakiki muundo na maendeleo ya ukataji vyuma hivyo wataenda Korea Kusini mwezi Juni na ujenzi utaanza Oktoba, mwaka huu na kukamilika Septemba 2020.

Alisema ujenzi wa chelezo mahali meli mpya itajengwa kwa makadirio ya kitaalamu, umefikia asilimia 30 na serikali imeshalipa malipo ya awali kwa mkandarasi STX engine akishirikiana na Sekyung, wote wa Korea Kusini.

Aidha, alisema mradi wa ukarabati wa meli ya MV Victoria unaohusisha uwekaji wa injini mpya, jenereta mpya, mitambo ya nguvu, pamoja na vyombo vya uongozaji na uokoaji, utaigharimu serikali Sh. bilioni 22 na vifaa hivyo vitaanza kuingia nchini mwishoni mwa mwezi Juni na ifikapo Machi 2020, meli hiyo itarudi majini na kuanza kutoa huduma kwa wananchi waishio kati ya Mwanza na Bukoba.

"Ujenzi wa MV Butiama unaogharimu Sh. bilioni tano unaendelea na mkandarasi Sekyung kwa kushirikiana na STX engine wanaendelea na kazi na punde meli hiyo itarudi kuanza safari zake kati ya Nansio Ukerewe kama ilivyokuwa inafanya kabla ya meli hiyo kuharibika mwaka 2010," alisema.

Alisema ahadi ya meli mpya inayojengwa sasa ilitolewa miaka 23 iliyopita baada ya ajali ya MV Bukoba iliyotokea mwaka 1996, ahadi hiyo ilishindwa kutimia kutokana na sababu mbalimbali, lakini kwa miaka mitatu ya uongozi wa Rais Magufuli ahadi hiyo inatimia na Watanzania 400 watanufaika na ajira wakati wa ujenzi.

Septemba 3, 2018 Rais Dk. John Magufuli, alishuhudia utiaji sahihi wa mikataba minne ya ujenzi wa meli mpya, chelezo, ukarabati mkubwa wa meli ya MV Victoria na MV Butiama kazi ambayo tayari inaendelea chini ya usimamizi wa kampuni ya huduma za meli MSCL.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kigoma, Raphael Mbwambo, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake eneo la Maweni Manispaa ya Kigoma/Ujiji. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Chavita yatakiwa kupigania lugha ya alama

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

CHAMA cha Viziwi Tanzania (Chavita), kimetakiwa kufanya ushawishi kwa serikali kupitia Wizara ya Elimu, ili kuwezesha somo la lugha ya alama kuingizwa katika mtaala wa shule na vyuo, kwa lengo la kufikisha elimu hiyo kwa watu wengi, ili kurahisisha mawasiliano.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawilo, wakati wa kufunga mafunzo ya lugha ya alama kwa wadau mbalimbali ikiwamo polisi, mahakama, magereza na uhamiaji, mwanasheria kutoka ofisi ya mkuu wa mkoa wa Kagera Jovin Ruttainulwa, alisema somo la lugha ya alama kuingizwa katika mtaala itasaidia kupatikana kwa wataalamu na wananchi wenye ufahamu wa lugha hiyo. "Inaweza ikapangwa ianzie wapi, katika elimu ya msingi, sekondari au vyuo, lakini kwa upande wa pili maana hiyo ni utatuzi wa muda mrefu, kuna umuhimu mkubwa sana kwa Chavita kuwafikia watendaji wa mitaa, vijiji na kata, pia maofisa tarafa maana hawa ndiyo wanafanya kazi zao za kila siku karibu na wananchi," alisema Ruttainulwa.

Kwa upande wake Kaimu Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Bukoba, Wingi Momboka, alisema katika zoezi la uandikishaji vitambulisho vya taifa walikutana na changamoto ya kushindwa kuwasiliana na viziwi na kutoa mfano kuwa kuna sehemu walikwenda wakakuta familia nzima ni viziwi. "Unafanya nini unapokwenda mahali ukakuta familia nzima ni viziwi na wewe hufahamu lugha ya alama, kwa hiyo mafunzo haya ni muhimu sana kwetu," alisema.

Naye Ramadhani Masimbo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi upande wa Idara ya Usalama Barabarani, alisema kuwa viziwi pia ni watumiaji wa barabara ambao nao wanakumbana na changamoto zilizoko barabarani ikiwamo kupata ajali na kuwa linapotokea hilo ni vigumu kuwasiliana naye.

"Hata kuweza kupata anapoishi mhusika au jamaa zake inakuwa ni shida na ni kazi ngumu sana kumpatia fomu ya matibabu (PF3), kwa hiyo kwa utaratibu kama huu mnaoendelea nao wa kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali likiwamo Jeshi la Polisi, ni jambo jema na limefika kwa wakati mwafaka," alisema.

# Wataka taulo mfumo wa bima

**Na Happy Severine,** MASWA

LICHA ya serikali kufanya jitihada kubwa za kuondoa kodi katika taulo za kike, bado wadau wa taasisi mbalimbali na wanawake wilayani Maswa wamelalamikia bei ya taulo hizo kuwa kubwa.

Bei hiyo hailingani na vipato walivyonavyo wakazi wa maeneo hayo.

Malalamiko hayo walitolewa jana wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani ambapo katika mkoa wa Simiyu yaliadhimishwa katika kijiji cha Shishiyu wilayani Maswa chini ya utaribu wa Shirika la World Vision.

Wamesema kuwa bado baadhi ya jamii hazina uwezo wa kununua bidhaa hizo na badala yake wameshauri serikali ifanye utaratibu wa kuzitoa kama dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya sambamba na kuingizwa katika mfumo wa bima ya afya.

"Tunaiomba serikali kubadilisha mfumo na utaratibu wa upatikanaji wa taulo hizo kutoka katika mfumo wa kuuzwa madukani na badala yake ziingizwe kwenye mfumo wa bima ya afya," alisema mkazi mmoja.

Mkazi wa kijiji cha Shishiwi, Tereza Ngaka, alisema kuwa mbali na kuondolewa kodi katika taulo za kike, bado taulo hizo zinapatikana kwa bei kubwa maeneo ya vijijini na wazazi wengi wenye maisha duni wanashindwa kumudu kununua.

"Watoto wetu wamekuwa wakiteseka kwa kukosa hizi taulo, wanalazimika kutumia soksi, kanga na vitu vingine pindi wanapoingia kwenye siku zao, inawafanya kutokuwa huru darasani, gharama zimekuwa kubwa ambazo wazazi wengi wanashindwa kuzimudu," alisema Ngaka.

# Umuonapo kijana huyu toa taarifa



**Na Mwandishi Wetu**

KIJANA Michael Mbogela (15) (pichani), anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao, Nianjema Bagamoyo mkoani Pwani na kwenda kusikojulikana, na taarifa zake zimefikishwa kituo cha polisi.

Kaka wa kijana huyo, Faraja Nwaka, alisema alitoweka nyumbani kwao Mei 14, mwaka huu, majira ya mchana, na kuwa wametafuta maeneo mbalimbali bila mafanikio, hivyo kufungua jalada katika kituo cha Polisi Bagamoyo, BAG/RB/1635/2019.

"Tumeamua kufika katika ofisi za gazeti hili kwa ajili ya kupata msaada zaidi na tunawaomba wasamaria wema watakaomuona mdogo wangu watoe taarifa katika kituo chochote cha polisi, na pia wawasiliane nasi kwa namba 0765-566821, 0658-331980 na 0715-506427," alisema Nwaka.

## HABARI KIMATAIFA

### Hatua ya Marekani yaathiri wateja

**BEIJING,** China

MWANASHERIA wa Kampuni ya Mawasiliano ya China ya Huawei, Song Liuping, amesema uamuzi wa Marekani kuiorodhesha katika kampuni zinazolengwa kibiashara itaathiri mabilioni ya watumiaji wake.

Akizungumza na waandishi wa habari, Liuping amesema katazo la kibiashara la Marekani, litawaathiri moja kwa moja kampuni za Kimarekani pamoja na ajira.

Hivi karibuni Marekani iliiorodhesha Huawei katika msururu wa kampuni ambazo Marekani imeyapiga marufuku kufanya nao biashara hadi watakapopata leseni maalumu.

Marekani ilichukua uamuzi wa kuizuia Huawei ambayo ni wazalishaji wakubwa duniani wa vifaa vya mawasiliano kwa kile ilichodai kuwa kampuni hiyo imekuwa ikidukua taarifa na ni hatari kwa usalama.

Huawei mara zote imekuwa ikikanusha tuhuma za Marekani ikisisitiza kuwa ni kampuni huru na haina uhusiano wowote na serikali.

Kampuni hiyo inasema uamuzi wa Marekani kuiorodhesha Huawei kama moja ya kampuni mbaya kiusalama, ina madhara makubwa kuliko utawala wa Washington unavyokadiria.

"Uamuzi huu unatishia kuwadhuru zaidi ya wateja wetu katika nchi 170 duniani, wakiwamo watu bilioni tatu ambao wanatumia bidhaa na huduma za Huawei," imesema taarifa ya kampuni hiyo. **RFI**

### Njiwa amuepusha dereva kulipa faini

**BONN,** Ujerumani

DEREVA aliyekuwa akiendesha gari kwa kasi nchini Ujerumani amenusurika kulipa faini ya paundi 93 baada ya njiwa mweupe kumuepusha kutambulika sura yake.

Mtu huyo alinaswa kwenye kamera za mwendo kasi, lakini sura yake ilifichwa na mabawa ya ndege huyo alipokuwa akiruka mbele ya kioo cha gari. Taarifa ya polisi inasema pengine "Roho mtakatifu" aliingilia kati, ishara ya njiwa mweupe kama alama ya uwepo wa Mungu katika imani ya dini ya kikristo.

"Tumeelewa ishara hiyo na kumuacha dereva kwa amani wakati huu."

Lakini maofisa katika mji wa Viersen, karibu na mpaka wa Ujerumani waliongeza: "Tuna matumaini kuwa dereva huyo aliyesaidiwa anaelewa 'onyo hili kutoka juu' na kuwa ataendesha vizuri siku za usoni."

Polisi imeeleza kuwa dereva huyo alikuwa akisafiri kwa kasi ya kilometa 54 kwa saa katika barabara ambayo alipaswa asafiri kwa kilomita 30 kwa saa.

Kutokana na gari pekee kubainika na siyo dereva, alinusurika kulipa faini hiyo "ashukuriwe malaika yule mwenye mabawa ambaye mbawa zake zilizuia sura ya dereza".

Polisi wa mji wa Viersen amesema kuwa njiwa huyo naye angetozwa faini kwa kupita kwa kasi kwenye eneo asilopaswa kupita. **BBC**

# Upinzani Malawi wapinga matokeo urais mahakamani

**BLANTYRE,** Malawi

CHAMA kikuu cha upinzani nchini Malawi, kimekwenda mahakamani kupinga matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Urais wa Mei 21, kikisema kulikuwa na dosari nyingi.

Kiongozi wa chama cha Malawi Congress, Lazarus Chakwera, amesema ni lazima kuwe na uwajibikaji kutokana na baadhi ya watu kukiuka waziwazi sheria za uchaguzi.

"Ni mfumo wa uchaguzi ambao maofisa wa tume wanaweza kutumia wino maalumu katika kufuta matokeo ya kwenye karatasi halisi nchi nzima... na bado watu wasichukuliwe hatua," alisema.

**Ni mfumo wa uchaguzi ambao maofisa wa tume wanaweza kutumia wino maalumu katika kufuta matokeo ya kwenye karatasi halisi nchi nzima...**

Chakwera ambaye alipata asilimia 35.41 ya kura zote, alishindwa na Rais Peter Mutharika ambaye katika uchaguzi huo alipata asilimia 38.57, huku wakitenganishwa na kura 150,000.

Wakati upinzani ukipinga matokeo ya uchaguzi huo, Rais Mutharika baada ya kuapishwa Jumanne ya wiki hii, aliwataka wanasiasa wa upinzani kukubali kushindwa na kuijenga nchi yao. Rais Mutharika alitumia hotuba yake kuwataka wanasiasa wa upinzani kuungana na kumsaidia kuijenga upya Malawi aliyosema imeendelea kukabiliwa na changamoto za kiuchumi.

"Ni muda wa kusonga. Hakuna muda wa kupigana. Kuna muda wa kuungana, na kuiendeleza nchi," alisema Rais Mutharika wakati akiwahutubia maelfu ya wafuasi wake kwenye uwanja wa Kamuzu mjini Blantyre.

Rais Mutharika kwa upande wake ametupilia mbali madai ya upinzani, huku akisema waangalizi wa kimataifa waliutaja uchaguzi wa Mei 21, kuwa ulikuwa uchaguzi huru na wa haki.

"Ni ushindi kwa utawala wa sheria na demokrasia. Demokrasia imeshinda," alisema Rais Mutharika.

Mgombea mwingine wa upinzani, Saulos Chilima, ambaye alikuwa Makamu wa Rais wa Mutharika wakati wa muhula wake wa kwanza, aliyejiondoa kwenye chama tawala kuwania urais, alipata asilimia 20.24 ya kura zote.

Chilima kwa upande wake alikubali kushindwa na kumpongeza bosi wake wa zamani kwa ushindi alioupata. **RFI**



Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, akitia saini ya kiapo cha kutumikia muhula wa pili wa urais kwa kipindi cha miaka minne, mjini Abuja, Nigeria jana. **PICHA: RFI**

# Hali ya watoto duniani imeboreka

**BONN,** Ujerumani

RIPOTI kuhusu hali ya watoto duniani iliyochapishwa na Shirika la Wahisani linaloshughulikia Haki za Watoto la Save the Children inaonyesha maendeleo makubwa katika sekta za afya, elimu na usalama katika nchi kadhaa.

Shirika hilo limesema ripoti yake ya kila mwaka, hali ya maisha ya watoto duniani imeimarika katika jumla ya nchi 173 kati ya 176 ambazo ilizifanyia utafiti.

"Angalau watoto milioni 280 duniani kote wana maisha bora ukilinganisha na ilivyokuwa miaka 20 iliyopita," ilisema ripoti hiyo.

Hata hivyo, ripoti hiyo inaonyesha kwamba robo ya watoto duniani kote bado wananyimwa haki ya usalama na kufurahia utoto, ambapo wengi bado wanakimbia makazi yao au kukwama katika nchi zilizo na mizozo.

Katika ripoti hiyo, Singapore inashika nafasi ya juu katika viwango vya ulinzi na huduma kwa watoto, ikifuatiwa na mataifa manane ya Ulaya ikiwamo Ujerumani pamoja na Korea Kusini.

Ripoti hiyo inataja nchi zilizoshika nafasi ya mwisho ambazo ni Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Mali na Sudan Kusini licha ya kushuhudiwa maendeleo katika miaka ya karibuni.

Niger ni mojawapo ya nchi iliyopiga hatua kubwa katika kuboresha maisha ya watoto ndani ya miongo miwili iliyopita ikifuatiwa na Rwanda, Sierra Leone na Ethiopia.

Katika ripoti hiyo ya mwaka huu, Marekani ipo nafasi ya 36 ikiwa sawa na China.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Carolyn Miles, alisema ripoti hiyo ilizingatia viashiria vinane vya ukuaji wa mtoto ikiwa ni pamoja na mtoto kunusurika, elimu, ajira za watoto na ndoa za mapema ikilinganisha na mwaka 2000.

"Kumekuwa na maendeleo mazuri ukiangalia duniani kote," alisema mkurugenzi huyo.

Aidha, watoto milioni 420 wanaishi katika maeneo yaliyo na mizozo duniani kote, ikiwa ni mara mbili ya idadi ya mwaka 1995 na takribani watoto milioni 31 hivi sasa wamelazimika kuyakimbia makazi yao.

Ripoti hiyo iliyotolewa kuelekea Siku ya Mtoto Duniani ambayo ni Juni mosi, inakadiria kuwa jumla ya watoto milioni 690 wanaporwa utoto wao kutokana na maradhi, vifo, ndoa za utotoni, mimba za mapema, utapiamlo au kushindwa kuhudhuria shule.

Ukilinganisha na mwaka 2000, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 49, ajira za watoto asilimia 40, utapiamlo sugu na ndoa za utotoni.

Ripoti hiyo inasema kati ya viashiria vinane vilivyotumika, kiashiria kimoja kimeonekana kuchomoza zaidi ambacho ni idadi ya watoto wanaoishi katika maeneo yenye mizozo au walioathiriwa na vurugu. **DW**

# Walinzi 3,800 wafa ulinzi wa amani UN

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ulinzi, Dk. Hussein Mwinyi, amesema takwimu zinaonyesha tangu mwaka 1948 walinzi wa amani waliopoteza maisha ni 3,800.

Dk. Mwinyi alitoa takwimu hizo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Walinda Amani iliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Alisema siku hiyo ni muhimu kwa sababu pamoja na kuwapongeza walinda amani waliopo nchi mbalimbali akitekeleza jukumu hilo, wanawakumbuka na wale waliopoteza maisha wakati wakilinda amani nchi mbalimbali.

"Takwimu zinaonyesha walinda amani 3,800 wamepoteza maisha kutokea jukumu hilo limeanza mwaka 1948, tupo hapa kwa ajili ya kuwapongeza wanaoendelea na kazi hiyo na kuwakumbuka waliopoteza maisha," alisema.

Alisema idadi karibu walinda amani 100,000 sasa hivi wapo nchi mbalimbali wakilinda amani na madhumuni ya siku hiyo ni kuwapongeza kwa kazi wanazozifanya za kujitoa.

Alisema Tanzania ina jukumu hilo ndio maana nchi ipo mstari wa mbele katika kuhakikisha walinzi wa amani wapo nchi mbalimbali.

"Kwa sasa tupo Darfur, Sudan, DRC (Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo), Afrika ya Kati, Lebanon na nyingine. Kama nchi tumelichukua jukumu hili na tunaendelea kupeleka walinzi, ambapo Umoja wa Afrika au Umoja wa Mataifa unapotuomba tufanye hivyo," alisema.

Mlinda amani, Mrakibu Msaidizi wa Polisi kutoka Makao Makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani, Mbunja Matibu, alisema ameshiriki ulinzi wa amani kuanzia mwaka 2010 mpaka 2013 Darfur nchini Sudan.

"Tulikwenda kulinda kundi maalum la watoto na wanawake, wazee na wengine kwa sababu kulikuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu, wanawake walikuwa wakienda kukata kuni tulikuwa tunawasindikiza ili wasifanyiwe matendo ya kiharamia na ubakaji ambao ulikuwa umekithiri," alisema.

Pia alisema walikuwa wanahakikisha katika nchi hizo hakuna ndoa za ututoni kwa sababu kulikuwa na watoto wadogo walikuwa wanaolewa na kukatishwa masomo hivyo waliipa elimu jamii husika.

Naye, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Alvaro Rodriguez, alisema katika sherehe za kukabidhi zawadi kwa walinda amani iliyofanyika Mei 24, Katibu Mkuu wa UN alitoa kwa watu 119 ambao ni polisi, wanajeshi na raia waliopoteza maisha mwaka 2018 na kwa mwaka huu ambapo Watanzania walikuwa ni sita.



Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Biashara ya DCB, James Ngaluko (katikati), akizungumza, wakati wa uzinduzi wa akaunti mpya ya muda maalum ijulikanayo kwa jina la 'DCB Lamba Kwanza', jijini Dar es Salaam jana, itakayomwezesha mteja kupata riba ya hadi asilimia 14 papo hapo mara baada ya kuwekeza. Wengine ni maofisa waandamizi wa benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wabunge walia na gharama za umeme

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wameitaka Wizara ya Nishati kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya umeme inayotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na kuangalia namna ya kupunguza gharama za huduma ya umeme kwa wananchi.

Watunga sheria hao walitoa rai hiyo bungeni jijini Dodoma jana walipokuwa wanachangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha.

Mbunge wa Kibakwe, George Simbachawene (CCM), alisema umeme utakuwa na tija kama utaenda katika huduma za kijamii na shughuli za uzalishaji.

Mbunge huyo ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini katika serikali ya awamu ya nne, alisema gharama za uzalishaji wa umeme kwa sasa ziko juu, hivyo serikali inatakiwa kuliangalia jambo hilo wakati ikielekea katika uchumi wa kati.

"Gharama za uzalishaji ziko juu, tunaposema uchumi wa viwanda, hatuwezi kufika bila kushughulika na jambo hili. Hizi kelele zipo tu, tusibadilishe mwelekeo sababu ya kelele. Kuna nchi gani inaupinga huu mradi wa Stiegler's Gorge? Tunaomba waziri kanyaga mafuta twende mbele," alisema.

Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia (CCM), alimtaka Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kuangalia suala la utoaji wa leseni kwa ajili ya kutafuta gesi.

Ghasia alisema tangu waziri huyo aingie madarakani, hajatoa leseni hata moja ya kutafuta gesi.

"Nikuombe chondo chonde kwa Kimakonde, kwanini hivi vibali vinachukua muda mrefu? Tukuombe hayo majadiliano yakamilike ili vibali vitolewe, tangu Kalemani umeingia haujatoa leseni hata moja, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu upo, naomba hili mnijibu," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Upendo Peneza (Chadema), aliitaka Wizara ya Nishati kuunda kitengo maalum cha kusimamia miradi ya umeme inayotekelezwa na REA. Peneza alisema kumekuwa na changamoto katika usimamizi wa miradi ya umeme inayotekelezwa na REA.

# PAET, TPDC wakubaliana mkataba mrefu mauzo gesi

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Pan-African Energy Tanzania (PAET) imeingia mkataba wa makubaliano ya muda mrefu ya mauzo ya gesi (GSA) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kwa lengo la kukidhi ongezeko la mahitaji ya umeme nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa makubaliano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa PAET, Andrew Hanna, alisema mkataba huo unatoa fursa ya usambazaji wa mpaka kufikia futi za ujazo milioni 20 za gesi asilia kwenye mitambo ya taifa ya gesi asilia inayoendeshwa na TPDC katika kisiwa cha Songo Songo, ambapo gesi hiyo itafanyiwa uchakataji na kisha baadaye kusafirishwa kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya uzalishaji wa nishati ya umeme.

"Kuanzishwa kwa makubaliano ya GSA kunaiwezesha PAET kuendelea kukidhi ongezeko la mahitaji la hivi karibuni kwa misingi ya muda mrefu, ikiwa inahakikisha TPDC inaweza kuisaidia Tanesco katika kudumisha uzalishaji na upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika na katika maeneo mbalimbali," alisema Hanna.

Aliongeza kuwa kutokana na kuanzishwa kwa uwezo wa ziada wa uzalishaji katika kitalu cha Songo Songo, PAET ina ujazo wa kutosha wa gesi uliopo tayari kukidhi ongezeko kubwa la mahitaji lililopo wakati Tanesco ikiendelea kupanua uwezo wake wa uzalishaji wa umeme, TPDC itaendelea kupanua mauzo ya gesi na biashara ya usambazaji, kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya gesi viwandani.

Hanna, alisema kuwa maendeleo ya Kitalu inahakikisha PAET inapata ujazo wa gesi ya kutosha kwa ajili ya kukidhi haraka mahitaji ya gesi ya hapo baadaye ambapo kampuni iko katika hatua za mwisho za kufunga mfumo wa kihifadhi gesi 'refrigerator' katika mitambo ya kuchakata gesi cha Songas katika kisiwa cha Songo Songo.

"Hii ni sehemu ya mpango wa jumla ambao hatimaye utajumuisha mitambo ya ukandamizaji na utaongeza zaidi na kudumisha upatikanaji wa gesi kuendana na mahitaji," alisema na kuongeza:

"Kwa kuangalia mbele, uwezo wa kubadilika na ushirikiano leo PAET iko katika nafasi nzuri kufikia mahitaji ya hivi karibuni na yajayo ya nishati ya umeme Tanzania," alisema Hanna.

Alisema mauzo ya gesi chini ya mkataba wa makubaliano wa GSA utakuwa badala ya futi za ujazo 20MM ya 35 MM ambazo zimeuzwa hivi karibuni na kampuni ya PAET chini ya mkataba wa makubaliano ya mauzo ya muda mfupi ulioanzishwa na TPDC na Tanesco Desemba mwaka jana.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MAGARI NA VIPURI**

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836

**MCHANGANYIKO**


**TUNATAFUTA MAWAKALA** wakununua mifuko rafiki wa mazingira kwa jumla. piga 0784000082, 0754710079


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI




**Boko Jumbe** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0312/0100** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 1988 ktika Shule ya sekondari Highlands.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: IRI/RB/23676/2019**

115251802

## KUPOTEA KWA CHETI



**John S. Edward** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1227/0063** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Misasi.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa : KAZ/RB/35/2019**

115252302

## KIMEPOTEA KWA CHETI



**ABUU HAMADI RASHIDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0306/0116** kilichotolewa na **DODOMA SEC.SHOOL** mwaka 2016.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/32282/2019.**

215252002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA.**

**YAH; MAOMBI YA MSINGI NA.24/2019.**

**KAZANA MAJURA...............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**JUMA R.FORODHA...............WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA JUMA R. FORODHA**

Popote Mlipo Mnaarifiwa Mfike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya KILOSA tarehe 10/06/2019 wenyewe binafsi au Wawakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa maamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 21 Mwezi 05 mwaka 2019.

115253102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 117/2019**

**Ombi la GODFREY CHARLES KAZANA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LILIAN CHARLES KAZANA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 27/05/2019.

115253202

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**LAND REVIEW NO 2 OF 2018**
**(C/F High Court Land Appeal No. 14 of 2017, District Land and Housing Tribunal of Karatu at. Karatu Land Case No. 4 of 2015).**

EUGENI PATRICE
MATEO PATRICE...................APPELLANTS
VERSUS
MARCELINA PATRICE.................RESPONDENT

**NOTICE OF HEARING**

TO: Marcelina Patrice
C/F Advocate J. Siay,
JK Siay & Co.
Namvua Plaza,
3rd Floor Near Arusha Main Bus Stand (Namanga Side),
P.o.box 7043,
Arusha.

**TAKE NOTICE** that above appeal has been fixed for Hearing in the High Court at Arusha on 10th day July,2019 at 09:00 o'clock.
YOU may appear in person or by Advocate or agent duly authorised to apoear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to realy upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time before mentioned,the Court may proceed to hear the appeal and pronounce Judgement in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 15th day of May,2019

215252202

## ILANI

**SECURITY DISTRIBUTORS LIMITED**

Inatolewa ilani kwa watu wote kwamba kampuni tajwa hapo juu iko mbioni kufutwa kwa ridhaa yetu.

**Wanahisa**

215252902

## KUPOTEA KWA KADI

**Sanli Afrika Development** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba **MC 117 ANQ** aina ya SANLI.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/2205/2019**

115251902

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455.**
**Fax: +255 26 2323233.**
**Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.**
**Tovuti: www.mwtc.go.TZ.**

**Mtaa wa Moshi**
**S.L.P 2888,**
**40470DODOMA**
**29/05/2019.**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMANNE tarehe 04/6/2019** kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **ARUSHA kuelekea KASULU** gari hilo lenye namba za usajili : **T188APK, T741CPB.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
**Urefu - mita 17**
**Upana - mita 2.6**
**Kimo - mita 1**

3. Njia itakayotumika ARUSHA hadi KASULU kupitia TABORA gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00Jioni).

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

2152522602


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

***0767 223311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# POCHETTINO KAOKOA KIPAJI CHANGU – LLORIS

**LONDON,** England

HUGO Lloris amemshukuru Mauricio Pochettino kwa kunusuru kipaji chake pale Tottenham wakati wakielekea kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool Jumamosi hii.

Golikipa huyo wa Tottenham mwenye umri wa miaka 32, kwa sasa yupo katika msimu wake wa saba na klabu hiyo baada ya kujiunga nayo akitokea Lyon mwaka 2012 kwa ada ya euro milioni 10, pamoja na bonasi ya euro milioni tano.

Hata hivyo, mambo yangeweza kuwa magumu mno kama Pochettino asingemuweka benchi Tim Sherwood mwaka 2014.

"Ni rahisi," alisema Lloris akiiambia ESPN FC katika mahojiano maalum.

"Wakati ule, baada ya miaka miwili na klabu, sikufurahia jinsi mambo yalivyobadilika. Nilijiuliza maswali mengi mno. Halafu nikakutana na Pochettino."

Baada ya misimu miwili migumu chini ya Andre Villas-Boas na baadaye chini ya Sherwood, Lloris angeweza kuondoka klabuni.

Hata hivyo, Pochettino alimchukua kutoka Southampton na kumshawishi nahodha huyo wa zamani wa Lyon kubakia hapo.

"Haraka nilipokutana naye, nilimjua haraka tu kwamba ni mtu sahihi kwa upande wangu," aliongeza kusema Lloris.

"Ni aina ya mtu ambaye unaweza kufanya naye kazi bila matatizo yoyote, kwamba huwezi kupigana naye. Ni vigumu kumwelezea zaidi, lakini ni mtu aliyesaidia zaidi kipaji changu."



# Villas-Boas kocha mpya Marseille

**MARSEILLE,** Ufaransa

ANDRE Villas-Boas ameteuliwa kuwa kocha mpya wa Marseille kwa mkataba wa miaka miwili akichukua nafasi ya Rudi Garcia, ambaye ameiongoza klabu hiyo katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu huu.

Kocha huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur na Chelsea amekuwa hana timu tangu alipoondoka katika Klabu ya Shanghai SIPG Novemba mwaka 2017 na awali alisema angependa kwenda kufundisha timu kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Hata hivyo, kocha huyo mwenye umri wa miaka 41, amekubali mpango wa kuwa kocha mpya wa Marseille baada ya kufanya mazungumzo na rais wa klabu hiyo, Jacques-Henri Eyraud na Mkurugenzi wa Michezo, Andoni Zubizarreta katika siku za hivi karibuni.

"Tuna furaha kumleta kocha mpya mwenye mafanikio na anayetambulika barani Ulaya na duniani," alisema mmiliki wa Marseille, Frank McCourt.

"Falsafa ya ufundishaji wa soka wa Andre Villas-Boas ndicho kitu tulichokiangalia zaidi na kwa namna yoyote atatosha kuifundisha timu yetu na kuipeleka mbali.

"Matarajio yetu ni kwamba ataipeleke mbali timu yetu na kuweza kufanya vizuri katika kila mashindano."

Villas-Boas, ndiye kocha mdogo zaidi kushinda taji la Ulaya wakati alipoiongoza Porto kutwaa Kombe la Ligi ya Europa mwaka 2011 wakati huo akiwa na umri wa miaka 33, na aliwasili pale Stamford Bridge kipindi cha majira ya joto mwaka 2011.

# Coutinho, Dembele chambo ya Neymar




**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona inapanga kumrudisha Neymar kwa kumtoa Philippe Coutinho au Ousmane Dembele pamoja na kiasi cha fedha, Sky Sports imeripoti.

Barca ilimuuza Neymar kwenda PSG kwa euro milioni 222 misimu miwili iliyopita, na sasa wanapanga kumrudisha kwa kumtoa kati ya Dembele au Coutinho, ambao wote hawajawa na msimu wa kuvutia zaidi hapo Catalunya.

Barca watalazimika kuingia mfukoni kumlipa Neymar mshahara wa euro milioni 30 baada ya makato ya kodi, huku mshambuliaji huyo wa PSG akionyesha wazi nia yake ya kutaka kurudi Hispania.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, wameripotiwa kwamba hawataki kumuachia mchezaji huyo, lakini kutokana na yeye mwenyewe kutaka kuondoka ni wazi kwamba anaweza akarudi pale Barca.

Baada ya kutolewa na Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, PSG ilishinda mechi tatu tu kati ya 10, kitu kinachoonyesha kwamba miamba hao kutoka Jiji la Paris hali si shwari.

Neymar pia amekuwa akitajwa kuwaniwa na Klabu ya Real Madrid ambayo pia inamnyatia kiungo wa Manchester United, Paul Pogba.

# Real Madrid klabu ghali zaidi kwa sasa



**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeipiku Manchester United kwa kutajwa kuwa klabu yenye thamani zaidi kibiashara barani Ulaya kwa kiwango cha euro zipatazo bilioni 3.22 kwa mujibu wa tafiti iliyofanywa na KPMG.

Klabu hiyo ya Hispania imetajwa kuwa juu katika thamani ya kibiashara baada ya kuripotiwa kwa matokeo ya utafiti uliofanyika katika msimu wa mwaka 2016 -2017 na 2017-2018 ukiangalia namna timu zinavyopata faida, umaarufu wa timu na thamani ya kiwanja.

Michuano ya mwisho ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliiweka Liverpool na Tottenham Hotspurs katika nafasi ya saba na tisa. Na katika ligi ya mwisho ya Ulaya, Chelsea na Arsenal walitajwa katika nafasi ya sita na nane.

Manchester City iko nafasi ya tano, hii ikiwa inamaanisha kuwa klabu sita za England zimeingia 10-bora.

Real Madrid imeshinda mashindano ya Ligi ya Mabingwa katika misimu miwili ambayo imeweza kuipa timu hiyo fursa ya kuwa juu katika soko kwa asilimia 10. Vilevile klabu ya Celtic imejumuishwa katika orodha ya klabu 32 ambazo ziko juu.

Mwandishi wa michezo wa kimataifa, Andrea Sartori, amesema kwamba kwa ujumla thamani ya sekta ya mpira wa miguu imekuwa kwa asilimia tisa ukilinganisha na miaka iliyopita.

"Kwa ujumla thamani ya kibiashara ya klabu 32 za juu imesababisha ongezeko la asilimia tano kwa jumla katika tozo za kodi," alisema Andera.

Kwa upande mwingine gharama ya wachezaji imeendelea kukua pia, hivyo kusababisha klabu hizo bora kuongezeka kwa pointi nne mpaka asilimia 63.

**KLABU BORA 10**

| | |
|---|---|
| Real Madrid | - Euro bilioni 3.224 |
| Man United | - Euro bilioni 3.207 |
| Bayern Munich | - Euro bilioni 2.696 |
| Barcelona | - Euro bilioni 2.676 |
| Man City | - Euro bilioni 2.460 |
| Chelsea | - Euro bilioni 2.227 |
| Liverpool | - Euro bilioni 2.095 |
| Arsenal | - Euro bilioni 2.008 |
| Tottenham | - Euro bilioni 1.697 |
| Juventus | - Euro bilioni 1.548 |

# KEITA ATAIKOSA SPURS-KLOPP




**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imepata pigo kubwa baada ya kiungo wake, Naby Keita kuripotiwa kwamba ataukosa mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumamosi hii.

Liverpool wataikosa huduma ya kiungo huyo wakati watakapoivaa Tottenham Hotspurs kwenye fainali hiyo itakayochezwa jijini Madrid nchini Hispania kutokana na kuwa majeruhi.

Keita alipata majeraha hayo kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Barcelona.

Kiungo huyo amesafiri na timu kwenye kambi ya Marbella na wachezaji wenzake kwenye maandalizi ya awali ya mchezo wa fainali.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp amethibitisha kwamba, hatamtumia kiungo huyo kwenye mchezo wake wa fainali utakaopigwa Juni Mosi, mwaka huu jijini Madrid.

# *Arsenal wampa sharti Emery kumsajili Umtiti*

**LONDON,** England

UONGOZI wa Klabu ya Arsenal umemwambia kocha wake, Unai Emery kwamba kama wataifunga Chelsea na kutwaa taji la Ligi ya Europa, watamsajili beki wa kati wa Barcelona, Samuel Umtiti.

Kocha Emery amekuwa na mipango ya kuisuka upya Arsenal yake hasa safu ya ulinzi, lakini jambo hilo litafanyika kama tu watashinda fainali hiyo ili kukata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Kwa maana hiyo kama hakutakuwa na michuano ya Ulaya msimu ujao, kocha Emery atabidi apambane tu na hali yake na kuendelea kubaki na mabeki waliopo kwa sasa kwenye kikosi chake.

Umtiti kwa sasa amekuwa wa nyongeza tu huko Barcelona baada ya Gerard Pique na Clement Lenglet kuanza, huku wababe hao wa Nou Camp wakipiga hesabu za kumnasa beki wa Ajax, Matthijs de Ligt.

Kutokana na hilo, Barcelona wanafikiria tu kumpiga bei Umtiti na wapo tayari kupokea ofa ya Pauni 50 milioni tu, lakini Arsenal hawatakuwa na pesa hiyo kama watashindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.



# DO A SOKA
# MAG A ULAYA




# SALAH KUITUNGUA SPURS KUTIBU JERAHA MADRID

●●● Si ndoto tu, nitafunga kweli na kutwaa ubingwa wa Uefa kisha ule wa Mataifa ya Afrika...

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Mohamed Salah ana ndoto za kufunga bao la ushindi kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati huu akitazama kutibu majeraha yake ya michuano hiyo msimu uliopita.

**Salah na Liverpool watarudi kwa mara ya pili mfululizo kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati watakapowavaa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Tottenham jijini Madrid Jumamosi.**

Liverpool ilipoteza kwa mabao 3-1 dhidi ya Real Madrid mwaka jana - matokeo yaliyochangiwa na majeraha ya bega kwa Salah ambayo yalimlazimu mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Misri kutoka nje ya dimba jijini Kiev akibubujikwa na machozi.

Lakini Salah -ambaye amefunga mabao 26 katika mashindano yote msimu huu - anataka kusahau maumivu hayo ya mwaka jana.

"Ni mwenye furaha kwamba nina nafasi tena ya kucheza fainali nyingine. Ninatumai safari hii ninaweza kucheza kwa muda wote wa mchezo," Salah aliiambia beIN SPORTS.

"Nina furaha sana kwa hilo. Ninatumai tunaweza kusahihisha kile kilichotokea msimu uliopita, kupata matokeo mazuri na kutwaa ubingwa."

Alipoulizwa kama ana ndoto za kufunga bao la ushindi kwa Liverpool, Salah alijibu: "Si ndoto tu. Ninatumai itakuwa kama ukweli na nitafunga katika fainali, kisha pia kutwaa ubingwa wa michuano ya Mataifa ya Afrika [itakayofanyika Misri mwezi ujao] ."

Salah aliongeza: "Hii ni fainali yangu ya pili mfululizo. Tulipoteza ya kwanza, lakini kila kitu kipo vizuri wakati huu na tuna uzoefu zaidi kuliko kipindi kilichopita.

"Tunatazama mbele na tumekuwa na maandalizi mazuri tukiwa hapa Hispania. Tunarudi Liverpool na tunajisikia kama wachezaji waliohamasika sana na benchi la ufundi. Ninatumai tutashinda safari hii.

"Tumekuwa na maandalizi makubwa Hispania na ni wakati mzuri wa kujiandaa pale. Timu kwa sasa ipo katika kiwango kizuri kiutimamu wa mwili. Hivyo natumai mwisho huu ulikuwa

## ZISIKUPITE

### HAZARD KIMEELEWEKA REAL

REAL Madrid inaamini wamekubaliana na Chelsea dili la pauni milioni 115 kwa kiungo Mbelgiji Eden Hazard, 28. ***(Sun)***

### LUKAKU ALILIA KUTUA INTER

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Ubelgiji, Romelu Lukaku, 26, yupo tayari kukatwa malipo yake ili kufanikisha uhamisho wake wa kujiunga na Inter Milan majira haya ya joto. ***(Gazzetta dello Sport)***

### ARSENAL YAMTAKA MEUNIER

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, anataka kumsajili beki wa kulia, Mbelgiji Thomas Meunier, 27, kutoka kwa klabu yake ya zamani Paris St-Germain. ***(France Football)***

### CONTE AMWAGA WINO INTER

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte, amesaini dili la kuwa kocha wa Inter Milan hadi mwaka 2022 - ikiwa ni miaka mitano tangu Mtaliano huyo kufanya kazi Serie A. ***(Tuttomercatoweb - in Italian)***

### KUVAA VIATU VYA COSTA

ATLETICO Madrid imemchagua mshambuliaji wa Paris St-Germain, nyota wa kimataifa wa Uruguay, Edinson Cavani, 32, kama mbadala wa straika Mhispania Diego Costa. ***(Cadena Ser - in French)***

### LAMPARD KUMRITHI SARRI

CHELSEA itahitaji kumrejesha Frank Lampard ambaye amekuwa katika mpango wao wa muda mrefu kama kocha endapo Maurizio Sarri atarudi Italia majira haya ya joto. Kiungo huyo wa zamani wa 'Blues' na England, Lampard ameiongoza Derby kucheza mechi ya fainali ya mchujo ya Championship katika kipindi chake cha kwanza uongozini. ***(Mail)***

### SOLSKJAER AJIPANGA UPYA

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameuweka mwaka ujao wa mwisho kwake kukamilisha mchakato kuuza wachezaji wote asiowataka ili kuisuka upya Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### AHAKIKISHIWA ULAJI BARCA

MABINGWA wa Hispania, Barcelona wameamua kuendelea na Ernesto Valverde kama kocha wao licha ya taarifa kwamba amekalia kuti kavu. ***(Marca)***

### ALDERWEIRELD KUKOMAA

BEKI wa Tottenham, Toby Alderweireld, 30, anatarajia kuendelea kuitumikia klabu hiyo msimu ujao licha ya kuwapo kwa taarifa zinazomhusisha na Manchester United. ***(Mail)***

### WILSON KUACHANA NA LIVER

WINGA wa Liverpool na Wales, Harry Wilson, 22, ameamua kuondoka Anfield ili kutafuta nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza baada ya kuitumikia Derby kwa mkopo kwa kipindi kirefu. Wilson anawaniwa na Klabu za Premier League, Bundesliga na La Liga. ***(Mirror)***

### MIGNOLET AWINDWA B'MOUTH

BOURNEMOUTH inataka kumsajili kipa wa Liverpool, Simon Mignolet, 31, baada ya Mbelgiji huyo kushindwa kufurukuta katika kikosi cha kwanza Anfield. ***(Sun)***

# Dunia kulipaisha soka Z'bar duniani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MGOMBEA Urais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ame Abdalla Dunia, ametaja vipaumbele nane endapo atachaguliwa kuwa rais wa shirikisho hilo, huku akieleza anataka kulifanya soka la visiwani hapa kuwa familia moja na mashirikisho mengine duniani hususan Fifa.

Dunia alianika mkakati wake huo mbele ya waandishi wa habari jana katika kampeni zake kuelekea uchaguzi wa shirikisho hilo unaotarajiwa kufanyika Juni 2, mwaka huu na kueleza moja ya kipaumbele chake itakuwa ni kuboresha ushirikiano wa kidiplomasia na mashirikisho mengine ikiwamo Caf (Shirikisho la Soka Afrika), Cecafa (Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati) pamoja Fifa (Shirikisho la Soka duniani).

Kadhalika, alisema ili kuwe na soka la nidhamu na lenye mafanikio, lazima kuwa na viongozi bora ambao watafuata sheria, kanuni na katiba ya shirikisho hilo.

Alisema uongozi wake hautakuwa wa mazoea badala yake utakuwa ni wakufuata misingi ya sheria na katiba ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Pia, alisema kipaumbele cha pili atahakikisha anasimamia vema ligi ya vijana kwa ngazi ya mikoa yote hususan ya vijijini ambayo ligi hiyo inasuasua ikilinganishwa na mjini.

Alisema sambamba na hilo, kipaumbele cha tatu atahakikisha kunakuwapo na mkurugenzi wa benchi la ufundi katika kila mkoa ili kuziandalia mazingira mazuri timu hizo.

Aidha, alisema kipaumbele kingine katika uongozi wake atahakikisha anaboresha ushirikiano na waamuzi ikiwamo mikakati ya kuwapunguzi majukumu mengi kwa kuwapo waamuzi watakaochezeha Ligi Kuu na kanda, wilaya pamoja na mikoa.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 38 | 29 | 6 | 3 | 77 | 15 | 93 |
| 2. Yanga | 38 | 27 | 5 | 6 | 56 | 27 | 86 |
| 3. Azam | 38 | 21 | 12 | 5 | 54 | 21 | 75 |
| 4. Kinondoni MC | 38 | 13 | 16 | 9 | 40 | 25 | 55 |
| 5. Mtibwa Sugar | 38 | 14 | 8 | 16 | 36 | 34 | 50 |
| 6. Lipuli | 38 | 12 | 13 | 13 | 32 | 40 | 49 |
| 7. Mbeya City | 38 | 13 | 9 | 16 | 38 | 39 | 48 |
| 8. Coastal Union | 38 | 11 | 15 | 12 | 32 | 42 | 48 |
| 9. Ndanda | 38 | 12 | 12 | 14 | 25 | 37 | 48 |
| 10. JKT Tanzania | 38 | 11 | 14 | 13 | 28 | 34 | 47 |
| 11. Alliance | 38 | 12 | 11 | 15 | 33 | 42 | 47 |
| 12. TZ Prisons | 38 | 11 | 13 | 14 | 30 | 31 | 46 |
| 13. Singida United | 38 | 11 | 13 | 14 | 30 | 39 | 46 |
| 14. Biashara United | 38 | 11 | 12 | 15 | 30 | 35 | 45 |
| 15. Ruvu Shooting | 38 | 11 | 12 | 15 | 35 | 43 | 45 |
| 16. Mbao | 38 | 11 | 12 | 15 | 27 | 41 | 45 |
| 17. Mwadui | 38 | 12 | 8 | 18 | 47 | 52 | 44 |
| 18. Kagera Sugar | 38 | 10 | 14 | 14 | 33 | 43 | 44 |
| 19. Stand United | 38 | 12 | 8 | 18 | 38 | 50 | 44 |
| 20. African Lyon | 38 | 4 | 11 | 23 | 23 | 54 | 23 |

# SIMBA YATAKA OFA YA KAGERE MEZANI

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

UONGOZI wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba umesema hakuna ofa rasmi iliyofika mezani kwao kwa ajili ya kutaka kumnunua mshambuliaji wao Mnyarwanda Meddie Kagere na kama wapo wanaomhitaji walete barua mezani.

**Kagere alitua Simba mwaka jana akitokea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Kenya, Gor Mahia na sasa amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake.**

Taarifa zinazosambaa katika mitandao zinaeleza kuwa mabingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika, Zamalek wameleta ofa ya kutaka kumnunua Kagere kwa dau la Dola za Marekani 450,000 zaidi ya Sh. bilioni moja za Tanzania, huku wakitaka kumlipa mshahara wa Dola za Marekani 18,000 (Sh. milioni 41.2) za Bongo kwa mwezi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema jana ofa zinazozungumzwa kuhusu Kagere ni za "mtaani" kwa sababu hakuna klabu iliyowasilisha barua rasmi.

Magori amesema klabu yake haiko tayari kufanya mazungumzo yoyote kupitia mawasiliano ya mdomo au kwa njia ya simu kwa sababu huo si utaratibu wa kiofisi.

"Tunapenda kuwataka wote wanaohitaji kusajili mchezaji wa Simba kutuandikia barua, barua itakapofika mezani tutaifanyia kazi kulingana na mapendekezo kutoka katika benchi la ufundi," alisema kiongozi huyo.

Wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed "Mo" Dewji, alisema klabu hiyo imejiandaa kushindana katika soko la usajili Afrika kwa sababu malengo yao ni kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa barani hapa.

Dewji alisema pia uamuzi wa mchezaji kuuzwa, kununuliwa au kuachwa utafanyika kwa kuzingatia ripoti ya ufundi itakayotolewa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Patrick Aussems na si nje ya hapo.

**WENGER KAZINI...**



Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, akimtoka mshindi wa zamani wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] na Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, katika mechi ya hisani juzi iliyopigwa Bordeaux, Ufaransa. **PICHA: MTANDAO**

# Motisun Group yaipiga tafu Taifa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Motisun Group imetangaza kuihudumia malazi na chakula Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) ambayo inatarajia kuingia kambini Jumamosi ili kuanza maandalizi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) zitakazofanyika nchini Misri baadaye mwezi ujao.

Katika fainali za Afcon ambazo zitachezwa kuanzia Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu, Taifa Stars imepangwa Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na majirani zao Harambee Stars ya Kenya.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Motisun Group, Subhash Patel, alisema kampuni yake imefikia uamuzi wa kuisaidia Taifa Stars kutokana na mafanikio waliyoyapata mwaka huu baada ya kushindwa kufuzu kwa kipindi cha miaka 39.

Patel alisema Watanzania wote wanatakiwa kujivunia kwa mafanikio ambayo wameyapata Taifa Stars mwaka huu, kwa sababu haifahamiki tena ni mwaka gani timu hiyo itafanikiwa kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo zinazoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

" Miaka 39 ni mingi sana, mara ya mwisho tumefuzu wakati ule Mzee wetu Tenga (Leodegar) alikuwa kijana, sasa ni mzee kama mimi, tuisaidie jamani, wakiwa pale watatumia vifaa kama ukumbi, kompyuta kujifunza mambo mbalimbali ili wakienda huko Cairo wakafanye vizuri, wakalitangaze jina la Tanzania, miaka 39 sio mchezo, Taifa Stars ni fahari ya Watanzania wote," alisema Patel.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema mchango huo uliotolewa na kampuni hiyo ni mkubwa kwa shirikisho lake ambalo bado hawajapokea fedha za maandalizi kutoka Caf na serikalini pia.

Karia alisema uamuzi uliofanywa na Motisun Group ni "mzito sana" katika kipindi hiki ambacho Taifa Stars inahitaji kujiandaa kabla ya kuelekea katika kambi nyingine huko Misri.

"Mzee wetu Subhash ameamua kuanza yeye kuisaidia Taifa Stars, timu itakaa pale Whitesands na itapata huduma zote muhimu kwa gharama ya Motisun Group, baadaye itaelekea Misri kuendelea na kambi yake huko ili kujiimarisha zaidi," alisema Karia.

# Michezo

Alhamisi Mei 30, 2019

Nipashe






Salah kuitungua Spurs kutibu jeraha la Madrid UKURASA 30




Kipa wa Simba, Deogratius Munishi 'Dida', akimwendesha dereva bodadoda aliyejitokeza kuipokea jana katika msafara wa timu hiyo, wakati ikitokea Morogoro ilipokabidhiwa ubingwa wao wa Ligi Kuu Bara juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mapokezi Simba yaweka rekodi

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Bara, Simba wamepokelewa kishujaa jana na mashabiki na wanachama wa klabu hiyo, wakati wakitokea mkoani Morogoro na kombe lao walilokabidhiwa wakati wakihitimisha msimu wa 2018/219 kwa sare tasa dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri juzi.

Katika mapokezi hayo yaliyoanzia Chalinze kabla ya msafara mkubwa kuanzia Kibaha, mashabiki hao jana walijitokeza kwa wingi wakiwa na magari na bodaboda kwa wingi na kuwafanya baaadhi ya wachezaji akiwamo kipa, Deogratius Munishi 'Dida' kushuka na kuonyesha uwezo kuendesha bodadoda.

Baada ya kufika Kibaha Stand, wachezaji walipanda kwenye gari la wazi wakiwa na kombe lao wakiwaonyesha mashabiki ambao walijitokeza sehemu mbalimbali barabarani katika maeneo ya Kibamba, Kimara, Mbezi, Ubungo mpaka Manzese kabla ya kuishia makao makuu ya klabu hiyo mtaa wa Msimbazi, Kariakoo.

Baada ya kutinga, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alikabidhiwa kombe na nahodha msaidizi, Mohamed Hussein 'Tshabalala' kabla ya msafara kuunganisha safari kupitia Magomeni na kuishia maeneo ya Sea Escape ilipo kambi ya wachezaji waliposhuka na kuanza kujinafasi kwa raha zao.

# TFF YAKIRI KUVURUNDA SAKATA KAGERA SUGAR

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Takwimu Nipashe zaisaidia, yairudisha kucheza mchujo dhidi ya Pamba, yaishusha daraja Stand...

UMAKINI wa takwimu za Gazeti la Nipashe sambamba na zile za Azam Tv, zimesaidia kuinusuru Kagera Sugar kushuka daraja kufuatia Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), kutazana upya na kubaini iliboronga katika takwimu zake, hivyo kuirejesha timu hiyo ya mkoani Kagera kucheza mechi ya mchujo ['play off'] dhidi ya Pamba ya Mwanza, ambayo itaamua kuendelea kucheza Ligi Kuu msimu ujao ama la.

Kwa mujibu wa takwimu za Nipashe ambalo limekuwa makini tangu kuanza kwa Ligi Kuu msimu huu, zinaonyesha Kagera Sugar ipo katika nafasi 18 ikiwa na alama 44 sawa na Stand United ambayo ipo nafasi ya 19, lakini timu hiyo ya kutoka mashamba ya miwa mkoani Kagera ikiwa na mabao yakufunga 33 na 43 ya kufungwa (tofauti ikiwa ni hasi 10).

Lakini Stand United ya Shinyanga yenyewe ina mabao ya kufunga 38 na 50 ya kufungwa [tofauti ikiwa ni hasi 12], hata hivyo, katika msimamo wa TFF ulikuwa ukionyesha timu hizo zililingana kila kitu na tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa ilikuwa ni hasi 11 (-11), jambo ambalo halikuwa sahihi, hivyo ikabatilisha uamuzi wake wa awali wa kuishuka Kagera Sugar.

**Juzi baada ya msimu wa Ligi Kuu Bara kumalizika, TFF kupitia Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Boniface Wambura, ilitangaza kuwa kutokana na timu hizo kulingana kila kitu katika takwimu, Kagera Sugar itashuka daraja kwa kuwa Stand United ilikuwa na matokeo mazuri timu hizo zilipokutana zenyewe kwa zenyewe (head to head).**

Hata hivyo, akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Wambura alisema kuna makosa ya kitakwimu yamebainika kufanyika katika kuandaa msimamo ambao ulisambazwa katika vyombo mbalimbali hapo juzi [si kwa Nipashe kwani lilikuwa likijiandalia takwimu zake kadri ligi ilivyokuwa ikiendelea].

Wambura alisema sasa rasmi Kagera Sugar imerejea katika ligi hiyo ya juu Tanzania Bara na itacheza mechi ya hatua ya mchujo 'play off' dhidi ya Pamba ya jijini Mwanza wiki ijayo.

"Ofisi yangu itampa adhabu ofisa ambaye amehusika na upotoshwaji huu wa takwimu," alisema Wambura.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, aliliambia gazeti hili jana kuwa amesikitishwa na Idara ya Takwimu ya Bodi ya Ligi kwa kufanya makosa ambayo yameidhalilisha nchi ndani na nje ya Tanzania.

Maxime alisema kwa upande wake hakuwa na wasiwasi wowote kwa sababu walikuwa wanaamini takwimu walizokuwa nazo na walikuwa wanasubiri taarifa rasmi kutoka TFF ili watangaze uamuzi wao.

"Kilichotokea jana (juzi) ni jambo la aibu sana, nashukuru sisi hatufanyi vitu vya kubahatisha, takwimu zetu ziko sahihi na hata kichwani ninazo ninaweza kukwambia, kuna vitu tunahitaji kubadilisha ili twende sawa, tusifanye kazi kwa mazoea, tunaidhalilisha nchi," alisema nahodha huyo wa zamani wa Taifa Stars.

Taarifa ambazo gazeti hili imezipata ni kuwa kiongozi huyo anayedaiwa kuhusika na idara hiyo ya takwimu (jina tunalo) ajira yake imekalia "kuti kavu".


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >